RUWAZA ZA MATUMIZI YA LUGHA NA ATHARI ZAKE KWA UMILISI WA LUGHA ZUNGUMZI YA KISWAHILI: MFANO WA WANAFUNZI WA SHULE ZA UPILI WILAYANI SIAYA

NA

ADIKA KEVOGO STANLEY

EGERTON UNIVERSITY LIBRARY

Ripoti iliyowasilishwa katika idara ya Fasihi, Lugha na Isimu kutosheleza baadhi ya mahitaji ya shahada ya uzamili (Kiswahili) katika Chuo Kikuu cha Egerton

CHUO KIKUU CHA EGERTON

2008/73074

JULAI, 2007

UNGAMO NA IDHINI

UNGAMO

Ripoti hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada yoyote katika Chuo Kikuu chochote.

Adika, K. S. Sahihi ..... Tarehe 18/07/2007

IDHINI

Ripoti hii imewasilishwa katika Idara ya Fasihi, Lugha na Isimu ya Chuo Kikuu cha Egerton kwa idhini yangu kama msimamizi aliyeteuliwa rasmi na Chuo Kikuu.

Dkt. Aswani, B. Sahihi ..... Tarehe 18/07/2007

HATILIZI

Haki zote zimehifadhiwa. Hakuna ruhusa ya kuiga, kunakili, kuchapisha, kutafsiri au kutoa sehemu ya ripoti hii au ripoti nzima kwa njia yoyote ile bila barua ya ithini kutoka kwa mwandishi au Chuo Kikuu cha Egerton.

TABARUKU

Nawatabarukia kazi hii kipenzi mamangu Florence Uside Kevogo, aliyejinyima si haba kugharamia elimu yangu na laazizi Sellah Nasimiyu Adika kwa subira yake kubwa.

SHUKRANI

Uchunguzi na hatimaye uandishi wa Ripoti hii haungewezekana bila msaada, himizo, changamoto na mawaidha kutoka kwa watu mbalimbali. Waama, itakuwa ni wizi wa fadhila ikiwa sitamshukuru Mwenyezi Mungu pamoja na wale wote walionisaidia kuiandaa na kuikamilisha kazi hii. Tangu nilipoanza uchunguzi huu, nimekutana na kupata misaada kutoka kwa wanafunzi, wazazi na walimu, wahadhiri, wanazuoni, wataalamu wa Isimu na wapenzi mbalimbali wa Kiswahili.

Kwanza kabisa shukrani zangu za dhati zimwendee msimamizi wangu, Dkt. Aswani, B. wa Chuo Kikuu cha Egerton kwa kunipa ushauri na maoni mengi ya kitaaluma. Uvumilivu na kujitoa mhanga kwake katika kuisoma na kuikosoa miswada yangu kulinipa ari na motisha wa kuendelea hadi tamati. Mawaidha yake yalisaidia kuupa mwelekeo uchunguzi huu.

Ningependa pia kumshukuru mwenyekiti wa Idara ya Fasihi, Lugha na Isimu, Dkt. Wako, kwa himizo na nasaha adimu. Aidha, nawashukuru wahadhiri idarani ambao nilijifunza mengi kutoka kwao ama kutokana na kozi walizonifundisha, kuzungumza nao ana kwa ana au kusoma makala na maandishi yao mbalimbali yanayohusu lugha ya Kiswahili na Isimu kwa jumla. Hawa ni: Dkt. Catherine Kitetu, Dkt. Beja, K. S., Dkt. Furaha Tchai, Dkt. Ogola James, Dkt. Kimemia John, Dkt. Yieke, Dkt. Walunywa, Dkt. Mukuthuria, Bw. Mayaka Gwachi, Bw. Nabea, Bi. Liguyani, Bi. Wandera, S. na Bi. Juma.

Ama kwa hakika ukusanyaji wa deta wilayani Siaya usingelifanikishwa bila msaada wa Ofisi ya Elimu wilayani na shule tano shiriki. Kwa sababu hiyo basi, ningependa kutoa shukurani za pekee kabisa kwa Walimu Wakuu, walimu wa lugha na wanafunzi wa shule za upili zifuatazo: Nyagondo, Agoro Oyombe, Ng'iya, Barding na Horace Ongili.

Ninaishukuru familia yangu yote, yaani mamangu mzazi Florence Uside Kevogo kwa kunitunza, kunilea kwa mkono wake mmoja na kunisomesha. Ndugu zangu Hudson na Mkewe,

Alex, Nikki, James na dada zangu Dainah, Pauline, Faith na Naomi kwa uvumilivu na upendo mkubwa walionionyesha wakati nikiandika kazi hii. Namshukuru mke wangu, Bi. Nasimiyu Sellah kwa kunivumilia na kunihimiza kuendelea kushika kalamu na karatasi licha ya pingamizi nyingi.

Itakuwa muhali kwangu kusahau kutoa shukrani zangu kwa wanafunzi wenzangu Riro Samuel, Ojwang' Stephen, Kevogo Alex, Kirema Severina, Minyori Matthew, Makori David na Wambua David kwa ushirika, changamoto na mijadala iliyonipa ari na msukumo wa kuichunguza mada hii.

Nawashukuru mabwana Mwangi na Onzere walioipiga chapa miswada ya ripoti hii. Mungu awakirimie baraka na heri njema.

Ijapokuwa nimejaribu kutoa shukrani zangu za dhati kwa kila aliyeniauni kwa namna moja au nyingine, ni vigumu kuwataja wote walionifadhili. Kwa hivyo, wale ambao sijawataja ningependa kuwashukuru kwa pamoja kwa kila aina ya msaada niliopata katika shughuli zangu za utafiti. Sina budi kukiri kwamba bila msaada na mchango wenu kazi hii haingekamilika.

IKISIRI

Utafiti huu ulihusu ruwaza za matumizi ya lugha na athari zake kwa umilisi wa lugha zungumzi ya Kiswahili. Jambo hili lilitokana na sababu kwamba umilisi wa kutumia lugha zungumzi fasaha ya Kiswahili katika shughuli za kila siku ulikuwa tatizo miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili. Hali hii ilihusishwa na athari za ruwaza za matumizi ya lugha mbalimbali miongoni mwao. Utafiti huu ulidhamiriwa kubainisha ruwaza za matumizi ya lugha na athari za ruwaza hizo kwa matamshi sahihi ya Kiswahili miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili wilayani Siaya. Tulikuwa na makisio kuwa wanafunzi wa shule za upili wilayani Siaya wana ruwaza mahususi za matumizi ya lugha zungumzi zinazoweza kutambulishwa na kwamba ruwaza hizo zinaathiri matamshi yao katika lugha ya Kiswahili. Jumla ya wanafunzi mia moja na walimu kumi wa somo la Kiswahili walishirikishwa. Nadharia ya usemi ya matumizi na ujifunzaji wa lugha ya pili pamoja na mtazamo wa Kiisimujamii wa Fishman, Hudson na Fasold ndio ulioongoza utafiti huu. Deta ilikusanywa kwa kutumia hojaji, mahojiano, mjarabu, mijadala na uchunguzi shiriki. Deta yenyewe ilikuwa matokeo ya mjarabu, idadi ya makosa ya kimatamshi katika mijadala, jumla ya lugha wanazozungumza wanafunzi na walimu, maelezo kuhusu matumizi ya lugha katika mawanda mbalimbali, nyumbani na shuleni. Deta hizi zilichanganuliwa kwa kutumia majedwali, misambao ya umaratokezi na asilimia. Matokeo yalidhihirisha kuwa wanafunzi waliteua na kutumia Lugha ya Mama na Sheng kuliko Kiswahili – hali iliyolemaza usahihi wao kimatamshi katika Kiswahili. Kwa hivyo, utafiti huu umechangia kubainisha athari za ruwaza za matumizi ya lugha kwa ujifunzaji wa lugha zungumzi ya Kiswahili na kutoa mapendekezo ambayo yakizingatiwa yanaweza kuboresha lugha zungumzi ya Kiswahili.

ABSTRACT

This study was about language use patterns and their effect on the acquisition of oral communication competence in standard Kiswahili. Competence in oral communication in Kiswahili for every day life was observed to be a problem among secondary school students. This was attributed to the prevalent language use patterns among learners which affected their acquisition of oral communication competence. The objectives of this research were: to investigate the prevalent language use patterns and their effect on the pronunciation of standard Kiswahili amongst secondary school students in Siaya District. Our hypotheses were that secondary school students in Siaya District have identifiable language use patterns and that these patterns affected their pronunciation in standard Kiswahili. A total of one hundred secondary school students together with ten Kiswahili language teachers participated in the study. It was guided by The Discourse Theory of Second Language Use and Learning. Also employed were sociolinguistic perspectives by Fishman, Hudson and Fasold. Data was collected through interviews, questionnaires, tests, debates and participant observation. Test results, pronunciation mistake frequencies in debates, student and teacher language repertoires and self reports on language use at home and school constituted our data. The data was classified and analyzed using tables, frequency distribution tables and percentages. Results of this study revealed that more often than not students chose and used Mother Tongue languages and Sheng in their speech. This denied them valuable opportunities to practice oral communication in standard Kiswahili thus resulting in poor pronunciation in the same. This study has helped describe the prevalent language use patterns and their effect on the acquisition of oral communication competence in Kiswahili. It has also recommended ways of improving oral communication competence in Kiswahili with particular reference to pronunciation.

YALIYOMO

UNGAMO NA IDHINI ii

HATILIZI iii

TABARUKU iv

SHUKRANI v

IKISIRI vii

ABSTRACT viii

YALIYOMO ix

MAELEZO YA VIFUPISHO xii

ORODHA YA MAJEDWALI xiii

SURA YA KWANZA: UTANGULIZI 1

1.1 Utangulizi 1

1.2 Usuli wa Mada 1

1.3 Mada ya Utafiti 4

1.4 Madhumuni ya Utafiti 4

1.5 Nadharia tete za Utafiti 4

1.6 Umuhimu wa Utafiti 4

1.7 Upeo wa Utafiti 7

1.8 Hitimisho 8

1.9 Maelezo ya Istilahi 8

SURA YA PILI: YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA YA UTAFITI 11

2.1 Utangulizi 11

2.2 Ruwaza za Matumizi ya Lugha Nchini Kenya 11

2.3 Ujifunzaji wa Lugha ya Pili 13

2.4 Tafiti Kuhusu Lugha Zungumzi 16

2.5. Matamshi Katika Kiswahili 18

2.6 Misingi ya Nadharia 20

2.7 Hitimisho 21

SURA YA TATU: MBINU ZA UTAFITI 23
3.1 Utangulizi 23
3.2 Njia za Utafiti 23
3.3 Jumuiya 23
3.4 Uteuzi wa Sampuli 24
3.5 Ukusanyaji wa Deta 25
3.6 Vifaa vya Ukusanyaji wa Deta 27
3.6.1 Hojaji 27
3.6.2 Mahojiano 29
3.6.3 Mjarabu 29
3.6.4 Mijadala 30
3.6.5 Uchunguzi Shiriki 31
3.7 Uchanganuzi wa Deta 31
3.8 Hitimisho 32
SURA YA NNE: UCHANGANUZI NA UFASIRI WA DETA 33
4.1 Utangulizi 33
4.2 Ruwaza za Matumizi ya Lugha 33
4.2.1 Jumla ya Lugha za Wanafunzi na Walimu 33
4.2.2 Matumizi ya Lugha Katika Mawanda Mbalimbali 34
4.2.3 Matumizi ya Lugha Nyumbani 36
4.2.4 Lugha ya Usomaji wa Magazeti na Usikilizaji wa Redio 41
4.2.5 Lugha ya Uandishi wa Barua 42
4.2.6 Matumizi ya Lugha Shuleni 43
4.2.6.1 Lugha ya Mazungumzo na Mwalimu 44
4.2.6.2 Lugha ya Mazungumzo na Wanafunzi Kutoka Shule Nyingine 45
4.2.6.3 Lugha Katika Majadiliano ya Mada na Masomo Mbalimbali 45
4.2.6.4 Matumizi ya Lugha Mahali Mbalimbali mwa Maingiliano Shuleni 46
4.2.6.5 Sera ya Lugha Shuleni 48
4.3 Uzungumzi wa Wanafunzi 54
4.3 1 Umilisi wa Kutumia Lugha Zungumzi ya Kiswahili 55
4.3.2 Motisha wa Kutumia Kiswahili 56
4.3.3 Uhamasishaji 57

4.3.5 Lugha Zungumzi Katika Mitihani ya Kitaifa 58
4.4 Athari za Matumizi ya Lugha Zungumzi kwa Matamshi Fasaha ya Kiswahili 59
4.4.1 Tathmini ya Matamshi ya Wanafunzi 59
4.4.2 Mjarabu 60
4.4.3 Mijadala 64
4.5 Majadiliano 68
4.5.1 Jumla ya Lugha za Wanafunzi na Walimu 68
4.5.2 Lugha Katika Mawanda Mbalimbali 70
4.5.3 Matumizi ya Lugha Nyumbani 71
4.5.4 Lugha ya Usomaji wa Magazeti na Usikilizaji wa Redio 73
4.5.5 Lugha ya Uandishi wa Barua 76
4.5.6 Matumizi ya Lugha Shuleni 77
4.5.7 Uzungumzi wa Wanafunzi 80
4.5.8 Athari za Matumizi ya Lugha Zungumzi kwa Matamshi Fasaha ya Kiswahili 83
4.6 Hitimisho 89
SURA YA TANO: MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO 90
5.1 Utangulizi 90
5.2 Muhtasari wa Matokeo Muhimu 90
5.3 Hitimisho 92
5.4 Mapendekezo 93
5.5 Mapendekezo ya Utafiti Zaidi 94
MAREJELEO 95
KIAMBATISHO A: HOJAJI KWA WANAFUNZI 100
KIAMBATISHO B: HOJAJI KWA WALIMU WA LUGHA 106
KIAMBATISHO C: MJARABU 110
KIAMBATISHO D : MWONGOZO WA MAHOJIANO NA MWALIMU 114
KIAMBATISHO E: MFUMO WA UAINISHAJI WA MATAMSHI 115
KIAMBATISHO F: SHULE ZA UPILI WILAYANI SIAYA 116

MAELEZO YA VIFUPISHO

L1	Lugha ya Kwanza. Pia Lugha ya Mama au Lugha ya uzawa katika kazi hii.
KIE	Kenya Institute of Education (Taasisi ya Elimu nchini Kenya).
KCSE	Kenya Certificate of Secondary Education (Mtihani wa kitaifa wa kidato cha nne).
CKRC	Constitution of Kenya Review Commission (Tume ya Marekebisho ya Katiba Nchini Kenya).

ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali 1 Sampuli 25

Jedwali 2 Matumizi ya Lugha Katika Mawanda Mbalimbali 35

Jedwali 3 Matumizi ya Lugha Katika Mazungumzo Nyumbani 37

Jedwali 4 Umilisi wa Wazazi Kimazungumzo 37

Jedwali 5 Vikwazo Kuhusu Matumizi ya Lugha Nyumbani 39

Jedwali 6 Lugha Zisizopendekezwa 40

Jedwali 7 Usomaji wa Magazeti na Majarida 41

Jedwali 8 Usikilizaji wa Vipindi vya Redio 42

Jedwali 9 Lugha ya Uandishi wa Barua 43

Jedwali 10 Lugha ya Mazungumzo na Mwalimu 44

Jedwali 11 Lugha ya Mazungumzo na Wanafunzi Kutoka Shule Nyingine 45

Jedwali 12 Lugha Katika Majadiliano ya Mada na Masomo Mbalimbali 46

Jedwali 13 Matumizi ya Lugha Mahali Mbalimbali mwa Maingiliano Shuleni 48

Jedwali 14 Uzingatiaji wa Sera ya Lugha Shuleni 54

Jedwali 15 Lugha Zilizopendekezwa kwa Mawasiliano Shuleni 54

Jedwali 16 Manufaa ya Kuwa na Umilisi Kutumia Lugha Zungumzi ya Kiswahili 57

Jedwali 17 (a) - (e) Matokeo ya Mjarabu 61

Jedwali 18 (a) - (e) Makosa ya Kimatamshi Yaliyotokana na Mijadala 65

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI

1.1 Utangulizi

Katika sura hii tumeshughulikia utangulizi wa utafiti ambapo tumejadili usuli wa mada, mada ya utafiti, madhumuni ya utafiti, nadharia tete za utafiti, umuhimu wa utafiti na upeo wa utafiti.

1.2 Usuli wa Mada

Kiswahili kina jukumu muhimu la kuwaunganisha wakenya ambao wanazungumza zaidi ya lugha arobaini za kikabila (Whiteley, 1974; CKRC, 2000: 95; Webb, V. & Kembo-Sure, 2000: 13; Kimemia, 2001). Njia moja ya kuhakikisha kuwa lugha ya Kiswahili inatekeleza jukumu hili nchini ni kuisambaza kwa kuifundisha shuleni kama ilivyo sasa na kuhakikisha inatumiwa kwa ufasaha katika miktadha mbalimbali.

Nchini Kenya, watu wengi hutumia lugha tatu - Kiingereza, Kiswahili, Lugha ya Kwanza - katika shughuli zao za mawasiliano (Mkilifi, 1987). Hali hii huzua ruwaza mbalimbali za matumizi ya lugha. Ruwaza za matumizi ya lugha ni uteuzi na matumizi ya lugha mbalimbali ambazo ni sehemu ya 'ghala la lugha' za mzungumzaji katika mawasiliano na shughuli za kimtagusano.

Ijapokuwa sera za lugha katika shule nyingi husisitiza matumizi ya Kiingereza na Kiswahili, matumizi ya lugha zingine kama vile ya kwanza na Sheng huibuka miongoni mwa wanafunzi. Ni dhahiri kwamba wanafunzi wengi wa shule za upili nchini Kenya hutumia Kiswahili, Kiingereza, lugha za kwanza na kwa kiwango fulani Sheng katika mawasiliano yao (Jumba, 1994; Kaniu, 2003; Kimemia, 2001). Katika hali ya wingilugha kama hii, ubadilishaji

msimbo na kuchanganya ndimi ni mambo ya kawaida. Ubadilishaji msimbo unaotumia zaidi ya lugha mbili shuleni unadhihirisha ruwaza mahususi za matumizi ya lugha. Ruwaza za matumizi ya lugha kama hizi zinaathiri umilisi na ujifunzaji wa lugha zungumzi fasaha ya Kiswahili hasa kwa upande wa matamshi.

Mbali na kupewa nafasi duni, matumizi ya Kiswahili yanaingiliwa na lugha hizi zingine hasa kwa upande wa matamshi, uteuzi wa msamiati na hata sarufi. Katika mazungumzo yao, wanafunzi wengi walikuwa makini kuzungumza Kiingereza kwa ufasaha ilhali hawakuonyesha kujali walipofanya makosa na kutatizika walipozungumza Kiswahili. Hali hii iliathiri ujifunzaji wa Kiswahili miongoni mwa wanafunzi hasa ikizingatiwa kwamba ni somo la kutahiniwa na lugha sambazi miongoni mwa wakenya.

Umilisi wa lugha ya pili hutegemea mazoezi na matumizi yake kwa wingi katika miktadha mbalimbali (Musau na Chacha, 2001). Hili linatokana na ukweli kwamba binadamu hujifunzą lugha vizuri kwa kuitumia. Isitoshe, jukumu muhimu la ujifunzaji wa lugha ni mawasiliano yanayofaa katika muktadha. Kwa hivyo, mazungumzo hukuza ufasaha wa lugha zungumzi na ujasiri wa kuzungumza. Kutokana na mantiki hii, wanafunzi wa Kiswahili kama lugha ya pili hawana budi kujihusisha katika shughuli za kimtagusano wakitumia Kiswahili fasaha.

Kama lugha ya taifa na somo la lazima linalofundishwa katika shule za msingi na upili, umilisi wa lugha zungumzi fasaha ya Kiswahili ni muhimu. Ili kuafikia umilisi unaohitajika, ni lazima wanafunzi wahimizwe kutumia Kiswahili fasaha shuleni na nje. Isitoshe, shule zitenge wakati kwa shughuli za kimtagusano kama vile mijadala, hotuba na mazungumzo ili kuwawezesha wanafunzi kufanya mazoezi ya yale waliyofundishwa, waweze kujitathmini na kuulinganisha umilisi wao.

Tafiti za awali (Atsenga, 2002; Kaniu, 2003) zimedhihirisha kwamba hali ya wingilugha inaathiri ujifunzaji wa lugha ya pili. Lugha tatu au nne zilizotumiwa katika shule nyingi za upili zilisheheni ruwaza mahsusi kimatumizi. Utafiti huu ulichunguza ruwaza za matumizi ya lugha na kubainisha athari za ruwaza hizo kwa matamshi fasaha ya Kiswahili miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili wilayani Siaya.

Ijapokuwa ufasaha wa lugha zungumzi hutekeleza majukumu muhimu kiuchumi na kijamii miongoni mwa wanafunzi wanaofuzu kutoka shule za upili, ufasaha wa kutumia Kiswahili ni tatizo. Wanafunzi wengi wa shule za upili wanakumbwa na matatizo ya kimatamshi, uteuzi wa msamiati, sarufi na kuingiliana kwa lugha (KIE, 2002). Hali hii inaathiri mawasiliano - baadhi ya wazungumzaji wanaeleweka kwa shida ilhali wengine hawaeleweki kamwe.

Utafiti huu, hata hivyo,ulijishughulisha tu na athari za kimatamshi zitokanazo na ruwaza za matumizi ya lugha zungumzi miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili. Hili lilitokana na ukweli kwamba kuna uhusiano mkubwa baina ya matamshi na hijai katika Kiswahili. Hali hii humfanya mwanafunzi kuandika maneno ya Kiswahili jinsi anavyoyatamka. Kwa hivyo, matamshi huathiri sio tu mazungumzo bali stadi zingine za lugha kama usomaji, uandishi, na usikilizaji pia.

Iwapo Kiswahili fasaha kitapewa nafasi kubwa katika maingiliano shuleni, matatizo haya yatakomeshwa na kuzalisha matumizi ya lugha zungumzi fasaha ya Kiswahili. Hata hivyo, tatizo linalojitokeza katika matumizi ya lugha zungumzi miongoni mwa wanafunzi ndilo lililouchochea na kuupa msukumo uchunguzi huu kubainisha ruwaza za matumizi ya lugha shuleni na athari zake kwa umilisi wa lugha zungumzi fasaha ya Kiswahili.

1.3 Mada ya Utafiti

Licha ya kwamba Kiswahili ni lugha ya taifa na ni somo la lazima linalofundishwa katika shule za msingi na upili, umilisi wa kutumia lugha zungumzi fasaha ya Kiswahili katika shughuli za kila siku umekuwa tatizo. Tatizo hili hujitokeza kimatamshi, kisarufi, na kimaana. Hali hii ndiyo iliyopelekea utafiti huu kuchunguza ruwaza za matumizi ya lugha na athari zake kwa umilisi wa lugha zungumzi fasaha ya Kiswahili miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili.

1.4 Madhumuni ya Utafiti

Utafiti huu ulilenga kuyaafikia madhumuni yafuatayo:-

(i) Kubainisha ruwaza za matumizi ya lugha zungumzi miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili wilayani Siaya.

(ii) Kubainisha athari za ruwaza za matumizi ya lugha zungumzi kwa matamshi fasaha ya Kiswahili miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili wilayani Siaya.

1.5 Nadharia tete za Utafiti

Uchunguzi huu ulikuwa na makisio yafuatayo kwa maswali ya utafiti:

(i) Wanafunzi wa shule za upili katika wilaya ya Siaya wana ruwaza mahususi za matumizi ya lugha zungumzi zinazoweza kutambulishwa.

(ii) Ruwaza za matumizi ya lugha zungumzi miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili wilayani Siaya zinaathiri matamshi yao katika lugha ya Kiswahili.

1.6 Umuhimu wa Utafiti

Uwezo wa kuzungumza kwa ufasaha ni tunu muhimu katika maisha ya binadamu. Ni dhahiri kwamba usikilizaji bora na uzungumzaji fasaha hutoa mchango mkubwa katika

kuendeleza stadi za kusoma na kuandika katika ujifunzaji wa lugha yoyote ile. Hali hii ilitupatia msukumo kuchunguza ruwaza za matumizi ya lugha na athari zake kwa umilisi wa lugha zungumzi ya Kiswahili miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili wilayani Siaya.

Utafiti huu ni mchango katika juhudi za kuhimiza wanafunzi wa shule za upili kutumia Kiswahili fasaha katika mazungumzo. Matumizi kama haya yatainua kiwango chao cha umilisi wa kutumia Kiswahili fasaha katika shughuli zao za kila siku. Jambo hili ni la kimsingi hasa inapozingatiwa kuwa Kiswahili ni lugha ya pili kwa wanafunzi wengi. Isitoshe, kama lugha ya pili, inakabiliwa na maingiliano ya lugha na vilugha vinginevyo ambavyo ni sehemu ya 'ghala la lugha' la mwanafunzi.

Mukuthuria (2001) anashikilia kwamba mielekeo potovu dhidi ya lugha ya Kiswahili haiwezi kufifishwa kwa kulazimisha watu kutumia lugha hii bali ni kwa juhudi za kielimu na utafiti wa juu. Anasisitiza kuwa kwa kufanya hivi, wale wasioonea Kiswahili fahari watabadilisha mielekeo yao. Kwa kubainisha ruwaza za matumizi ya lugha na athari zake kwa umilisi wa Kiswahili zungumzi, utafiti huu umechangia kufifisha mielekeo potovu na hasi dhidi ya lugha zungumzi ya Kiswahili.

Matumizi na ujifunzaji lugha zungumzi fasaha, hususan mitindo na sajili mbalimbali, humwadabisha mwanafunzi kuhusu matumizi ya Kiswahili kutegemea muktadha, kaida na miiko katika jamii za Kiafrika na Kimataifa. Hili linatokana na uhalisia kwamba Kiswahili kinazungumzwa na mamilioni ya wakazi wa mataifa mbalimbali ya Afrika na mengine yaliyo nje ya Bara la Afrika (KIE, 2002: 23; Chimerah, 1998: 2 na Beja, 2001). Kwa hivyo, umuhimu wa kuchunguza na kusisitiza matumizi ya lugha zungumzi fasaha na sanifu hasa shuleni ambako Kiswahili kinafundishwa na kukuzwa ulikuwa dhahiri.

Ujifunzaji wa lugha, hasa zungumzi, hautendeki katika ombwe tupu. Wazungumzaji lazima wazungumzie mada au masuala mahsusi yanayomzunguka na kumwathiri binadamu kila

uchao - magonjwa hatari, ufisadi, imani, maadili na mengine mengi. Kwa hivyo kutalii ruwaza za matumizi ya lugha na athari zake kwa umilisi wa lugha zungumzi ya Kiswahili ni kutalii na kuieleza jamii kwa ujumla wake. Huu sio mchango tu kwa maendeleo ya Isimu, bali jamii pia.

Utafiti huu ni natija kwa walimu wa Kiswahili vilevile. Taasisi ya Elimu nchini Kenya (KIE, 2002) inasisitiza lengo la mwalimu wa Kiswahili kuwa 'Kumpa mwanafunzi nafasi ya kutagusana (kuingiliana) na wengine, mwalimu, waalikwa, matini na mazingira'. Matokeo ya utafiti huu ni dafina muhimu kwa mwalimu kama huyu kwani yamebainisha na kueleza ruwaza za matumizi ya lugha na kuonyesha athari zake kwa umilisi wa lugha zungumzi fasaha ya Kiswahili.

Isitoshe, watawala wa shule watanufaika kutokana na mapendekezo yaliyotolewa kuhusu utekelezaji wa sera ya lugha shuleni. Mapendekezo haya mbali na kuchochea utafiti zaidi, yatapelekea kukuza matumizi ya Kiswahili fasaha shuleni na kuboresha matokeo katika mitihani ya kitaifa.

Wakuza mitalaa, hususan ya Kiswahili watanufaika kutokana na uchunguzi huu. Jopo la Kiswahili katika Taasisi ya Elimu (KIE) limeainisha madhumuni ya kufundisha Kiswahili katika shule za upili kuwa ni:

> Kumpa (mwanafunzi) uwezo wa kudumu wa kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika ipasavyo kwa lugha ya Kiswahili;
> Kutumia Kiswahili katika mawasiliano na shughuli za kila siku;
> Kuthamini kufurahia na kujivunia Kiswahili kama lugha ya taifa na kimataifa;
> Miongoni mwa mengine mengi. (KIE, 2002: 25).

Kwa kiwango kikubwa matokeo ya utafiti huu ni msaada kwa wanajopo wa Kiswahili kutathmini utekelezaji na kuafikiwa kwa madhumuni haya. Isitoshe, huu utakuwa mchango katika kupendekeza nyenzo mwafaka za kuyaafikia malengo haya.Aidha, umetoa mchango katika kupendekeza nyenzo mwafaka za kuyaafikia malengo haya.

Sera ya lugha kuhusu Kiswahili imekuwa ikitetereka kabla na hata baada ya uhuru nchini Kenya. Huku kuyumbayumba kwa sera kumeathiri vibaya ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili katika viwango mbalimbali vya elimu (Whiteley, 1974; Kimemia, 2001 na Mukuria, 1995). Hali hii imezorotesha maendeleo ya Kiswahili katika matumizi mapana. Hata hivyo, tatizo kubwa sio kuzinduliwa kwa sera mwafaka bali ni utekelezaji wa sera hizo zilizopo. Kwa hivyo, ni kutokana na msingi huu ambapo umuhimu wa kuchunguza masuala yanayohusiana na ruwaza za matumizi ya lugha na athari zake kwa umilisi wa lugha zungumzi ya Kiswahili yalipewa kipaumbele kama sehemu ya kueleza utekelezaji wa sera ya lugha kuhusu Kiswahili.

1.7 Upeo wa Utafiti

Utafiti huu unahusu ruwaza za matumizi ya lugha na athari zake kwa umilisi wa lugha zungumzi ya Kiswahili miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili wilayani Siaya. Ingawa kuna uwezekano wa kuwepo athari zingine tofauti zinazotokana na ruwaza za matumizi ya lugha kwa Kiswahili, utafiti huu ulijikita katika eneo la Isimu ambapo ulishughulikia matamshi fasaha.

Kaniu, G.M. (2003) ameonyesha ruwaza za matumizi ya lugha miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili katika taarafa ya Kandara Wilayani Maragwa. Aidha, amebainisha jinsi ruwaza hizo zinavyoathiri umilisi wa mawasiliano zungumzi katika lugha ya Kiingereza. Ijapokuwa utafiti huu ulinufaika pakubwa kutokana na njia za utafiti alizotumia Kaniu, uchunguzi huu ulikuwa tofauti kwa ambavyo ulibainisha jinsi ruwaza za matumizi ya lugha zinavyoathiri umilisi wa lugha zungumzi ya Kiswahili miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili wilayani Siaya. Isitoshe, baadhi ya shule zilizohusishwa, hususan za bweni; zina wanafunzi wanaotumia lugha za kwanza tofauti kinyume na sampuli aliyoitumia Kaniu ambayo ilijumuisha wanafunzi wanaotumia lugha ya kwanza moja.

Uchunguzi wenyewe ulifanywa nyanjani, yaani shuleni. Jumla ya shule tano za upili wilayani Siaya zilichaguliwa kwa uteuzi wa sampuli mtabakisho. Wanafunzi ishirini wa kidato cha tatu kutoka kila shule walishirikishwa katika zoezi hili. Wanafunzi wa kidato cha tatu walitumiwa kwa sababu wana ujuzi wa Kiswahili unaozidi miaka kumi, wana uzoefu katika mazingira ya shule ya upili, ni wakomavu kiakili na hawaogopi wenzao, walimu wala wageni shuleni. Aidha, walimu wawili wa lugha ya Kiswahili walihojiwa na kujaza hojaji. Kwa jumla, wanafunzi mia moja na walimu kumi walishirikishwa katika utafiti huu.

1.8 Hitimisho

Katika.sura ya kwanza tumejadili mada muhimu katika utangulizi wa utafiti. Tumeeleza usuli wa mada na hivyo kuuwekea msingi utafiti wetu. Tumeeleza pia mada ya utafiti, madhumuni ya utafiti, nadharia tete za utafiti, umuhimu wa utafiti na upeo wa utafiti. Katika sura ya pili tumehakiki kazi zilizoandikwa kuhusu mada ya utafiti ili kuuweka uchunguzi wetu katika mkabala wa tafiti zilizopo na kueleza misingi ya nadharia iliyoongoza uchunguzi huu.

1.9 Maelezo ya Istilahi

Ruwaza za Matumizi ya Lugha	Uteuzi na matumizi ya lugha mbalimbali azijuazo mzungumzaji.
Mwongozo wa Uchunguzi	Tafsiri yetu ya 'Observation Schedule'.
Uteuzi wa Sampuli Mtabakisho	Tafsiri yetu ya 'Stratified Random Sampling.'
Lugha Zungumzi	Ni kutamka, kunena au kusema kwa njia ya mdomo, hasa katika maongezi yanayoakisi hali halisi. Tafsiri yetu ya 'Spoken language'.
Lugha Fasaha	Ni lugha yenye usafi wa maneno; yenye kutoa, kutamka au

	kupa kila neno au maneno maana yake sahihi. Ni lugha yenye matamshi sahihi.
Lugha Sanifu	Ni lugha yenye kufuata taratibu au kanuni za kisarufi zilizokubaliwa.
Lugha ya Kikabila	Ni lugha inayozungumzwa kiasili na kikundi cha watu katika taifa wanaohusiana kwa mila, desturi na utamaduni.
Sheng	Ni lugha yenye sarufi geugeu inayosikika na kutamkika kama Kiswahili (Ngesa, 2002) lakini iliyo na msamiati wa kipekee usio thabiti. Ni lugha maarufu miongoni mwa vijana wengi mijini na wachache mashambani nchini Kenya (Ongechi, 2002: 4).
Wingilugha	Hali ya mtu mmoja kuwa na uwezo wa kusema na kuelewa lugha kadhaa kando na lugha yake ya uzawa.
Ghala la lugha	Hazina ya lugha azijuazo mtu na ambazo hutawala matumizi yake ya lugha.
Lugha Sambazi	Pia huitwa *lingua franca.* Hii ni lugha inayotumiwa miongoni mwa watu ambao huzungumza lugha tofauti kabisa. Ni lugha iliyoenea kijiografia hadi ikaanza kuzungumzwa na watu wengi.
Kuhamisha/Kubadilisha msimbo	Ni ile hali ambapo msemaji aliye na umilisi wa zaidi ya lugha moja huweza kugeuza mazungumzo yake kutoka lugha moja hadi nyingine kutegemea hali iliyopo katika mazingira fulani, mada au mtindo.

Kuchanganya msimbo Ni ile hali ya msemaji kutumia vipashio au maneno ya lugha mbalimbali katika hali moja ya mazungumzo.

Sera ya lugha Ni kaida au maamuzi yanayohusu uchaguzi wa lugha za kutumiwa shuleni. Maamuzi haya hutolewa na walimu.

Umilisi wa lugha Ni ile hali ya msemaji kutumia vipashio au maneno ya lugha kwa ufasaha. Tumeitumia dhana hii kurejelea ya Kiingereza 'Language Competence'.

SURA YA PILI

YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA YA UTAFITI

2.1 Utangulizi

Katika sura ya kwanza, tulitanguliza uchunguzi wetu kwa kubainisha usuli wa mada, mada yenyewe, madhumuni, nadharia tete, umuhimu na upeo wa utafiti. Sura ya pili, kwa upande wake, imetumiwa kujadili yaliyoandikwa kuhusu mada ya utafiti na misingi ya nadharia. Mbali na kuhakiki yaliyoandikwa kuhusu mada ya utafiti, lengo la sehemu hii ni kuuweka uchunguzi huu katika mkabala wa tafiti zilizopo na kuonyesha pengo lililokuwepo na ambalo utafiti wetu umeliziba. Uhakiki wa maandiko wenyewe ulifanywa kwa kuzingatia mada zifuatazo:-

(a) Ruwaza za matumizi ya lugha nchini Kenya.

(b) Ujifunzaji wa lugha ya pili.

(c) Tafiti kuhusu lugha zungumzi.

(d) Matamshi katika Kiswahili

2.2 Ruwaza za Matumizi ya Lugha Nchini Kenya

Wakenya wengi, wakiwemo wanafunzi, hutumia lugha tatu - lugha ya kwanza, Kiswahili na Kiingereza. Katika hali fulani lugha hizi huchangiana na kukamilishana kimajukumu (Gorman, 1974; Chimerah, 2000; Beja, 2001). Kiingereza ni lugha rasmi na ya kufundishia shuleni na Vyuoni. Kiswahili kimekuwa lugha ya taifa nchini tangu Disemba 31, 1971 (Hopkins, 1977). Hali hii, hata hivyo, imeanza kubadilika kutokana na maendeleo na matumizi ya lugha kama Sheng miongoni mwa vijana. Utafiti huu ulijikita katika ruwaza za matumizi ya lugha zinazoibuka katika mazingira ya wingilugha kama haya. Ulibainisha ruwaza za matumizi ya

lugha miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili na athari zake kwa umilisi wa lugha zungumzi ya Kiswahili.

Katika uchunguzi wake kuhusu uteuzi na matumizi ya lugha nchini Kenya, Marylyn (1978) ameonyesha kuwa wanafunzi hufanya uteuzi wa mara kwa mara kati ya lugha mbili au tatu. Alihitimisha kwa kusema kwamba kufanana au kutofautiana kwa lugha za `kwanza miongoni mwa wanafunzi hutekeleza jukumu muhimu katika uteuzi wa misimbo mwafaka ya mawasiliano. Kwa jumla, uchunguzi wa Marylyn ulihusu ruwaza za matumizi ya lugha zinazoibuka katika shughuli za kimtagusano kati ya wanafunzi. Utafiti huu ulitumia mbinu kama za Marylyn na kujengea hapo kwa kubainisha athari za ruwaza hizi kwa umilisi wa lugha zungumzi ya Kiswahili kwa kuzingatia matamshi ya wazungumzaji.

Kimemia (2001) anapendekeza ukuzaji na upanuzi wa Kiswahili katika mfumo wa Elimu nchini Kenya. Anashikilia kwamba uteuzi na matumizi ya lugha yoyote hutegemea sababu zilizo nje ya sera za lugha za shule. Kwake, uteuzi wa lugha hutegemea uelewano, mshikamano wa kijamii, urasmi au urafiki na natija itakayopatikana kwa kuchagua na kutumia lugha moja dhidi ya nyingine. Licha ya kwamba ni vigumu kubashiri ni lugha ipi au ni aina ipi ya lugha itakayotumiwa na wazungumzaji, mawazo ya Kimemia yalikuwa muhimu katika kubainisha kwetu ruwaza za matumizi ya lugha miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili kama jumuiya lugha mahsusi.

Kwa mujibu wa Kimemia (mtaje) lugha kuu za mawasiliano katika shule za upili ni Kiingereza na Kiswahili ambazo ni masomo ya lazima yanayotahiniwa na lugha sambazi. Uteuzi na matumizi ya Kiswahili au Kiingereza nje ya darasa hutegemea, kwa kiasi kikubwa, utekelezaji na utendakazi wa sera ya lugha au kanuni za shule kuhusu lugha zinapopatikana. Kwa jumla, Kiingereza hutumika zaidi katika miktadha ya darasani - masomo yote isipokuwa ya lugha hufundishwa kwa Kiingereza. Hata hivyo, katika miktadha isiyokuwa rasmi nje ya darasa,

matumizi ya Kiingereza na Kiswahili hubadilishana nafasi. Matumizi ya Lugha za Kikabila na Sheng yamepigwa marufuku kwingi. Uchunguzi wetu, mbali na kuthibitisha ruwaza hizi mahsusi za matumizi ya lugha zungumzi nje ya darasa, ulionyesha pia athari zitokanazo na ruwaza hizi kwa matamshi sahihi ya Kiswahili sanifu.

Akiandika kuhusu matumizi ya lugha nchini Kenya, Whiteley (1974) anasema kuwa wazungumzaji, wakiongozwa na tajiriba au uzoefu, huchagua lugha mwafaka watakayoitumia bila mushkeli wala kutatiza mazungumzo katika miktadha au hali fulani. Maoni ya Whiteley yalitusaidia katika kubainisha aina ya uteuzi na matumizi ya lugha miongoni mwa washiriki. Utafiti huu, hata hivyo, ulijifunga katika kuwachunguza wanafunzi wa shule za upili.

Kuhusu mabadiliko na udhibiti wa lugha miongoni mwa jamii zilizohamia Marekani, Fishman (1966) anaonelea kwamba vijana wanaobaleghe huathiriwa pakubwa na utamaduni pendwa na lugha ya vyombo vya habari kama magazeti, filamu, magazini za picha na nyimbo pendwa. Kimsingi, ujumbe wa vyombo hivi huwasilishwa kwa Kiingereza. Kama ilivyo Marekani, mawazo ya Fishman yana mashiko nchini Kenya. Utafiti huu ulihusu matumizi ya lugha ya vijana wanaobaleghe. Mawazo ya Fishman yalitusaidia kuchunguza athari za vyombo vya habari na lugha yake, kwa ruwaza za matumizi ya lugha na umilisi wa lugha zungumzi fasaha ya Kiswahili miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili.

2.3 Ujifunzaji wa Lugha ya Pili

Ufasaha wa lugha ya pili unahusu kuwa na umahiri kimazungumzo (Chomsky, 1957) na Umahiri kimawasiliano (Hymes, 1971) ambao ni ujuzi wa matumizi ya lugha katika miktadha mbalimbali. Hili lina maana kwamba usemi au mazungumzo ni muhimu sana katika ujifunzaji wa kaida zinazoongoza matumizi na sarufi ya lugha. Kwa hivyo, utafiti huu ulichunguza ruwaza za matumizi haya ya lugha kama njia moja ya kueleza umilisi wa lugha ya pili. Aidha,

ulionyesha jinsi matumizi haya ya lugha yanavyoathiri umilisi wa lugha zungumzi fasaha ya Kiswahili hasa matamshi yake.

Saussure (1916) alitofautisha mfumolugha na utendaji. Alieleza mfumolugha kuwa mfumo dhahania wa lugha fulani ambao hutumiwa na jamii fulani. Mfumo huo hurithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine na hujengwa na vipashio mbalimbali ambavyo huhusiana kiuteuzi na kiusilisila. Kwa upande mwingine alieleza utendaji kuwa ule usemaji wenyewe wa lugha ambao hufanywa na kila mtu. Mtu binafsi aghalabu atazingatia mfumolugha ili aweze kuzungumza kwa usahihi kadiri anavyoweza. Hata hivyo, utendaji huwa si sahihi kutokana na udhaifu wa maumbile ya binadamu. Anatamatisha kwa kusema kuwa utendaji wowote si kiwakilisho sahihi cha mfumolugha alionao mzungumzaji. Maoni ya Saussure yamekita mizizi katika matumizi ya lugha ya wazawa asilia wa lugha. Hata hivyo, mawazo haya yalitusaidia kueleza utendaji wa lugha mbalimbali wa wanafunzi na athari zake kwa umilisi wa lugha zungumzi fasaha ya Kiswahili. Isitoshe, mawazo ya Saussure yalitunufaisha katika kueleza 'usafi' au ufasaha wa matamshi ya lugha zungumzi ya Kiswahili kama mfumolugha.

Seliger (1971) anashikilia kuwa lazima umahiri katika lugha ya pili uonekane katika mazungumzo na shughuli za kimtagusano. Analinganisha umilisi katika lugha ya pili na utendaji, yaani lugha zungumzi. Seliger anawaeleza wanafunzi wanaoingiliana kimazungumzo katika lugha ya pili kuwa 'wazalishi wakuu' kwani wanahimiza maendeleo ya lugha husika miongoni mwa wale walio karibu nao. Kiswahili ni lugha ya taifa la Kenya na ni somo la lazima linalofundishwa katika shule za msingi na upili. Kwa hivyo, shule hazina budi kutoa fursa na mazingira mwafaka kwa mazoezi na matumizi ya lugha zungumzi ya Kiswahili. Utafiti huu umependekeza njia mwafaka za kuchochea na kuhimiza matumizi ya Kiswahili fasaha. Isitoshe, matokeo ya utafiti huu ni mchango katika kuyafanya mazingira ya shule kuwa mwafaka kwa uzungumzaji wa Kiswahili fasaha.

Kimemia (2001) analalamikia hali ya ufundishaji wa Kiswahili nchini Kenya. Anasema kwamba katika kiwango cha shule za upili, mbinu ya kufundisha ya 'kusoma - kuandika' haitoi fursa ya kutosha kwa wanafunzi kujifanyiza mazoezi ya mazungumzo kuhusu dhana zilizofundishwa. Hali hii ina maana kuwa wanafunzi wengi wa shule za upili humaliza masomo yao wakiwa na lugha zungumzi finyu ya Kiswahili - lugha iliyojaa utata, makosa ya uteuzi wa msamiati, matamshi na hata makosa ya kisarufi. Hali hizi zinakwamiza umilisi wa lugha zungumzi fasaha ya Kiswahili na ndiposa utafiti huu ulilenga kuliangazia suala hili.

Akiandika kuhusu umuhimu wa lugha zungumzi, Byne (1976) anapendekeza wanafunzi katika viwango vyote kuanzia cha chini hadi cha juu zaidi wahimizwe kutafuta na kutumia wakati wao mwingi kwa matumizi ya lugha waliyojifunza ili kukuza umahiri wao katika uzungumzi.

Naye Brumfit (1976) akimuunga mkono Byne anashikilia kuwa dhamira kuu ya kufundisha lugha ya pili ni kuendeleza umilisi wa lugha zungumzi, yaani, uwezo na ujasiri wa kutumia lugha. Wanayoyazungumzia Byne na Brumfit yatawezekana tu pale ambapo wanafunzi watahimizwa kujihusisha katika shughuli mbalimbali za kimtagusano katika lugha zungumzi fasaha ya Kiswahili. Matokeo ya utafiti huu yanatoa mchango katika kutekeleza jukumu hili.

Tafiti nyingi kuhusu ujifunzaji wa lugha ya pili, kama vile wa Dahl na Johnson (1978), zimeonyesha kwamba kuna uhusiano mkubwa kati ya lugha zungumzi fasaha na uwezo wa kusoma na kuandika. Wameonyesha kwamba wazungumzaji mahiri wa lugha ya pili husoma na kuandika vizuri katika lugha hiyo. Ni dhahiri kuwa matokeo ya tafiti hizi yalikuwa muhimu kwa uchunguzi huu kwa sababu uzungumzi wa Kiswahili fasaha utainua kiwango cha uandishi kwa jumla na hasa insha na hivyo kuboresha matokeo ya mitihani ya kitaifa na matumizi ya Kiswahili fasaha hasa kimatamshi nchini.

2.4 Tafiti Kuhusu Lugha Zungumzi

Mfumo wa Elimu wowote unahitaji kufanyiwa utafiti mara kwa mara kuhusu mbinu, yaliyomo na madhumuni. Iwapo mfumo huo unashughulikia zaidi ya lugha moja ni muhimu lugha zote zifanyiwe utafiti. Kutafiti lugha moja, kama inavyofanyiwa lugha ya Kiingereza, ni kukosa mwelekeo. Katika utafiti wa awali maktabani, hatukuweza kupata utafiti wowote uliofanywa kubainisha ruwaza za matumizi ya lugha na athari zake kwa umilisi wa lugha zungumzi ya Kiswahili. Utafiti mwingi tulioupata unahusu au unashughulikia lugha zungumzi ya Kiingereza. Ni dhahiri kwamba kazi zilizofanywa kwa au kuhusu lugha zungumzi ya Kiswahili na lugha zingine za kiafrika ni ndogo. Hali hii inachangia, mielelekeo hasi kuhusu lugha hizi (Whiteley, 1974). Utafiti huu ulijaribu kuliziba pengo hili.

Atsenga (2002) alichunguza tatizo la ukosefu wa umilisi wa lugha zungumzi fasaha ya Kiingereza miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili Wilayani Vihiga na Kakamega. Matokeo yake yalidhihirisha kuwa walimu wa Kiingereza hawakushughulikia ufundishaji wa mazungumzo vilivyo kama ulivyoratibiwa katika mtalaa. Mbali na kwamba uchunguzi wa Atsenga ulijikita darasani, ni dhahiri kwamba unahusu mbinu za kufundishia lugha zungumzi vile vile. Uchunguzi wetu, hata hivyo, ulihusu lugha zungumzi ya Kiswahili. Uchunguzi wa Atsenga unahusu Kiingereza ambayo ni moja kati ya lugha zinazofundishwa na kutumiwa na wanafunzi wa shule za upili. Kwa hivyo, utafiti huu ulibainisha athari za matumizi ya Kiingereza na lugha zingine kwa umilisi wa lugha zungumzi fasaha ya Kiswahili.

Kwa mujibu wa Crystal (1987) wanafunzi hupata fursa ndogo mno kujihusisha katika mazungumzo darasani. Alipendekeza ujifunzaji wa Lugha katika vitendo visivyoongozwa na mwalimu katika mazingira ya shule. Maoni ya Crystal yalikuwa muhimu kwetu kwa sababu tulichunguza tu zile ruwaza za matumizi ya lugha zinazodhihirika nje ya darasa na ambazo haziongozwi moja kwa moja na mwalimu.

Kaniu (2003) alichunguza ruwaza za matumizi ya lugha na athari zake kwa ujifunzaji wa mawasiliano zungumzi katika Kiingereza miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili katika taarafa ya Kandara Wilayani Maragwa. Matokeo yake yalionyesha kuwa matumizi ya lugha ya kwanza yalikuwa maarufu katika mawasiliano katika shule zilizotumia lugha ya kwanza moja. Hali hii ilipunguza fursa ya matumizi ya Kiingereza fasaha katika mawasiliano na hivyo kuathiri vibaya matumizi ya Kiingereza fasaha. Kaniu alihitimisha kuwa ipo haja ya kubadilisha ruwaza za matumizi ya lugha zilizopo ili kukuza ufasaha wa kuzungumza Kiingereza.

Uchunguzi huu ulinufaika pakubwa kutokana na nadharia na mbinu alizotumia Kaniu (2003). Hili tulilifanya ili kudhibitisha ufaafu wa nadharia na vifaa alivyotumia Kaniu. Hata hivyo, kuna tofauti kubwa kati ya tafiti hizi. Kwanza, utafiti wa Kaniu umeegemea kwa matumizi ya lugha ya Kiingereza katika taarafa ya Kandara Wilayani Maragwa. Utafiti huu ulifanywa Wilayani Siaya na unahusu lugha zungumzi ya Kiswahili. Pili, sampuli ya Kaniu ilikuwa ndogo na inayotumia lugha ya kwanza moja ya kibantu. Sampuli ya utafiti huu ilikuwa kubwa na ilishirikisha baadhi ya watafitiwa waliotumia lugha za kwanza tofauti.

Kuna sababu anuai zinazomfanya mtu au kundi la watu kuchagua, kuchanganya au kuhamisha misimbo au lugha. Dorian (1981) alitambua umri na utambulisho wa wazungumzaji kuwa sababu dhahiri zinazoongoza uteuzi wa lugha. Sababu hizi, hata hivyo, zinahusu watu binafsi wala sio jumuiya lugha.

Fishman (1965) kwa upande wake anatoa sababu zinazoongoza uteuzi na uhamishaji wa lugha. Anaziainisha kuwa: kwanza, mandhari, wakati, mahali na muktadha. Pili ni washiriki ambao huchunguzwa kwa misingi ya umri, uana na hali yao ya kiuchumi. Sababu ya tatu ni mada ya mazungumzo na ya nne ni uamilifu wa shughuli ya mtagusano husika. Sababu wanazotoa Dorian (1981) na Fishman (1965) zimeegemea sana upande wa uhamishaji lugha unaomhusu mtu binafsi wala sio jumuiya lugha. Uchanganuzi wa lugha kama huu, ulikuwa

muhimu kwa utafiti wetu ambao ulilenga kubainisha motisha unaoelekeza uteuzi na matumizi ya lugha miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili.

Gorman (1971) alichunguza vipengele vya matumizi ya lugha na umilisi wa wanafunzi waliojiunga na shule za upili nchini Kenya mwaka wa 1968. Alijihusisha na ujuzi na matumizi ya Kiingereza, Kiswahili na lugha ya kwanza katika hali mahsusi za kimtagusano na usikilizaji. Uchunguzi wa Gorman ulibainisha mikondo na ruwaza za matumizi ya lugha miongoni mwa wanafunzi wanaojiunga na shule za upili. Mbali na kujengea alipoachia Gorman, utafiti huu ulinufaika kutokana na mbinu na vifaa alivyotumia kama vile hojaji na mahojiano. Hata hivyo, kuna kipindi kirefu cha wakati kati ya utafiti wa Gorman (1971) na wetu - jambo ambalo lilizua tofauti. Isitoshe, utafiti huu ulitumia sampuli ya wanafunzi wa kidato cha tatu ambao wanaelekea kumaliza masomo ya shule ya upili. Ruwaza zao za matumizi ya lugha zilibainishwa na kuonyesha athari zake kwa umilisi wa matamshi fasaha ya Kiswahili.

Simon (1980) amejishughulisha na ufundishaji na matumizi mabaya ya Kiingereza nchini Marekani katika miaka hamsini iliyopita. Tatizo aliloshughulikia ni utata wa mawasiliano unaosabishwa na ufundishaji na matumizi mabaya. Katika muktadha wa Marekani, lugha inayolengwa ni Kiingereza sanifu. Hata hivyo, mbali na Kiingereza sanifu lahaja zingine zisizo sanifu zinang'ang'ania usawa wa matumizi. Kimsingi, katika muktadha wa Marekani, tatizo hili linahusu lugha moja na athari za lahaja zake kwa ile sanifu. Hali hii ni kinyume cha hali nchini Kenya ambamo muna zaidi ya matumizi ya lugha tatu. Utafiti huu ulieleza ruwaza za matumizi ya lugha hizi na kuonyesha athari zake kwa umilisi wa lugha zungumzi fasaha ya Kiswahili.

2.5. Matamshi Katika Kiswahili

Matamshi ni tatizo kubwa sio tu kwa Wakenya wengi, bali pia kwa wanafunzi katika shule za upili (Mbaabu, 1985; 1995; Mangwa, 2004). Makosa yanayohusu sauti yanasababishwa

na sababu kadhaa kama vile: maingiliano yanayotokana na ujuzi wa Lugha ya Kwanza (L1), unyonge wa kutojitahidi katika kuyatamka maneno ambao hujitokeza katika maandishi; athari za lugha nyingine na vilugha vinavyozuka kama Sheng; athari za mazingira mtoto anamokulia; na upungufu wa msamiati na mazoezi ya matumizi ya lugha husika. Utafiti huu ulijishughulisha na sababu ya mwisho- mazoezi ya matumizi ya lugha. Kwa kurejelea ruwaza za matumizi ya lugha miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili wilayani Siaya, tumeonyesha athari za ruwaza hizi kwa umilisi wa matamshi fasaha.

Utafiti wa Mangwa (2004) ulibainisha kwamba wanafunzi waliohusishwa katika mijadala walikuwa na matatizo mengi katika matamshi (66.9%) yakifuatiwa na yale ya kisarufi (25.8%) na hatimaye ya msamiati (7.3%). Mangwa alipendekeza wanafunzi wapewe mazoezi mengi katika mazungumzo na uandishi wa insha. Alitoa wito kwa wanafunzi waepuke kutumia lugha yao ya kwanza (Ekegusii) katika mawasiliano yao mengi kama wakati wa michezo, mapumziko na shughuli nyinginezo. Kwake, matumizi ya Kiingereza katika masomo mengi na shughuli nyinginezo yalionekana kuchangia kutozingatiwa kwa Kiswahili. Utafiti wa Mangwa ulijikita zaidi katika makosa bila kuupa nafasi usahihi na matumizi fasaha ya Kiswahili. Makosa ni moja tu kati ya athari zingine nyingi za matumizi ya lugha. Hata hivyo, mapendekezo yake ni muhimu na yaliuchochea na kuupa mwelekeo uchunguzi wetu wa ruwaza za matumizi ya lugha na athari zake kwa umilisi wa lugha zungumzi ya Kiswahili.

King'ei na Musau (2002) katika utafiti wao wameonyesha matatizo ya kimatamshi waliyo nayo wakenya wengi, ingawa sio wote, wanaojifunza au kuzungumza Kiswahili kama lugha ya pili. Walizingatia jinsi lugha kadha za kikabila zilivyotofautiana na Kiswahili. Pia walizingatia matatizo ya kimatamshi yanayoweza kutokana na tofauti hizo. Ni dhahiri kwamba uchunguzi wao ulijifunga katika kubainisha aina za matatizo ya kimatamshi kwa kulinganisha lugha za kikabila na Kiswahili, yaani lugha mbili. Utafiti wetu, hata hivyo, ulijengea hapa kwa

kuzingatia matumizi ya lugha zote ambazo ni sehemu ya 'ghala la lugha' za wanafunzi. Ulibainisha athari - ambazo makosa ni moja kati yazo - za ruwaza za matumizi ya lugha zungumzi kwa matamshi fasaha ya Kiswahili miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili wilayani Siaya.

2.6 Misingi ya Nadharia

Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Usemi ya Matumizi na Ujifunzaji wa lugha ya pili iliyoasisiwa na Hatch (1978). Hii ni nadharia ya matumizi ya lugha inayochukulia mawasiliano au matumizi ya lugha kuwa dhihirisho la ujuzi wa lugha husika. Hatch anapendekeza kuwa ujifunzaji wa lugha uelezwe kwa misingi ya namna ambavyo mwanafunzi anavumbua maana mbalimbali zinazoweza kupatikana katika lugha kwa kushiriki katika mawasiliano.

Hatch (1978) anasisitiza kwamba vijenzi vya lugha - kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika - hukuzwa kutokana na matumizi yake katika shughuli mbalimbali za kimtagusano. Anasema kuwa muundo wenyewe wa lugha ni kivuli cha jukumu linalotekelezwa na lugha hiyo. Kwa hivyo, kujifunza kuwasiliana au kuzungumza ni kujifunza lugha husika pia. Kupitia kwa mawasiliano au mazungumzo na watu wengine ulimwenguni, mwanafunzi hukuza kaida za muundo na matumizi ya lugha husika.

Kwa mujibu wa nadharia hii, mwanafunzi hujifunza lugha anapojihusisha katika shughuli za kimtagusano kama vile mazungumzo. Mazungumzo katika Kiswahili hayana budi kukuzwa shuleni kwa vyovyote vile kwani huku ndiko kuliko miktadha muhimu ya ujifunzaji wa lugha.

Kwa kusisitiza umuhimu wa mwanafunzi kujihusisha katika mazungumzo nje na darasani kwa kutumia Kiswahili, nadharia hii ilitusaidia kufanikisha uchunguzi huu. Imedhihirika wazi kwamba ni kupitia kwa matumizi ya Lugha kama haya, ambapo mwanafunzi ataweza kuthibiti ujuzi wake wa lugha na kuitumia kwa ufasaha katika mawasiliano.

Mihimili mikuu ya nadharia hii ni kuwa:

a) Inachukulia mawasiliano au matumizi ya lugha katika mandhari na miktadha halisi kuwa dhihirisho la ujuzi wa lugha husika.

b) Inasisitiza kuwa matumizi ya lugha ni dhihirisho la umilisi wa lugha hiyo alionao mtumiaji wa lugha husika.

Nadharia hii ilitusaidia kuyaafikia malengo yetu. Hili lilitokana na kusisitiza kwake kwa umuhimu wa wanafunzi kutumia lugha wanayojifunza katika mandhari na miktadha halisi ili waweze kukuza ufasaha na umilisi wao katika mazungumzo. Nadharia hii ilituelekeza kubainisha na kueleza ruwaza mahususi za matumizi ya lugha zungumzi miongoni wanafunzi wa shule za upili wilayani Siaya. Aidha, ilitufaidi pakubwa katika kubainisha nafasi ya Kiswahili fasaha katika mawasiliano ya wanafunzi hawa. Isitoshe, kutokana na kusisitiza kwake kuwa matumizi ni dhihirisho la umilisi wa lugha, nadharia hii ilitusaidia kubainisha athari za matumizi ya lugha zungumzi kwa matamshi fasaha ya Kiswahili miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili wilayani Siaya. Uchunguzi huu vile vile ulitumia mtazamo wa kiisimujamii wa Fishman (1972 a), Hudson (1980) na Fasold (1984).

Kwa hivyo, ni kutokana na msingi huu wa nadharia ambapo utafiti huu ulichunguza ruwaza za matumizi ya lugha miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili. Aidha, athari za ruwaza hizi kwa matamshi fasaha ya Kiswahili zilibainishwa na mapendekezo mwafaka kutolewa.

EGERTON UNIVERSITY LIBRARY

2.7 Hitimisho

Sura ya pili imetumiwa kuhakiki na kujadili utafiti ambao umefanywa kuhusiana na mada ya utafiti. Uhakiki umefanywa kuhusu ruwaza za matumizi ya lugha nchini Kenya na ujifunzaji wa lugha ya pili. Tafiti za awali kuhusu lugha zungumzi zimechambuliwa na kuonyesha uhitaji

wa kubainisha athari za matumizi ya lugha mbalimbali kwa umilisi wa lugha zungumzi fasaha ya Kiswahili. Vile vile, kazi kuhusu matamshi katika Kiswahili zimehakikiwa. Hatimaye, tumeeleza misingi ya nadharia iliyotawala uchunguzi mzima. Katika sura ya tatu tumejadili mbinu za utafiti.

SURA YA TATU

MBINU ZA UTAFITI

3.1 Utangulizi

Katika sura ya pili tulihakiki na kujadili kazi na tafiti ambazo zimefanywa kuhusiana na mada ya utafiti na kubainisha pengo ambalo utafiti huu umeziba. Sura hii imetumiwa kueleza mbinu za utafiti. Ili kufanikisha maelezo haya, sura yenyewe imegawanywa katika sehemu hizi: njia za utafiti, jumuiya, uteuzi wa sampuli, ukusanyaji wa deta na hatimaye jinsi uchanganuzi wa deta ulivyofanywa.

3.2 Njia za Utafiti

Utafiti huu ulifanywa nyanjani, yaani shuleni. Uchunguzi wenyewe ulinuiwa kubainisha habari mahsusi kuhusu ruwaza za matumizi ya lugha miongoni mwa wanafunzi katika shule za upili wilayani Siaya. Hili lilitokana na upekuzi wa maandishi ambao ulithibitisha kwamba ufasaha katika kuzungumza lugha ya pili ungeweza kufikiwa tu iwapo wanafunzi wangetumia muda wao mwingi kwa mawasiliano katika lugha husika. Kwa hivyo, utafiti wa nyanjani ulihitajika kuchunguza ruwaza mahsusi za matumizi ya lugha zungumzi na kisha kubainisha athari zake kwa matamshi fasaha ya Kiswahili.

3.3 Jumuiya

Utafiti huu ulichunguza ruwaza za matumizi ya lugha na athari zake kwa umilisi wa lugha zungumzi ya Kiswahili miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili wilayani Siaya. Wilaya hii ina jumla ya shule za upili sabini na moja. Kati ya shule hizi, 11 ni za Bweni za Wasichana, 8 za Bweni za Wavulana, 49 ni za Kutwa za Mseto na 3 ni za Mseto za Kutwa na Bweni (Tazama

Kiambatisho F). Mbali na kwamba kuna lugha zingine za kikabila (lugha za kwanza), Dholuo ndiyo lugha ya kwanza kwa wanafunzi wengi katika shule za upili nyingi pamoja na viunga vyazo wilayani Siaya.

3.4 Uteuzi wa Sampuli

Jumla ya shule tano za upili zilichaguliwa kwa uteuzi wa sampuli mtabakisho. Shule mbili za Mseto na za Kutwa katika kiwango cha Wilaya na mbili za Bweni katika kiwango cha Mkoa- moja ikiwa ya wavulana na nyingine ya wasichana. Nayo shule ya tano ilikuwa ya Mseto na iliyo na wanafunzi wa kutwa na wa bweni. Shule zilichaguliwa kwa kategoria hizi ili kuifanya sampuli iliyoteuliwa iwakilishe vizuri na kikamilifu jumuiya ya wanafunzi wa shule za upili wilayani Siaya.

Shule za Wilaya zilichaguliwa kwa sababu zinateka wanafunzi wake kutoka Wilaya husika - wanafunzi ambao aghalabu wanatumia lugha ya kwanza moja ambayo ni Dholuo. Shule za kiwango cha Mkoa, tofauti na za Wilaya, huchagua wanafunzi.wake kutoka Wilaya tofauti na wanafunzi hawa wanatumia lugha za kwanza tofauti. Aidha, wanafunzi katika shule za Bweni hutumia muda wao mwingi shuleni wakilinganishwa na wenzao wa shule za Kutwa wanaorudi nyumbani na kulazimika kutumia lugha ya kwanza. Hali hizi zilituwezesha kulinganisha ruwaza za matumizi ya lugha katika kategoria hizi na kubainisha athari zake kwa umilisi wa matamshi fasaha ya Kiswahili.

Wanafunzi ishirini wa kidato cha tatu kutoka kila shule waliteuliwa kishelabela na kushirikishwa. Wanafunzi wa kidato cha tatu walitumiwa kwa sababu walikuwa na ujuzi na umilisi wa Kiswahili unaozidi miaka kumi, uzoefu wao katika shule ya upili, ni wakomavu kiakili na hawaogopi wenzao, walimu wala wageni shuleni. Isitoshe, walichukuliwa kuwa na

uwezo wa kutumia Kiswahili na lugha zingine wazijuazo katika nyanja, hali na miktadha anuwai.

Walimu wawili wa lugha ya Kiswahili kutoka kila shule walihusishwa katika mahojiano na kujibu maswali ya hojaji. Majibu ya walimu yalitumiwa kubainisha umadhubuti wa majibu yaliyotolewa na wanafunzi na kuonyesha uhusiano uliokuwepo kati ya makundi haya mawili ya deta.

Jumla ya wanafunzi mia moja na walimu kumi walishiriki katika utafiti huu. Tulichagua kushirikisha watafitiwa wachache kwa sababu idadi ndogo ya watafitiwa katika utafiti wa kiisimujamii humwezesha mtafiti kupata deta ya kina (Milroy, 1987: 21). Akimnukuu Sankoff (1980), Milroy anashikilia kuwa mtafiti hana budi kuchagua idadi ndogo ya watafitiwa ambayo ataingiliana nayo ipasavyo. Jedwali 1 hapa chini linaoonyesha sampuli iliyoteuliwa.

Jedwali 1 Sampuli

SHULE	WANAFUNZI	WALIMU	AINA YA SHULE	JINA LA SHULE
A	20	02	Shule ya Kutwa ya Mseto	Nyagondo
B	20	02	Shule ya Kutwa ya Mseto	Agoro Oyombe
C	20	02	Shule ya Bweni ya Wasichana	Ng'iya
D	20	02	Shule ya Bweni ya Wavulana	Barding
E	20	02	Shule ya Mseto ya Kutwa & Bweni	Horace Ongili

3.5 Ukusanyaji wa Deta

Ukusanyaji wa deta katika uchunguzi huu ulifanikishwa kupitia kwa ;Hojaji, Mjarabu, Mahojiano, Mijadala na Uchunguzi shiriki. Vifaa hivi viliandaliwa na kufanyiwa majaribio katika uchunguzi awali uliofanywa katika shule moja kabla ya utafiti wenyewe. Kupitia kwa

uchunguzi awali, baadhi ya matatizo katika vifaa yalitambuliwa na kutatuliwa. Baadhi ya matatizo yaliyoibuka yalikuwa ugumu wa lugha, urefu wa Hojaji na mpangilio wa maswali katika Mjarabu, Mwongozo wa Maswali ya Mahojiano na Mwongozo wa Uchunguzi.

Ukusanyaji wa deta katika uchunguzi wenyewe, ulianza pindi baada ya mtafiti kupata kibali cha kufanya utafiti kutoka kwa Mkuu wa Elimu wilayani Siaya. Mtafiti alizuru shule zilizoteuliwa na kuomba ruhusa kufanya utafiti kutoka kwa walimu wakuu husika. Aidha, aliomba msaada wa walimu wawili wa Kiswahili katika zoezi zima ambalo lilichukua wiki moja katika kila shule.

Jumla ya wanafunzi mia moja wa kidato cha tatu, ishirini kutoka kila shule walipewa Mjarabu (Kimbatisho C) kutathini umilisi wao wa lugha ya Kiswahili kimatamshi. Isitoshe, walikamilisha Hojaji (Kiambatisho A) na kuandika habari kuhusu matumizi yao ya lugha mbalimbali katika mawanda, mahali na miktadha tofautitofauti.

Kwa ushirikiano na walimu wa Kiswahili, mijadala iliandaliwa katika kila shule. Kila mzungumzaji alipewa dakika tano kuchangia mjadala. Mazungumzo yao yalinaswa kwa kinasa sauti. Kutokana na mazungumzo haya, kuwepo makosa au usahihi wa matamshi miongoni mwa wanafunzi ishirini kuliorodheshwa. Kuwepo kwa makosa haya kulitumiwa kubainisha baadhi ya athari za ruwaza matumizi ya lugha kwa umilisi wa lugha zungumzi ya Kiswahili.

Walimu kumi - wawili kutoka kila shule - walijaza Hojaji (Kiambtisho B) na kutoa habari kuhusu utekelezaji wa sera ya lugha na jinsi ya kufanikisha ufasaha wa lugha zungumuzi ya Kiswahili miongoni mwa wanafunzi. Isitoishe, kutokana na mahojiano (Kiambatisho D), walimu walithibitisha na kutoa habari zaidi kuhusu ruwaza za matumizi ya lugha shuleni mwao.

Kumwezesha kuthibitisha na kufidia habari zilizotolewa kupitia kwa Hojaji na Mahojiano, mtafiti alichunguza matumizi ya lugha ya wanafunzi darasani, uwanjani, ukumbini, wakati wakipiga gumzo, wakati wa buraha na wakati wa maakuli. Hili lilifanywa kwa muda wa

wiki moja katika kila shule huku mtafiti akirekodi mambo muhimu kwa msaada wa Mwongozo wa Uchunguzi.

Hatimaye, deta hizi zote ziliainishwa katika majedwali na misambao ya umaratokezi. Deta hizi zote zilichanganuliwa kithamano na kiwingidadi ili kufasiri na kueleza matokeo ya utafiti.

3.6 Vifaa vya Ukusanyaji wa Deta

Kutuwezesha kufanikisha uchunguzi huu hojaji, mahojiano, Mjarabu, mijadala na uchunguzi shiriki ndivyo vifaa ambavyo vilitumiwa katika ukusanyaji wa deta.

3.6.1 Hojaji

Aina mbili za hojaji ziliandaliwa na kutumiwa kukusanya deta – Hojaji kwa Wanafunzi (Kiambatisho A) na Hojaji kwa Walimu wa lugha (Kiambatisho B). Hojaji zote mbili zilijumuisha maswali funge na wazi ili kumpa kila mtafitiwa uhuru wa kutoa habari zaidi na kamilifu kwa mujibu wa madhumuni ya utafiti.

Hojaji kwa wanafunzi ililenga kupata habari kuhusu matumizi ya lugha katika hali na nyanja halisi za kimtagusano na usikilizaji. Maswali yenyewe yalinuiwa kuzua habari zifuatazo kutoka kwa kila mwanafunzi:

a) Lugha anazozijua na kuzungumza mwanafunzi katika mawanda na miktadha mbalimbali.
b) Kugeza uzungumzi wa baba na mama katika Kiswahili, Kiingereza na Sheng kwa kutumia kipimo cha viwango vinne – 'Vizuri Sana,' 'Vizuri,' 'Sio Vizuri Sana' na 'Hajui Hata Kidogo.'
c) Vikwazo kuhusu matumizi ya lugha fulani nyumbani.
d) Matumizi ya lugha katika miktadha mbalimbali shuleni.

e) Matumizi ya lugha mbalimbali katika kujadili mada tofautitofauti kama vile Hisbati, Fasihi katika Kiingereza, Fasihi katika Kiswahili na Sherehe ya kitamaduni.

f) Lugha wazitumiazo wanafunzi katika usikilizaji wa vipindi vya redio na usomaji wa magazeti na majarida.

g) Sera ya lugha shuleni: kuwepo na utekelezaji wake.

h) Habari nyingine muhimu kuhusu matumizi ya lugha ya wanafunzi kama vile aina ya shule na jinsia ya mwanafunzi.

Hojaji kwa walimu kwa upande mwingine ilinuiwa kudhibitisha habari zilizotolewa na wanafunzi kuhusu ruwaza za matumizi ya lugha huku ikitoa habari zaidi kuhusu:

a) Idadi ya lugha wanazozungumza walimu na wanafunzi .

b) Lengo, utekelezaji na matatizo yanayokumba ufanisi wa sera ya lugha shuleni.

c) Kiwango cha umilisi wa wanafunzi wao katika kutumia lugha zungumzi ya Kiswahili.

d) Uhamasishaji wa wanafunzi kuhusu umuhimu, manufaa na nafasi ya Kiswahili katika ulimwengu wa kisasa na wa siku za usoni.

e) Uhusishaji wanafunzi katika shughuli za kimtagusano kama vile mazungumuzo dayolojia, michezo ya lugha, hotuba, uigizaji, na mijadala katika miktadha na mazingira yanayoakisi hali halisi.

f) Maoni na mapendekezo kuhusu jinsi ya kuboresha lugha zungumzi miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili.

g) Habari nyinginezo muhimu kwa uchunguzi huu kama vile jinsia, aina ya shule kiwango cha elimu na tajiriba ya kufundisha.

Majibu kwa maswali katika hojaji hizi yaliainishwa katika majadwali na kutumiwa kubainisha ruwaza za matumizi ya lugha, kwa kuzingatia umaratokezi, miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili wilayani Siaya.

3.6.2 Mahojiano

Mahojiano yalifanywa na walimu wa lugha katika kila shule shiriki. Mwongozo wa maswali yaliyoongoza mahojiano na walimu wa Kiswahili (Kiambatisho D) uliandaliwa kabla ya uchunguzi wenyewe. Mwongozo huu wa mahojiano ulituwezesha kusawazisha mahojiano yenyewe na kupata deta iliyohitajika kuyaafikia malengo mahsusi ya uchunguzi wetu katika shule zote tano husika. Kutokana na majibu kwa maswali ya mahojiano, walimu wa lugha walithibitisha deta iliyopatikana kupitia kwa hojaji na kutoa habari zaidi kuhusu ruwaza za matumizi ya lugha shuleni mwao.

Aidha, maelezo kuhusu aina na hali ya Kiswahili kinachozungumzwa na wanafunzi shuleni yalitolewa. Mahojiano haya pia yaliibua habari kuhusu kuwepo au kutokuwepo kwa sera inayoongeza matumizi ya lugha miongoni mwa wanafunzi shuleni; hadhi inayopewa lugha ya Kiswahili katika mazungumuzo na mapendekezo ya walimu husika kuhusu hatua za kuboresha lugha zungumzi ya Kiswahili miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili.

3.6.3 Mjarabu

Wanafunzi 20 wa kidato cha tatu katika kila shule walifanya mjarabu (Kiambatisho C) ili kutathmini umilisi wao wa matamshi fasaha ya Kiswahili. Mjarabu wenyewe ulikuwa na sehemu mbili – A na B.

Sehemu ya A ilikuwa na maswali yaliyomtaka mtahiniwa kuchagua neno moja kati ya mawili au matatu aliyopewa linalowakilisha matamshi mwafaka kujazia pengo lilokuwa limeachwa katika kila sentensi. Maswali katika sehemu hii yalituzwa jumla ya alama 45. Hata hivyo, wanafunzi wengi walipata alama za juu katika sehemu hii kutokana na uwezekano wa kubahatisha na kupata jibu sahihi. Tathmini ya sehemu hii haikutoa picha halisi ya umilishi wa

lugha zungumzi ya Kiswahili miongoni mwa watahiniwa. Hili lililazimisha mtafiti kuegemea sehemu ya B.

Sehemu ya B, kwa upande wake, ilikuwa na maswali yaliyomtaka mtahiniwa kutofautisha sentensi zilizokuwa na maneno yenye sauti zilizokanganya; kueleza tofauti za kimaana zilizotokana na matamshi ya maneno waliyopewa; kuandika upya sentensi ambazo ni zao la matamshi mabaya ili zisheheni matamshi sahihi na fasaha; na kutunga sentensi mbili kwa kila jozi ya maneno ili kuyatofautisha kimatamshi. Sehemu hii ilituzwa jumla ya alama 55. Tathmini ya sehemu hii iligeza vizuri umilishi wa lugha zungumzi ya Kiswahili kimatamshi kwa sababu haikutoa nafasi kwa kubahatisha. Mtahiniwa alilazimika kujieleza na kuonyesha umilisi wake.

Kwa jumla, matokeo ya sehemu B ndiyo yaliyotumiwa kueleza baadhi ya athari za ruwaza za matumizi ya lugha kwa umilisi wa lugha zungumzi ya Kiswahili miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili.

3.6.4 Mijadala

Kwa ushirikiano na walimu wa Kiswahili, mijadala iliandaliwa kwa wanafunzi wa kidato cha tatu katika shule tano zilizochaguliwa. Masuala ya kujadiliwa yaliafikiwa siku mbili kabla ya mjadala wenyewe. Kutokana na mijadala hii, wanafunzi walitoa hoja zao kwa mawazo yaliyofululiza kwa uhalisia wake na hivyo kubainisha umilisi wao katika Kiswahili zungumzi.

Kila mzungumzaji alipewa fursa ya dakika tano kuchangia mjadala kwa kupinga au kuunga mkono. Kila upande uliwakilishwa na washiriki kumi. Mazungumzo yalinaswa kwa kinasa sauti. Kutokana na mazungumzo haya, makosa au ukosefu wa makosa ya kimatamshi miongoni mwa wanafunzi ishirini uliorodheshwa. Kuwepo au kutokuwepo kwa makosa haya

kulitumiwa kubainisha baadhi ya athari za ruwaza za matumizi ya lugha kwa umilisi wa lugha zungumzi ya Kiswahili.

Kati ya washiriki ishirini kila mmoja alichangia shule yake alama tano. Kila kosa la kimatamshi lililofanywa lilipunguza alama hizi kwa nusu alama hadi makosa kumi. Hata hivyo, utafiti huu haukujishughulisha na aina ya kosa lenyewe la matamshi. Kwa mfano, mwanafunzi aliyefanya makosa 8 alipoteza alama 4 na kuchangia shule yake alama moja.

3.6.5 Uchunguzi Shiriki

Kupitia kwa Uchunguzi Shiriki, matumizi ya lugha zungumzi ya wanafunzi yalichunguzwa. Mazungumzo ya wanafunzi katika mahali, mazingira na miktadha mbalimbali kama vile uwanjani, darasani, wakati wa gumzo, wakati wa buraha na hata wakati wa maakuli yalichunguzwa kwa makini.

Ruwaza za matumizi ya lugha, yaani uteuzi na matumizi ya lugha mbalimbali azijuazo mzungumzaji, zilichunguzwa kwa msaada wa Mwongozo wa Uchunguzi. Uteuzi na matumizi ya lugha yalichunguzwa kwa kuzingatia: mada, mahali, miktadha, washiriki, uamilifu wa shughuli ya mtagusano husika na umaratokezi wa lugha husika katika mazungumzo ya wanafunzi.

Deta zilizopatikana zilitumiwa kufidia na kuthibitisha habari iliyopatikana kupitia kwa hojaji na mahojiano.

3.7 Uchanganuzi wa Deta

Baada ya kukusanywa, deta zote zilitathminiwa na kuainishwa kwa mujibu wa madhumuni ya utafiti. Deta zilichanganuliwa kwa kutumia uchanganuzi thamano na wingidadi. Majibu kwa kila swali la hojaji na mahojiano yaliainishwa kimakundi katika majedwali ili kubainisha ruwaza mahsusi za matumizi ya lugha zungumzi katika kila shule. Maelezo

yametolewa katika Sura ya Nne ili kufafanua yaliyomo katika majedwali. Matokeo haya yalihusishwa na matokeo ya Mjarabu - Kiambatisho C.

Matokeo ya Mjarabu na mijadala yalisaidia kubainisha athari za ruwaza za matumizi ya lugha zungumzi kwa matamshi fasaha ya Kiswahili. Kipimo cha cha wastani wa kihesabu kilitumiwa kuainisha umilisi wa matamshi ya kila shule. Alama kati ya 00 - 29 iliwakilisha 'Matamshi finyu mno'; 30 - 44 'Matamshi dhaifu'; 45 - 59 'Matamshi wastani'; 60 - 74 'Matamshi mazuri' 75 - 100 'Matamshi mazuri sana' kama inavyoonyeshwa na Kiambatisho E. Ulinganisho wa ruwaza za matumizi ya lugha na umilisi wa lugha zungumzi kimatamshi kwa kila shule ulituwezesha kufikia hitimisho kuwa wanafunzi waliofanya vyema katika mtihani wa matamshi wanatumia Kiswahili zaidi katika mazungumzo yao ilhali wale waliofanya vibaya wanatumia lugha zingine- hasa ya kwanza - mbali na Kiswahili.

Kwa jumla, uchanganuzi na muhtasari wa deta hizi ulifanywa kwa misingi ya msambao wa umaratokezi, wastani wa kihesabu na asilimia ili kufasili matokeo ya utafiti yanayowasilishwa katika Sura ya Nne. Takwimu muhimu zilizopatikana zilitumiwa katika majadiliano na kutoa mapendekezo kuhusu jinsi ya kuboresha lugha zungumzi ya Kiswahili miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili wilayani Siaya.

3.8 Hitimisho

Katika sura hii tumetoa habari kuhusu mbinu za utafiti ambazo zilitumika kufanikisha uchunguzi huu. Ufafanuzi wa kina umetolewa kuhusu njia za utafiti, jumuiya, uteuzi wa sampuli, ukusanyaji wa deta na mwishowe habari kuhusu uchanganuzi wa deta imetolewa. Sura ya Nne mejengea hapa kwa kuwasilisha uchanganuzi na ufasiri wa deta.

SURA YA NNE

UCHANGANUZI NA UFASIRI WA DETA

4.1 Utangulizi

Sura hii imewasilisha uchanganuzi na ufasiri wa deta iliyopatikana katika uchunguzi. Majedwali yametumiwa kuainisha na kueleza ruwaza za matumizi ya lugha miongoni mwa wanafunzi wa shule tano za upili wilayani Siaya. Sehemu inayofuatia imeeleza hali ya uzungumzi wa wanafunzi. Kisha, athari za matumizi ya lugha zungumzi kwa matamshi fasaha ya Kiswahili zimewasilishwa kwa takwimu ili kufanikisha ufasiri wa matokeo ya mjarabu na majadiliano. Sehemu ya mwisho imehitimisha kwa kutoa ufafanuzi kwa njia ya majadiliano.

4.2 Ruwaza za Matumizi ya Lugha

Uteuzi na matumizi ya lugha mbalimbali azijuazo mzungumzaji aghalabu hubainisha ruwaza mahsusi za matumizi ya lugha. Ruwaza hizi hutegemea na kuathiriwa na mandhari, miktadha, mada, washiriki, ujuzi wao na namna ya matumizi ya lugha zenyewe. Lugha hazipishani wala kubadilishana zamu tu bali hutofautiana kiuamilifu na kwa hivyo kila moja inapoteuliwa na kutumiwa hutekeleza jukumu la kipekee. Sehemu hii inaeleza matokeo kuhusu jumla ya lugha za wanafunzi na walimu, matumizi ya lugha katika mawanda mbalimbali, uteuzi na matumizi ya lugha miongoni mwa wanafunzi nyumbani, katika vyombo vya habari, uandishi wao wa barua na hatimaye wakiwa shuleni.

4.2.1 Jumla ya Lugha za Wanafunzi na Walimu

Ili kufanikisha maelezo kuhusu ruwaza za matumizi ya lugha miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili, watafitiwa waliuzwa kutaja idadi ya lugha ambazo hutumia katika shughuli zao za kimtagusano. Matokeo yalidhihirisha kuwa lugha tatu – Lugha ya Kwanza (L1),

Kiingereza na Kiswahili zilizungumzwa na 30%; Nne, ikiwemo Sheng zilizungumzwa na 59% ilhali 11% walizungumza lugha tano. Ni wazi kwamba matumizi ya Sheng katika mazungumzo miongoni mwa wanafunzi yamekita mizizi hata katika shule za mashambani. Isitoshe, baadhi ya wanafunzi wanatumia zaidi ya lugha mbili za kigeni na za kikabila.

Kati ya wanafunzi wote walioshiriki katika uchunguzi huu, 89% walizungumza Lugha ya Kwanza (L1) moja – Dholuo. Hili lilitokana na hali kwamba wengi wa wanafunzi katika shule za kutwa ni wakazi wa viunga vya shule husika. Hata hivyo, 11% walitumia kati ya Lunyole, Luloogoli, Kikamba, Kikisii, Gikuyu au Kinandi kama lugha zao za kwanza. Ni dhahiri kwamba shule za upili wilayani Siaya, na hasa za bweni zinasheheni hali ya wingilugha.

Matumizi ya lugha ya walimu kumi yalichunguzwa ili kuthibitisha iwapo yaliathiri yale ya wanafunzi wao. 80% ya walimu walizungumza lugha tatu ilhali 20% walizungumza lugha nne. Wote (100%) walizungumza Kiingereza na Kiswahili. 75% walitumia Dholuo kama Lugha ya Kwanza huku 25% waliobaki wakizungumza Lutsotso, Lumarachi, Lunyole au Lulogooli kama lugha yao ya kwanza.

Kwa hivyo, midahalo na shughuli nyingine za kimtagusano miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili wilayani Siaya zinatekelezwa katika mazingira ya wingilugha. Hata hivyo, mbali na Kiswahili na Kiingereza, Dholuo ni lugha muhimu na maarufu katika mazungumzo ya walimu (70%) na ya wanafunzi wao vilevile (98%). Sheng kwa upande mwingine imebainika kama lugha ya wanafunzi (69%) wala si maarufu miongoni mwa walimu wanaoipiga vita.

4.2.2 Matumizi ya Lugha Katika Mawanda Mbalimbali

Kupitia kwa hojaji, wanafunzi waliulizwa lugha walizozitumia kwa urahisi na wepesi mno katika mawanda tofauti tofauti, yaani Kuzungumza, Kusikiliza, Kuandika na Kusoma.

Kwa jumla, wanafunzi wengi walitaja Kiingereza kuwa lugha ambayo wangeweza kusoma (85%) na kuandika (79%) kwa urahisi na haraka zaidi. Kuhusu mazungumzo, 31% walipendelea Sheng, 27% Dholuo, 22% Kiingereza, 19% Kiswahili na 1% Kinandi. Usikilizaji uliripotiwa kutekelezeka kwa urahisi zaidi katika Kiswahili (28%), Kiingereza (25%), Dholuo (25%) na Sheng (22%).

Jedwali 2 Matumizi ya Lugha Katika Mawanda Mbalimbali

Lugha	**Kuzungumza**		**Kusikiliza**		**Kuandika**		**Kusoma**	
	N	**%**	**N**	**%**	**N**	**%**	**N**	**%**
Kiingereza	22	22	25	25	79	79	85	85
Kiswahili	19	19	28	28	20	20	14	14
Dholuo	27	27	25	25	00	00	00	00
Sheng	31	31	22	22	01	01	01	01
Kinandi	01	01	00	00	00	00	00	00
Jumla	**100**	**100**	**100**	**100**	**100**	**100**	**100**	**100**

Maelezo haya ya wanafunzi katika sehemu hii yalilinganishwa na yale ya sehemu zingine ili kuthibitisha na kuonyesha uhusiano uliokuwepo. Stadi ya kuzungumza ililinganishwa na lugha ya mazungumzo nyumbani, stadi ya kusoma ilihusishwa na usomaji wa magazeti na majarida, stadi ya kusikiliza ilihusishwa na usikilizaji wa vipindi vya redio ilhali stadi ya kuandika ilihusishwa na uandishi wa barua.

4.2.3 Matumizi ya Lugha Nyumbani

Uteuzi na matumizi ya lugha nyumbani huathiriwa na kuchochewa na sababu muhimu mbalimbali. Kwingi, hata hivyo, yaelekea Lugha ya Mama huteuliwa na kutumiwa kwa sababu tofauti tofauti. Katika uchunguzi wetu, moja kati ya sababu zilizoathiri uteuzi huu ilikuwa jumla ya lugha wazijuazo wanafunzi kwa upande mmoja, na wazazi na wale wapatikanao nyumbani kwa upande mwingine. Hali hii iliwawekea watafitiwa vikwazo katika uteuzi wao lugha nyumbani.

Kutuwezesha kueleza matumizi ya lugha nyumbani, watafitiwa waliulizwa kudokeza habari kuhusu matumizi ya lugha katika mazungumzo nyumbani, umilisi wa wazazi katika kuzungumza lugha mbalimbali na kueleza iwapo waliwekewa vikwazo vyovyote kwa matumizi ya lugha fulani nyumbani.

Kufanikisha maelezo kuhusu matumizi ya lugha mbalimbali nyumbani, wanafunzi waliulizwa kutaja lugha mbalimbali wanazozitumia sana wanapozungumza na wazazi, ndugu na dada, marafiki jirani na wanapopiga gumzo na marafiki nje ya shule. Matokeo katika shule zote yalibainisha Sheng (34.5%) na Dholuo (33.75%) kuwa lugha zilizotawala midahalo ya watafitiwa nyumbani. Sheng ndiyo lugha iliyotumiwa sana katika mazungumzo na marafiki ilhali mazungumzo na wazazi yalifanyika katika Dholuo (L1). Kiswahili na Kiingereza pamoja na lugha zingine za kikabila kama vile Kisii, Lunyole na Kinandi zilisemekana kutumika nyumbani na wachache mno. Muhtasari huu unajitokeza vyema katika Jedwali 3 lifuatalo:

Jedwali 3 Matumizi ya Lugha Katika Mazungumzo Nyumbani

Lugha	Mazungumzo na Wazazi		Mazungumzo na Ndugu & Dada		Mazungumzo na Marafiki Jirani		Gumzo na Marafiki Nje ya shule		Jumla	
	N	%	N	%	N	%	N	%	N	%
Dholuo	76	76	25	25	27	27	07	07	135	33.75
Kiingereza	06	06	07	07	08	08	10	10	31	7.75
Kiswahili	17	17	34	34	19	19	19	19	89	22.25
Sheng	00	00	33	33	45	45	60	60	138	34.50
Kisii	01	01	00	00	01	01	00	00	02	0.50
Lunyole	00	00	00	00	00	00	01	01	01	0.25
Sheng & Dholuo	00	00	00	00	00	00	03	03	03	0.75
Kinandi	00	00	01	01	00	00	00	00	01	0.25
Jumla	100	100	100	100	100	100	100	100	400	100.00

Kufidia deta tuliyoipata kuhusu matumizi ya lugha nyumbani, wanafunzi waliulizwa kugeza umilisi wa wazazi wao katika kuzungumza Kiswahili, Kiingereza na Sheng. Hili tulilifanya ili kuthibitisha iwapo umilisi wa wazazi katika lugha mbalimbali uliathiri uteuzi na matumizi ya lugha mbalimbali nyumbani. Jambo hili lilipewa msukumo na hali kwamba umilisi wa wazazi katika kutumia lugha hizi ungewafanya ama kuzitumia au kutozitumia katika mazungumzo na watoto wao. Wanafunzi waliwageza wazazi wao kwa kutumia kipimo cha viwango vinne – 'Vizuri Sana', 'Vizuri', 'Sio Vizuri Sana' na 'Hajui hata kidogo'. Matokeo yameainishwa katika Jedwali 4 hapa chini.

Jedwali 4 Umilisi wa Wazazi Kimazungumzo

Uzungumzi wa Kina Baba

Lugha	Vizuri Sana		Vizuri		Sio Vizuri Sana		Hajui		Hayuko		Jumla
	N	%	N	%	N	%	N	%	N	%	
Kiswahili	24	24	32	32	33	33	00	00	11	11	100
Kiingereza	48	48	27	27	10	10	04	04	11	11	100
Sheng	00	00	02	02	23	23	64	64	11	11	100

Uzungumzi wa Kina Mama

Lugha	Vizuri Sana		Vizuri		Sio Vizuri Sana		Hajui		Hayuko		Jumla
	N	%	N	%	N	%	N	%	N	%	
Kiswahili	31	31	35	35	22	22	02	02	10	10	100
Kiingereza	35	35	23	23	25	25	07	07	10	10	100
Sheng	01	01	04	04	22	22	63	63	10	10	100

Matokeo yalidhihirisha kuwa wazazi wa watafitiwa hawana umilisi katika kuzungumza Sheng (idadi ya wale ambao 'hawaijui kabisa' na wenzao ambao 'hawaijui vizuri sana' wakijumlishwa pamoja) – 87% ya kina baba na 85% ya kina mama. Hali hii inaweza kuhusishwa na uhalisia kwamba lugha hii, kimsingi, hutumiwa na vijana katika mazungumzo kati yao ili kujitenga kimawasiliano na wazee wao. Wazee nao kwa upande wao huiona Sheng, kama lugha ya 'kihuni' au ya vijana mitaani na ambayo haifai kutiliwa maanani. Hali hii inawapelekea kupiga vita matumizi ya Sheng nyumbani.

Ni dhahiri kwamba wazazi wa wanafunzi hawa wana umilisi mzuri wa kuzungumza Kiswahili na Kiingereza, yaani idadi ya wale walioelezwa kuzuzingumza lugha hizi 'vizuri sana' na 'vizuri' wakijumlishwa pamoja. Miongoni mwao, 56% ya kina baba na 66% ya kina mama waliripotiwa kuwa na umilisi wa kuzungumza Kiswahili huku 75% ya kina baba na 58% ya kina mama walikuwa na uwezo wa kutumia Kiingereza. Umilisi huu unaweza kuhusishwa na elimu, mielekeo yao chanya na mchango wa vyombo vya habari kama vile redio na magazeti na kuingiliana kwao na watu wanaozungumza lugha tofauti za kikabila hasa mijini na kulazimika kutumia *lingua franca* - Kiswahili au Kiingereza.

Hata hivyo, kinachoibuka hapa ni kwamba ujuzi wa wazazi kuzungumza Kiswahili na Kiingeza haukuathiri uteuzi na matumizi ya lugha kati yao na watoto wao nyumbani. Hali hii ilitupelekea kuchunguza nafasi ya vikwazo katika matumizi ya lugha nyumbani. Vikwazo vya

kijamii na vile vitokanavyo na wazazi vinaweza kuwa na athari kubwa kwa uteuzi na matumizi ya lugha miongoni mwa wanafunzi.

Ni katika maanzili haya ambapo watafitiwa waliulizwa kueleza iwapo walikumbana na vikwazo vyovyote katika uteuzi na matumizi yao ya lugha nyumbani. Wanafunzi wengi, kama Jedwali 5 linavyoonyesha, hawakupingwa na wazazi wao kutumia lugha fulani nyumbani.

Jedwali 5 Vikwazo Kuhusu Matumizi ya Lugha Nyumbani

Shule	**Kuna Vikwazo**		**Hakuna Vikwazo**		**Jumla**	
	N	%	N	%	N	%
A	04	20	16	80	20	100
B	02	10	18	90	20	100
C	05	25	15	75	20	100
D	06	30	14	70	20	100
E	05	25	15	75	20	100
Jumla	**22**	**22**	**78**	**78**	**100**	**100**

Matokeo katika Jedwali 5 hapo juu yanadhihirisha kuwa 78% ya watafitiwa hawakukabiliana na vikwazo vyovyote katika matumizi yao ya lugha nyumbani. Hata hivyo, baadhi ya watafitiwa (22%) walipingwa kutumia baadhi ya lugha wazijuazo. Shule A (20%), Shule B (10%), Shule C (25%), Shule D (30%) na Shule E (25%) ndizo zilizokumbwa na hali hii. Hili lilituchochea kutafuta kujua ni lugha ipi au zipi ambazo hazikupendekezwa katika matumizi nyumbani na sababu zilizochochea uamuzi kama huu kufanywa. Jedwali 6 hapa chini linatoa muhtasari wa deta hii.

Jedwali 6 Lugha Zisizopendekezwa

Shule	LUGHA													
	Sheng		Kiingereza		Kiswahili		L1		Nyinginezo		Hakuna Vikwazo		Jumla	
	N	%	N	%	N	%	N	%	N	%	N	%	N	%
A	02	10	02	10	00	00	00	00	00	00	16	80	20	100
B	01	05	01	05	00	00	00	00	00	00	18	90	20	100
C	05	25	00	00	00	00	00	00	00	00	15	75	20	100
D	04	20	00	00	00	00	02	10	00	00	14	70	20	100
E	03	15	01	05	00	00	00	00	01	05	15	75	20	100
Zote	**15**	**15**	**04**	**04**	**00**	**00**	**02**	**02**	**01**	**01**	**78**	**78**	**100**	**100**

Matokeo katika Jedwali 6 yanadhihirisha kwamba matumizi ya Sheng (15%), Kiingereza (4%) Dholuo (L1, 2%) na lugha nyinginezo (1%) hayakupendekezwa nyumbani mwa baadhi ya wanafunzi. Kutopendelewa kwa Sheng nyumbani kuliripotiwa miongoni mwa watafitiwa 15 kati ya watafitiwa wote 22 waliokumbwa na vikwazo hivi. Hali hii ilitokana na uhalisia kwamba watu wengi nyumbani na katika ujirani hawakuelewa wala kutumia lugha ya Sheng na ndiposa haikupendekezwa. Wengi wao, hasa wazee na wasioifahamu wala kuielewa, huifikiria lugha hii kuwa ya 'kihuni' au ya vijana mijini.

Isitoshe, japo wanafunzi wengi (78%) waliripoti kutotingwa katika uteuzi na matumizi yao ya lugha, ni dhahiri kwamba kuwepo kwa washiriki katika mazungumzo wasioelewa lugha kama Kiswahili au Kiingereza kuliathiri uteuzi na matumizi yao ya lugha. Kwa jumla, kuwepo kwa vikwazo kama hivi kulitinga uhuru wa uteuzi na matumizi ya lugha nyumbani na kwa kiwango fulani kuathiri matumizi na umilisi wa kutumia lugha zungumzi fasaha ya Kiswahili.

4.2.4 Lugha ya Usomaji wa Magazeti na Usikilizaji wa Redio

Vyombo vya habari vina nafasi nzuri ya kuathiri fikra na mielekeo ya umma kwa jumla na hasa vijana. Vinaweza kujenga au kubomoa; vinaweza kukuza au kudumaza; vinaweza kuchochea hisia chanya au hasi kuhusu lugha fulani. Ni katika muktadha huu ambapo tulitafuta kujua habari kuhusu usikilizaji wa vipindi vya redio na usomaji wa magazeti na majarida katika lugha mbalimbali. Hili tulifanya ili kuhakikisha iwapo usikilizaji na usomaji kama huo uliathiri uteuzi na matumizi ya lugha zungumzi fasaha ya Kiswahili.

Kufanikisha maelezo kuhusu usomaji wa magazeti na majarida katika lugha mbalimbali, watafitiwa waliulizwa kueleza usomaji wao wa machapisho hayo katika Kiswahili, Kiingereza, Lugha ya Mama na Sheng kwa kuzingatia viwango vinnne – 'mara kwa mara', 'mara moja moja', 'kwa nadra sana' , na 'hata/hata kidogo'. Muhtasari wa matokeo haya umeaiknishwa katika Jedwali 7 hapa chini.

Jedwali 7 Usomaji wa Magazeti na Majarida

ugha	Mara Kwa Mara		Mara Moja Moja		Kwa Nadra Sana		Hata/Hata Kidogo		Jumla	
	N	%	N	%	N	%	N	%	N	%
wahili	41	41	43	43	15	15	01	01	100	100
gereza	85	85	11	11	04	04	00	00	100	100
	06	06	17	17	37	37	40	40	100	100
ng	38	38	09	09	24	24	29	29	100	100

Kwa jumla, wanafunzi wengi walieleza kusoma magazeti na majarida ya Kiingereza mara kwa mara (85%). Usomaji katika Kiswahili uliripotiwa miongoni mwa 41% ya wanafunzi. Usomaji wa magazeti katika lugha ya Sheng uliripotiwa miongoni mwa 38% ya wanafunzi.

Wengi wao waliripoti kusoma magazeti katika Lugha ya Mama kwa nadra sana. Ajabu ni kwamba magazeti haya, hasa ya kisiasa na kidini, yalisemekana kuwepo.

Watafitiwa waliulizwa kueleza usikilizaji wao wa vipindi vya redio katika Kiswahili, Kiingereza, Lugha ya Mama na Sheng. Maelezo haya yalitolewa kwa kuzingatia viwango vinne- 'mara kwa mara', 'mara moja moja', 'kwa nadra sana' na 'hata/hata kidogo'. Majibu ya wanafunzi yaliyoainishwa katika Jedwali 8 hapa chini yanaonyesha kuwa wanafunzi wengi walieleza kusikiliza vipindi vya redio katika Kiswahili kuliko Kiingereza, Sheng au Lugha ya Mama. Usikilizaji wao mwingi uliripotiwa kutekelezeka vyema zaidi katika Kiswahili (70%), Kiingereza (65%), Sheng (37%) na hatimaye Lugha ya Mama (13%).

Jedwali 8 Usikilizaji wa Vipindi vya Redio

Lugha	Mara kwa Mara		Mara Moja Moja		Kwa Nadra Sana		Hata		Jumla	
	N	%	N	%	N	%	N	%	N	%
Kiswahili	70	70	24	24	06	06	00	00	100	100
Kiingereza	65	65	26	26	09	09	00	00	100	100
Sheng	37	37	23	23	15	15	25	25	100	100
L1	13	13	23	23	43	43	21	21	100	100

4.2.5 Lugha ya Uandishi wa Barua

Kupitia kwa hojaji wanafunzi walihitajika kueleza ni lugha ipi waliyotumia sana katika kuandika barua kwa marafiki, wazazi na wengine. Hapa, 'wengine' walichukuliwa kuwa watu wasio na uhusiano wa karibu na watafitiwa. Majibu yao yalisheheni matokeo yaliyoainishwa katika Jedwali 9 hapa chini:

Jedwali 9 Lugha ya Uandishi wa Barua

LUGHA	UANDISHI WA BARUA KWA:							
	Marafiki		Wazazi		Wengine		Jumla	
	N	%	N	%	N	%	N	%
Kiingereza	47	47	51	51	77	77	175	58.3
Kiswahili	10	10	20	20	18	18	48	16.0
Lugha ya Mama	01	01	29	29	04	04	34	11.3
Sheng	42	42	00	00	01	01	43	14.3
Jumla	100	100	100	100	100	100	300	100

Kwa mujibu wa Jedwali 9, ni dhahiri kwamba Kiingereza ndiyo lugha maarufu zaidi katika mawasiliano kupitia uandishi wa barua, yaani 47% kwa marafiki, 51% kwa wazazi na 77% kwa wengine. Katika uandishi wao wa barua kwa jumla, wanafunzi walielekea kupendelea Kiingereza (58.3%), Kiswahili (16.0%) wala sio Sheng (14.3%) au Lugha ya Mama (11.3%).

4.2.6 Matumizi ya Lugha Shuleni

Shuleni, lugha kuu za mawasiliano ni Kiswahili na Kiingereza kama lugha rasmi. Kiingereza hutumiwa kufundishia masomo yote isipokuwa Kiswahili na lugha zingine za kigeni. Ijapokuwa matumizi ya Sheng na Lugha za Kikabila yamepigwa marufuku katika shule nyingi, umaarufu wa lugha hizo ni jambo ambalo haliwezi kupuuziliwa mbali. Kwa jumla, hata hivyo, uteuzi na matumizi ya lugha nje ya darasa kwa kiasi fulani hutegemea utekelezaji wa kaida za shule na utendakazi wa sera ya lugha shuleni.

Kutuwezesha kueleza ruwaza za matumizi ya lugha shuleni, watafitiwa waliulizwa kutoa habari kuhusu matumizi yao ya lugha katika hali, mahali na miktadha mbalimbali ya maingiliano shuleni. Hili walifanya kwa kueleza lugha ya mazungumzo na mwalimu, lugha katika miktadha mbalimbali ya maingiliano, lugha ya mazungumzo na wanafunzi kutoka shule nyingine, lugha

katika majadiliano ya mada na masomo mbalimbali na sera ya lugha shuleni. Habari hizi zilithibitishwa kupitia uchunguzi shiriki.

4.2.6.1 Lugha ya Mazungumzo na Mwalimu

Watafitiwa waliulizwa kutaja lugha waliyoitumia kwa urahisi katika mazungumzo yoyote yale na mwalimu. Ijapokuwa wengi katika shule zote walielekea kupendelea Kiingereza katika mazungumzo ya aina hii, tofauti ndogo ndogo ziliibuka kutoka shule moja hadi nyingine kama inavyobainika katika Jedwali 10 hapa chini.

Kwa jumla, hali iliyoibuka ni kuwa Kiingereza (62%) ndiyo lugha iliyokuwa maarufu zaidi katika mazungumzo na mwalimu katika takribani shule zote. Baadhi ya wanafunzi walitumia mseto wa Kiingereza na Kiswahili (24%) huku wachache (14%) wakitumia Kiswahili hasa. Sheng na Lugha ya Mama hazikupewa nafasi kimatumizi katika mawasiliano ya aina hii. Kwa hivyo, walimu waliathiri lugha iliyoteuliwa na kutumiwa na wanafunzi katika mazungumzo nao.

Jedwali 10 Lugha ya Mazungumzo na Mwalimu

Shule	A		B		C		D		E		Jumla	
Lugha	N	%	N	%	N	%	N	%	N	%	N	%
Lugha ya Mama hasa	00	00	00	00	00	00	00	00	00	00	00	00
Kiswahili hasa	04	20	00	00	04	20	03	15	03	15	14	14
Kiingereza hasa	14	70	02	10	15	75	17	85	14	70	62	62
Kiingereza na Kiswahili	02	10	18	90	01	05	00	00	03	15	24	24
Sheng	00	00	00	00	00	00	00	00	00	00	00	00
Jumla	20	100	20	100	20	100	20	100	20	100	100	100

4.2.6.2 Lugha ya Mazungumzo na Wanafunzi Kutoka Shule Nyingine

Wanafunzi waliulizwa kutaja ni lugha ipi waliyotarajia kutumia katika mazungumzo na wanafunzi kutoka shule nyingine. Majibu yao yalitofautiana kutoka shule moja hadi nyingine kama vile Jedwali 11 linavyoonyesha.

Hata hivyo, wanafunzi wengi (45%) waliripoti kutumia Sheng katika mazungumzo na wenzao kutoka shule nyingine. 22% walitaja Kiingereza, 21% Kiswahili na 12% mseto wa Kiswahili na Kiingereza.

Jedwali 11 Lugha ya Mazungumzo na Wanafunzi Kutoka Shule Nyingine

Shule	A		B		C		D		E		Jumla	
Lugha	N	%	N	%	N	%	N	%	N	%	N	%
Lugha ya Mama hasa	00	00	00	00	00	00	00	00	00	00	00	00
Kiswahili hasa	05	25	02	10	07	35	05	25	02	10	21	21
Kiingereza hasa	06	30	03	15	04	20	04	20	05	25	22	22
Kiingereza na Kiswahili	02	10	06	30	01	05	00	00	03	15	12	12
Sheng	07	35	09	45	08	40	11	55	10	50	45	45
Jumla	20	100	20	100	20	100	20	100	20	100	100	100

4.2.6.3 Lugha Katika Majadiliano ya Mada na Masomo Mbalimbali

Maelezo kuhusu jinsi kubadilika kwa mada au masomo mbalimbali kunavyoathiri uteuzi na matumizi ya lugha katika miktadha isiyo rasmi yalifanikishwa na majibu ya watafitiwa kwa swali lililowataka kutaja ni lugha ipi waliyotarajia kutumia katika mazungumzo kuhusu Hisbati, Kemia, Fasihi katika Kiingereza, Fasihi katika Kiswahili na Sherehe ya kitamaduni. Majibu yao yalibainisha ruwaza zilizodokezwa katika Jedwali 12 hapa chini.

Matokeo katika shule zote yalionyesha masomo ya Hisbati, Kemia, na Fasihi katika Kiingereza yalijadiliwa na takriban wanafunzi wote katika Kiingereza, yaani 90%, 96% na 94%

mtawalia. Somo la Fasihi katika Kiswahili nalo lilijadiliwa katika Kiswahili (99%). Mada kuhusu sherehe ya kitamaduni zilijadiliwa pakubwa katika Lugha ya Mama (71%).

Jedwali 12 Lugha Katika Majadiliano ya Mada na Masomo Mbalimbali

Somo / Mada	Kiingereza		Kiswahili		Lugha ya Mama		Sheng	
	N	%	N	%	N	%	N	%
Hisbati	90	90	04	04	01	01	05	05
Kemia	96	96	03	03	00	00	01	01
Fasihi katika Kiingereza	94	94	04	04	01	01	01	01
Fasihi katika Kiswahili	00	00	99	99	00	00	01	01
Sherehe ya Kitamaduni	10	10	12	12	71	71	07	07
Jumla	290	58.0	122	24.4	73.0	14.6	15	3.0

4.2.6.4 Matumizi ya Lugha Mahali Mbalimbali mwa Maingiliano Shuleni

Eneo la shule aghalabu huwa pana na lenye mahali mbalimbali ambamo maingiliano miongoni na baina ya wanafunzi, wafanyikazi, walimu na hata wageni shuleni hutendeka. Kila mahali pa maingiliano huhitaji matumizi ya lugha maalumu ambayo ni mwafaka kwa mada na vitendo vinavyoendelea. Kutuwezesha kueleza jinsi kubadilika kwa mahali kulivyoathiri uteuzi na matumizi ya lugha shuleni, wanafunzi waliulizwa kutaja lugha waliyoitumia hasa katika sehemu mbalimbali za maingiliano shuleni - darasani, bwenini, uwanjani, ukumbini mwa maakuli na njiani wakielekea nyumbani. Muhtasari wa matokeo haya umetolewa katika Jedwali 13 hapa chini.

Baadhi ya vitendo vilivyopelekea wanafunzi kutumia lugha darasani ni kama vile kuazima vitabu, madaftari na kalamu. Mbali na kupiga soga, lugha pia ilihitajika katika majadiliano ya wanafunzi kuhusu masomo, mada na walimu wao. Hata hivyo, kuwepo kwa mwalimu kuliathiri uteuzi na matumizi ya lugha darasani.

Bwenini lugha ilitumika kuzungumzia matukio ya siku nzima, hali ya anga, kupiga gumzo, kuazima vitu mbalimbali na kuzungumzia matamanio yao. Wanafunzi waliotarajiwa kujibu maswali katika sehemu hii walikuwa wa shule za bweni pekee yao.

Uwanjani, lugha moja haikujitokeza kuwa maarufu zaidi kuliko zingine. Wanafunzi wengi walisikika wakizungumza zaidi ya lugha moja. Isitoshe, kuchanganya ndimi, kuhamisha msimbo na kubadilisha msimbo kulijitokeza sana. Hali hizi zilielekea kutegemea mada iliyozungumziwa, miktadha au mandhari na vitendo vya mawasiliano. Jambo ambalo liliafikiana na sifa wanazozitoa Aswani, B. na wenzake (2006: 71-74) kuhusu ubadilishaji na uchanganyaji msimbo.

Katika ukumbi wa maakuli lugha ilitumika kuzungumzia hali ya chakula, kulalamika kuhusu hali ya chakula na kuomba nyongeza. Lugha pia ilitumika kumpongeza mpishi, kukashifu waliokula vibaya, kulinganisha kiasi cha chakula miongoni mwa walaji mbalimbali na kupiga gumzo vilevile.

Swali kuhusu matumizi ya lugha njiani liliwahusu watafitiwa katika shule za kutwa pekee (yaani shule A, B na E). Wanafunzi walitakiwa kueleza lugha waitumiayo wanaposafiri kwenda na kurudi shuleni kila asubuhi na jioni.

Kwa jumla, Sheng ndiyo lugha iliyotumika mahali kwingi zaidi (43.7%), Kiswahili (17.3%), na mseto wa Kiswahili na Kiingereza (13.7%). Lugha ya Mama haikutumika katika sehemu nyingi za maingiliano shuleni.

Jedwali 13 Matumizi ya Lugha Mahali Mbalimbali mwa Maingiliano Shuleni

LUGHA	MAHALI											
	Darasani		Uwanjani		Ukumbi wa Maakuli		Bwenini		Njiani		Jumla	
	N	%	N	%	N	%	N	%	N	%	N	%
L1	00	00	01	01	08	08	05	11.5	17	29.8	31	7.8
Kiswahili	19	19	22	22	18	18	03	7.0	07	12.2	69	17.3
Kiingereza	25	25	08	08	10	10	03	7.0	06	10.5	52	13.0
Kiingereza&Kiswahili	29	29	10	10	11	11	04	9.3	01	1.8	55	13.7
L1 na Kiswahili	01	01	01	01	02	02	02	4.7	05	8.8	11	2.8
L1 na Kiingereza	00	00	01	01	03	03	01	2.3	02	3.5	7	1.7
Sheng	26	26	57	57	48	48	25	58.2	19	33.3	175	43.7
Jumla	100	100	100	100	100	100	43	100	57	100	400	100

4.2.6.5 Sera ya Lugha Shuleni

Kuhakikisha kwamba wanafunzi wanatumia muda wao mwingi kujizoesha kuzungumza Kiingereza na Kiswahili, shule nyingi huweka sera ya lugha ili kuthibiti matumizi ya Lugha ya Kwanza na Sheng. Hali hii huathiri uteuzi na matumizi ya lugha miongoni mwa wanafunzi. Ni kutokana na maanzili haya ambapo tulitafuta kujua iwapo kulikuwa na sera ya lugha katika shule zilizochunguzwa. Hili lilifanywa kupitia kwa majibu kwa maswali ya hojaji kwa wanafunzi na walimu ambao walihitajika kueleza changamoto na utekelezaji wa sera ya lugha husika.

Majibu ya wanafunzi katika shule A ambayo yalithibitishwa na walimu wao (kupitia kwa hojaji na mahojiano) yalionyesha kuwa palikuwepo sera ya lugha iliyoongeza matumizi ya lugha shuleni. Kwa mujibu wa sera hii ya lugha, wanafunzi walihitajika kutumia Kiingereza kuanzia Jumatatu hadi Alhamisi. Kiswahili kilitumiwa Ijumaa pekee. Lugha ya Mama na Sheng zilikuwa

marufuku shuleni. Waliopatikana wakizitumia wangeadhibiwa. Walimu walieleza lengo la sera hii kuwa kustawisha Kiswahili na Kiingereza kimatamshi na kimawasiliano.

Kuhusu uzingatiaji wa sera hii ya lugha, walioripoti kuizingatia 'vizuri sana' (10%) walieleza kusoma vitabu vingi vya Kiswahili na Kiingereza na kutozungumza Lugha ya Mama wakiwa shuleni. Walioizingatia 'vizuri' (30%) walikiri kutoitii sera ya lugha mara moja hasa wakiwa pekee yao bila mwalimu au kiranja. Wengi wao (50%) walioeleza 'kutoizingatia vizuri sana' walishikilia kuwa walifanya hivyo kwa kuitii (sera ya lugha) kwa kiwango fulani tu kwa sababu ni kaida ya shule na kwamba mara nyingi walijikuta wamezichanganya lugha hizi au hata kutumia ya kwanza. Waliokiri kutoizingatia (10%), walitumia Lugha ya Mama hasa katika midahalo yao. Ni dhahiri kwamba wengi wa watafitiwa (60%) ama 'hawaizingatii vizuri sana' au 'hawaizingatii hata kidogo' kama inavyobainika katika Jedwali 14 hapo chini.

Wakieleza kuhusu utekelezaji wa sera ya lugha shuleni, walimu katika shule A walithibitisha deta iliyotolewa na wanafunzi kwa kushikilia ama utekelezaji wake umefanikisha 'kwa kiwango fulani tu' au 'hauna mafanikio makubwa'. Hili walisema linatokana na uhalisia kwamba mara nyingi wanafunzi hutumia Lugha ya Mama na kwamba kuna pingamizi kutoka kwa baadhi ya walimu na wanafunzi wanaopuuza matumizi ya Kiswahili na kupendelea Kiingereza.

Kwa maoni yao, 55% ya wanafunzi katika shule A walipendekeza Kiswahili kitumike katika mawasiliano shuleni. Hili walisema ni kwa sababu Kiswahili ni lugha inayoeleweka kwa urahisi na wengi, ni lugha ya taifa iliyo na wazungumzaji wengi na kwamba hii ni fursa nzuri ya kuinua matokeo ya Kiswahili katika mitihani ya kitaifa kwani ni ya chini mno. 30% walipendekeza Kiingereza kwa sababu masomo mengi hufundishwa kwayo, inaeleweka na kusomeka kwa urahisi na ni lugha ya kimataifa. Mseto wa Kiswahili na Kiingereza ulipendekezwa na 10% walioeleza kuwa hii ndiyo njia ya kufanikisha mawasiliano mingoni mwa

watu wa matabaka mbalimbali shuleni na nje. 5% waliopendekeza Sheng waliitetea kwa kusema kuwa ni lugha ya kisasa na maarufu katika midahalo ya wanafunzi.

Shule B iliripotiwa kuwa na sera ya lugha. Sera hii iliwataka wanafunzi kutumia Kiingereza na Kiswahili pekee shuleni. Lugha ya Mama na Sheng hazikuruhusiwa. Kiiingereza kilitumiwa kuanzia Jumatatu hadi Alhamisi ilhali Kiswahili kilitumika Ijumaa. Lengo kuu la sera hii ni kuboresha matumizi ya Kiswahili na Kiingereza miongoni mwa wanafunzi.

Kati ya watafitiwa wote katika shule B, 20% waliripoti kuzingatia sera ya lugha 'vizuri sana' mandhali hawakutumia Sheng wala Lugha ya Mama shuleni. 45% walieleza kuizingatia 'vizuri' kwa sababu walijaribu kuizingatia 'japo sio kikamilifu kwani wakati mwingine huzungumza Kiingereza siku ya Kiswahili au kinyume chake'. Waliokiri 'kutoizingatia vizuri sana' walikuwa 35%. Hawa walikiri kuizingatia tu pale palipo mwalimu au kiranja 'msaliti'. Hali hii ilipelekea walimu wao kueleza utekelezaji wa sera ya lugha kuwa ama 'hauna mafanikio makubwa' au 'umefanikishwa kwa kiwango fulani'. Hili, walisema linatokana na tatizo la kimielekeo kuwa Kiswahili ni kigumu miongoni mwa wanafunzi.

Wakipendekeza ni lugha ipi itumike kama njia ya mawasiliano shuleni, 50% ya watafitiwa walipendekeza Kiswahili na Kiingereza ili kufanikisha uelewa wa maswali katika mitihani yoyote ile. Aidha, lugha hizi zingewawezesha kuwasiliana na watu wa matabaka mbalimbali. 15% walipendekeza Kiswahili pekee kwa sababu wanafunzi wengi walikielewa na kwamba hii ingekuwa njia mojawapo ya kuikuza lugha ya Kiswahili kimatumizi kwani kilikuwa kimepuuzwa na wengi katika janibu hizo. Kiingereza kilipendekezwa na 30% waliokitetea kuwa lugha rasmi na ya kimataifa, kwamba ni lugha inayotumiwa kufundishia na katika mitihani na kwamba wanafunzi wengi walikuwa na ufasaha katika kuzungumza Kiingereza. 5% waliopendekeza Sheng walishikilia kuwa ni lugha maarufu miongoni mwa wanafunzi wengi.

Kutokana na majibu ya wanafunzi na ambayo yalithibitishwa na walimu, hakukuwa na sera yoyote iliyoongoza matumizi ya lugha katika shule C. Kwa hivyo, utekelezaji wa sera yoyote ile haukuwepo hata kidogo. Hata hivyo, matumizi ya Lugha ya Kwanza hayakuwa dhahiri. Wanafunzi walielekea kuteua na kutumia kati ya Kiingereza, Kifaransa, Kiswahili, na kwa kiwango fulani Sheng.

Wakitoa maoni kuhusu lugha waliyoipendekeza itumike kama njia ya mawasiliano shuleni, wengi kati ya watafitiwa (80%) katika katika shule C walipendekeza Kiingereza. Walipendekeza Kiingereza kwa sababu ndiyo lugha inayotumika kufundishia masomo mengi, ni lugha rasmi nchini Kenya na kwamba ni ya kimataifa, ni lugha ya kifahari, ni muhimu katika kutafuta kazi katika sekta mbalimbali na kwamba waliona haja ya kujizoesha kimatumizi katika Kiingereza ili kuboresha ujuzi wao wa kuizungumza. 10% waliopendekeza Kiswahili walikitetea kwa kusema ni lugha rahisi kuzungumza sio tu shuleni bali hata nje ya shule na watu wa kawaida. Kwa upande wao, 10% waliopendekeza Sheng waliitetea kuwa inaeleweka na kupendwa na wanafunzi wengi na baadhi ya walimu wao.

Shule D iliripotiwa kuwa na sera ya lugha shuleni. Hii ililenga kuimarisha Kiingereza na Kiswahili miongoni mwa wanafunzi. Sera hii iliwataka wanafunzi kutumia Kiswahili Jumatatu na Ijumaa na Kiingereza siku za wiki zilizosalia. Kiingereza na Kiswahili ndizo lugha zinazopendekezwa kwa matumizi shuleni ilhali Sheng na Lugha ya Kwanza ni marufuku.

Walipoulizwa kueleza kuzingatia kwao kwa sera ya lugha, 30% ya wanafunzi katika shule D walieleza kuizingatia 'vizuri sana'. Hili walifanya kwa kutii kaida za shule na kwamba waliiona kama njia mojawapo ya kuwawezesha kupita mitihani yao na ya kuwawezesha kuendeleza na kukuza ufasaha na umilishi wao katika Kiswahili na Kiingereza. Vile vile, 25% walikiri kuizingatia sera ya lugha 'vizuri' kwa sababu walitumia Kiingereza na Kiswahili katika mazungumzo yao kila wakati. Hata hivyo, 50% waliokiri 'kutoizingatia sera ya lugha vizuri

sana' walieleza kuwa wakati mwingine hutumia Sheng na hata Lugha ya Mama katika mazungumzo na marafiki. Hakuna mwanafunzi aliyedai 'kutoizingatia hata kidogo'.

Wakieleza kuhusu utekelezaji wa sera ya lugha shuleni, walimu kwa upande wao walielekea kuthibitisha waliyoyasema wanafunzi kwa kueleza kuwa ama, umefanikishwa 'kwa kiwango fulani' au 'hauna mafanikio makubwa'. Hili walieleza lilitokana na kutowajibika miongoni mwa wanafunzi kwa upande mmoja na walimu wa lugha kwa upande mwingine.

Wakipendekeza lugha ya mawasiliano shuleni, 25% ya wanafunzi katika shule D walipendekeza Kiswahili. Hili walisema ni kwa sababu Kiswahili kinaeleweka na kufahamika na watu wengi, ni lugha ya kiafrika inayounganisha makabila mbalimbali na kwamba kwa kufanya hivyo wangeweza sio tu kukuza ufasaha wao bali kuboresha matokeo yao katika mitihani ya Kiswahili vilevile. 15% walipendekeza Kiingereza kwa sababu kinaeleweka na wengi nchini Kenya, ni lugha ya kimataifa na ya teknolojia ya habari na mawasiliano na kuwa ni lugha inayotumiwa shuleni kufundishia. Hata hivyo, wengi wao (80%) walipendekeza Kiswahili kutumika sambamba na Kiingereza kwa sababu lugha hizi hutumika kwa majukumu mbalimbali na wanajamii na matabaka mbalimbali nchini Kenya, kwamba zote ni lugha za kimataifa na kwamba kuzikuza lugha hizi sambamba ni kukuza masomo yote yanayotahiniwa katika mitihani ya kitaifa. Hakuna aliyependeza Sheng itumiwe katika mawasiliano shuleni.

Kuwepo kwa sera ya lugha katika Shule E kulihakikishwa na majibu ya walimu na wanafunzi kwa maswali ya hojaji na mahojiano. Lugha zilizopendekezwa kwa matumizi shuleni ni Kiswahili na Kiingereza. Kiingereza kilitumiwa kuanzia Jumatatu hadi Alhamisi ilhali Kiswahili kilitumika Ijumaa. Sheng na Lugha ya Mama zilikuwa marufuku. Wanafunzi wa bweni walitarajiwa kuteua na kutumia kati ya Kiswahili na Kiingereza Jumamosi na Jumapili. Lengo la sera hii ya lugha lilielezwa kuwa kuboresha matumizi na ufasaha wa Kiswahili na Kiingereza kwa kuzitumia katika midahalo shuleni.

Wakijibu swali kuhusu kuzingatia kwao kwa sera ya lugha 20% ya watafitiwa katika shule E walijibu: 'vizuri sana' yaani waliifuata bila tashwishi. 30% miongoni mwao walieleza kuizingatia 'vizuri'. Hata hivyo, 50% walikiri 'kutoizingatia vizuri sana' - yaani baadhi yao walishindwa kuwasilisha ujumbe wao vyema kwa Kiswahili na Kiingereza na hivyo kutumia Lugha ya Kwanza, wengine walijikuta wamezungumza Sheng, Lugha ya Kwanza au Kiingereza siku ya Kiswahili, na kwamba wengi wa wanafunzi huzungumza Lugha ya Mama iwapo mwalimu hayupo. Hakuna mwanafunzi aliyekiri 'kutoizingatia sera ya lugha hata kidogo'.

Wakieleza utekelezaji wa sera ya lugha shuleni, walimu katika shule E walithibitisha waliyoyaripoti wanafunzi wao kwa kueleza kuwa 'hauna mafanikio makubwa'. Hali hii waliihusisha na hali kwamba wanafunzi hawakujibiki na walipenda kufuatwa ili watumie lugha husika na kwamba ushirikiano kati ya walimu na utawala wa shule haukuwepo.

Ijapokuwa wanafunzi katika shule E walikiuka sera ya lugha kwa kuzungumza Lugha ya Mama, hakuna aliyeipendekeza kuwa lugha ya mawasiliano shuleni. 45% walipendelea Kiingereza kwa sababu mitihani mingi hutungwa na kujibiwa kwa Kiingereza, kwamba masomo mengi hufundishwa kwa Kiingereza na baadhi yao wakatoa kisababu kwamba hawajui kuzungumza Kiswahili. Hata hivyo, 55% walipendekeza Kiswahili kwa kuwa ni lugha ya taifa ambayo inafaa kuwa fahari ya kila mkenya mzalendo na kwamba ni lugha ya matumizi mapana zaidi sio tu shuleni bali katika nchi nzima na kimataifa vievile. Hakuna aliyependekeza matumizi ya Sheng shuleni.

Jedwali 14 Uzingatiaji wa Sera ya Lugha Shuleni

Shule	**A**		**B**		**C**		**D**		**E**		**Jumla**	
Kigezo	N	%	N	%	N	%	N	%	N	%	N	%
Vizuri sana	02	10	04	20	--	--	05	25	04	20	15	18.8
Vizuri	06	30	09	45	--	--	05	25	06	30	26	32.5
Siizingatii Vizuri sana	10	50	07	35	--	--	10	50	10	50	37	46.2
Siizingatii hata kidogo	02	10	00	00	--	--	00	00	00	00	02	2.5
Jumla	20	100	20	100	--	--	20	100	20	100	80	100

Jedwali 15 Lugha Zilizopendekezwa kwa Mawasiliano Shuleni

Shule	**A**		**B**		**C**		**D**		**E**	
Lugha	N	%	N	%	N	%	N	%	N	%
Kiingereza	06	30	06	30	16	80	03	15	09	45
Kiswahili	11	55	03	15	02	10	05	25	11	55
Kiingereza na Kiswahili	02	10	10	50	00	00	12	60	00	00
Sheng	01	05	01	05	02	10	00	00	00	00
Lugha ya Mama	00	00	00	00	00	00	00	00	00	00

Kwa jumla, kinachoibuka ni kwamba sera ya lugha katika nyingi ya shule hizi (A, D, na E) inazingatiwa 'vizuri tu' au 'haizingatiwi vizuri sana'. Shule B pekee ndiyo imeonyesha ufanisi kwa kiwango fulani (65%) – 'Vizuri sana' na 'Vizuri' pamoja. Shule C haikuona haja ya kuwa na sera kama hii na labda hiyo ndiyo sera yake, yaani wanafunzi watumie ama Kiingereza, Kifaransa au Kiswahili bila kujifunga katika mikatale ya wakati au siku.

4.3.0 Uzungumzi wa Wanafunzi

Kutokana na ukweli kwamba sera ya lugha haizingatiwi katika takriban shule zote, tulitaka kujua kilichowapatia wanafunzi msukumo kutaka kujifunza Kiswahili na kutaka

kukizungumza. Tulitekeleza hili kwa kutafuta habari kuhusu umilisi wa wanafunzi kutumia lugha zungumzi ya Kiswahili, motisha wa kuitumia, manufaa ya kuwa na umilisi kwayo, juhudi za uhamasishaji na hatimaye hali ya lugha zungumzi katika mitihani ya kitaifa.

4.3 1 Umilisi wa Kutumia Lugha Zungumzi ya Kiswahili

Kupitia kwa hojaji na mahojiano, walimu waliulizwa kueleza iwapo walidhani matumizi ya lugha ya wanafunzi wao yaliathiri uzungumzi wao wa lugha zungumzi ya Kiswahili. Walimu wote (100%) katika shule zote tano zilizochunguzwa walikubaliana kuwa kulikuwa na uhusiano wa moja kwa moja kati ya ruwaza za matumizi ya lugha na lugha zungumzi fasaha ya Kiswahili. Wote walielekea kukubaliana kwamba iwapo wanafunzi wangejihusisha zaidi katika shughuli za kimtagusano katika sehemu mbalimbali za maingiliano shuleni kwa kutumia Kiswahili, basi wangekimudu na kukithibiti zaidi kimazungumzo - jambo ambalo walisema haliko sasa.

Huku wakigeza umilisi wa wanafunzi wao katika kutumia lugha zungumzi ya Kiswahili kwenye kipimo cha viwango vinne, walimu katika shule A walieleza wanafunzi wao kuwa 'wanazungumza kwa ufasaha wastani'. Hili walisema ni kwa sababu matumizi yao ya Kiswahili ni ya kiwango cha chini. Jambo ambalo walisema linaathiri ufasaha wa lugha hasa matamshi, umilisi wake na matokeo ya mitihani.

Umilisi wa wanafunzi katika shule B uligezwa kuwa: 'hawana ufasaha katika mazungumzo'. Hili, walimu walieleza, ni kwa sababu ama ni waoga kuzungumza Kiswahili au wanafunzi wana mazoea ya kutumia lugha vibaya na hivyo ikawa vigumu kwao kujifunza lugha zungumzi fasaha.

Umilisi wa kutumia lugha zungumzi ya Kiswahili wa wanafunzi katika shule C ulielezwa kwa maneno: 'wanazungumza kwa ufasaha wastani'. Ruwaza za uzungumzi wao ziliathiri umilisi wao wa lugha zungumzi ya Kiswahili kwa sababu wengi walisemwa kuandika kwa

kutegemea jinsi walivyozungumza lugha yenyewe. Aidha, walisemekana kutumia mùda wao mwingi kuzungumza Kiingereza na Sheng na hivyo kudumaza ufasaha wao wa Kiswahili sanifu.

Wanafunzi katika shule D waligezwa kuwa: 'wanazungumza kwa ufasaha wastani' na walimu wao. Walieleza kuwa matumizi yao ya lugha yaliathiri umilisi wao katika Kiswahili kwa sababu walielekea kunasibisha sarufi ya Lugha ya Mama na ile ya Kiswahili kwa kutozoea kutumia Kiswahili katika mazungumzo yao.

Kwa upande wao, wanafunzi wa shule E walielezwa kuwa 'hawana ufasaha katika mazungumzo'. Hali hii ilishtakiwa kutokana na wanafunzi ama kujizoesha kuzungumza Lugha ya Mama au kutumia sarufi iliyopotoshwa na athari za lugha nyingi zingine wanazotumia zaidi na hivyo kuathiri umilisi wao wa lugha zungumzi ya Kiswahili ambayo waliitumia kwa nadra sana.

4.3.2 Motisha wa Kutumia Kiswahili

Sababu au hali fulani humpa mtu ilhamu na mshawasha wa kutaka kutenda jambo. Msukumo wa aina hii ndio hujulikana kama motisha. Kama njia moja ya kueleza motisha wa wanafunzi kuzungumza Kiswahili, waliulizwa kueleza iwapo kuna manufaa ya kuwa na umilisi wa kutumia lugha zungumzi fasaha ya Kiswahili. Jambo hili lilitokana na uhalisia kuwa stadi ya kuzungumza haikutahiniwa katika mitihani ya kitaifa, jambo ambalo lingewafanya kutoitilia maanani.

Idadi kubwa (84%) ya wanafunzi katika shule zote zilizochunguzwa walikubaliana kuwa kulikuwa na manufaa ya kuwa na umilisi wa lugha zungumzi ya Kiswahili. Hata hivyo, idadi ndogo (16%) hawakuona umuhimu wa kuwa na stadi hii kama inavyoonyeshwa katika Jedwali 16 hapa chini.

Jedwali 16 Manufaa ya Kuwa na Umilisi Kutumia Lugha Zungumzi ya Kiswahili

Shule	Kuna Manufaa		Hakuna Manufaa	
	N	%	N	%
A	15	75	05	25
B	19	95	01	05
C	13	65	07	35
D	20	100	00	00
E	17	85	03	15
Jumla	**84**	**84**	**16**	**16**

Katika ufafanuzi wao, watafitiwa walitaja manufaa haya kuwa: kuweza kuwasiliana kwa ufasaha na makabila mbalimbali, ni dhihirisho la uzalendo wa mhusika kwa sababu Kiswahili ni Lugha ya Taifa, ni njia ya kumpa mwanafunzi uwezo wa kufanya vizuri katika sarufi pia, humwezesha mtu kupata fahari itokanayo na ugwiji/ulumbi, ni njia moja ya kukikuza na kukionea fahari Kiswahili, kwamba ni njia ya kumwezesha mzungumzaji kupata ajira na ni sehemu ya kivutio cha watalii - upekee wa wakenya na taifa lao.

4.3.3 Uhamasishaji

Moja kati ya nyenzo bora za kuwafanya wanafunzi waienzi na kuionea fahari lugha yoyote ile ni kupitia kwa uhamasishaji wa mara kwa mara. Hili linaweza kutendeka iwapo wanafunzi watapata habari mpya, masuala ibuka na maendeleo kuhusu lugha husika. Kufuatia hili, walimu waliulizwa kugeza juhudi zao katika kuwahamasisha wanafunzi wao kuhusu umuhimu na manufaa ya lugha ya Kiswahili kwao sasa na katika siku za usoni. Walifanya hivyo kwa kuzingatia viwango vinne muhimu – 'mara kwa mara', 'mara moja moja', 'kwa nadra sana' na 'la hasha'.

Walimu katika shule zote walikiri kuwa wanafunzi wao ama wanafahamu 'vizuri' au 'vizuri sana' umuhimu wa lugha ya Kiswahili. Hili, walishikilia, lilitokana na juhudi zao za kuwahamasisha wanafunzi . Waliripoti kuwafahamisha habari kuhusu Kiswahili ama 'mara kwa mara' au 'mara moja moja'. Hata hivyo, juhudi zao katika kuwahusisha wanafunzi katika shughuli za kimtagusano kama vile mazungumzo, dayalojia, michezo ya lugha, hotuba, michezo ya kuigiza na mijadala kwenye miktadha na mazingira yanayoakisi hali halisi zilikuwa ndogo mno - jambo ambalo lilipunguza nafasi kwa wanafunzi kujieleza katika lugha zungumzi ya Kiswahili. Hali hii ilibainika hasa katika shule E na B.

4.3.5 Lugha Zungumzi Katika Mitihani ya Kitaifa

Mtihani wowote uwao ule hufanywa ili kupima kiwango cha kufaulu kwa mtalaa katika kuyaafikia malengo ya elimu husika. Ni dhahiri kwamba stadi ya kuzungumza, japo inafundishwa kuanzia kidato cha kwanza hadi cha nne, haitahiniwi katika mtihani wa kitaifa (KCSE). Hali hii ilithibitishwa na walimu wote walioshiriki katika uchunguzi huu.

Hali hii ilielekea kudumaza juhudi za kuafikiwa kwa malengo ya stadi za 'Kusikiliza' na 'Kuzungumza' katika mtalaa wa Kiswahili. Ni katika msingi huu ambapo walimu, kama watekelezaji wa mtalaa wenyewe nyanjani, waliulizwa kutoa maoni yao kuhusu uwezekano wa hali hii ya kutotahiniwa kwa stadi za 'Kusikiliza' na 'Kuzungumza' katika mitihani ya kitaifa kuwa kikwazo kwa umilisi wa lugha zungumzi fasaha ya Kiswahili.

Walimu wote (100%) walieleza kuwa kutotahiniwa kwa lugha zungumzi katika mitihani ya kitaifa kulifanya stadi hii isitiliwe maanani sio tu na walimu pekee yao bali na wanafunzi pia. Hata hivyo, ni jambo la kushusha moyo kutambua kwamba walimu na wanafunzi hupuuzilia mbali stadi na mada ambazo hazitahiniwi moja kwa moja katika mitihani ya kitaifa japo ziko katika mtalaa.

Kwa hivyo, kinachoibuka hapa ni kwamba ipo haja ya kushughulikia tatizo la ukosefu wa umilisi wa lugha zungumzi miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili. Njia moja ya kufanya hivyo, yaelekea, ni kutahini stadi za 'Kusikiliza' na 'Kuzungumza' katika mitihani ya kitaifa.

4.4 Athari za Matumizi ya Lugha Zungumzi kwa Matamshi Fasaha ya Kiswahili

Ruwaza mahsusi za matumizi ya lugha zungumzi katika kila shule zimebainishwa katika sehemu iliyotangulia. Maelezo yametolewa kufafanua yaliyomo katika majedwali na misambao ya umaratokezi. Sehemu hii, kwa hivyo, inahusisha matokeo haya na matokeo katika Mjarabu na Mijadala.

4.4.1 Tathmini ya Matamshi ya Wanafunzi

Tathmini ni hali ya kupima utendaji wa jambo fulani. Ni sehemu muhimu katika utekelezaji wa mtalaa wowote ule. Inapofanywa, tathmini huwa imenuiwa kupima iwapo stadi au mada imekamilika au shabaha imetimizwa. Humjuza mtathmini juu ya kufaulu na kutofaulu kwa stadi au mada yake pamoja na ubora wa nyenzo alizozitumia.

Kutuwezesha kueleza athari za ruwaza za matumizi ya lugha kwa matamshi ya wanafunzi wa shule za upili, Mjarabu pamoja na Mijadala iliandaliwa. Tulifanya hili ili kupima kiwango cha umilisi wa lugha zungumzi kimatamshi cha wanafunzi katika kila shule. Kipimo cha wastani wa kihesabu kilitumiwa kuainisha umilisi kimatamshi.

Alama za wanafunzi zilipewa thamani kutegemea usahihi wa matamshi mintarafu ya mfumo wa uainishaji wa usahihi wa matamshi (Kiambatisho E) uliokuwa umeandaliwa awali. Alama kati ya 00 - 29 iliwakilisha 'Matamshi finyu mno'; 30 - 44 'Matamshi dhaifu'; 45 - 59 'Matamshi wastani'; 60 - 74 'Matamshi mazuri' 75 - 100 'Matamshi mazuri sana'.

4.4.2 Mjarabu

Wanafunzi ishirini kutoka kila shule walioshiriki katika uchunguzi huu walifanya Mjarabu (rejelea Kiambatisho C). Mjarabu wenyewe ulilenga kutathmini umilisi wao wa matamshi fasaha ya Kiswahili sanifu. Mjarabu huu ulikuwa na sehemu mbili kuu, yaani A na B. Watahiniwa walihitajika kujibu maswali yote.

Watahiniwa walijibu maswali katika sehemu A kwa kuchagua neno moja, kati yà mawili au matatu, lililowakilisha matamshi sahihi kujazia pengo katika kila sentensi. Maswali katika sehemu hii yalituzwa jumla ya alama 45 ambazo ziliwasilishwa kwa asilimia (%). Baada ya kusahihishwa, hata hivyo, wanafunzi katika takriban shule zote walipata alama za juu katika sehemu hii. Alama za wastani wa kihesabu kwa kila shule zilikuwa: shule A 87.15%, shule B 89.0%, shule C 93.2%, shule D 89.1% na shule E 78.0%, yaani 'Matamshi mazuri sana' katika shule zote. Hali hii ilitokana na uwezekano wa wanafunzi kubahatisha na kupata jibu sahihi. Kwa hivyo, tathmini ya sehemu hii haikutoa picha halisi ya umilisi wa lugha zungumzi ya Kiswahili miongoni mwa watahiniwa. Hili lilimlazimu mtafiti kuegemea sehemu B kugeza umilisi wa wanafunzi kimatamshi.

Maswali katika Sehemu ya B yalimtaka mtahiniwa kutofautisha sentensi zilizokuwa na maneno yenye sauti zilizokanganya; kueleza tofauti za kimaana zitokanazo na matamshi ya maneno waliyopewa; kuandika upya sentensi ambazo ni zao la matamshi mabaya ili zisheheni matamshi sahihi na fasaha; na kutunga sentensi mbili kwa kila jozi ya maneno ili kuyatofautisha kimatamshi. Wanafunzi walituzwa jumla ya alama 55 zilizowasilishwa kwa asilimia. Tathmini ya sehemu hii ilitokea kuwa kigezo mwafaka cha umilisi wa lugha zungumzi ya Kiswahili kimatamshi kwa sababu haikutoa nafasi kwa mtahiniwa kubahatisha jawabu. Mtahiniwa alilazimika kujieleza na kuonyesha umilisi wake. Matokeo haya yamewasilishwa hapa chini katika Jedwali 17 (a) - (e).

Jedwali 17 (a) - (e) Matokeo ya Mjarabu

(a) Shule A

Alama	f	x	fx
60 – 69	03	64.5	193.50
50 – 59	04	54.5	218.00
40 – 49	03	44.5	133.50
30 – 39	04	34.5	138.00
20 – 29	03	24.5	73.50
10 – 19	03	14.5	43.50
	∑f 20		∑fx 800

Kutokana na msambao wa umaratokezi (a), alama ya wastani ya wanafunzi katika shule A ilikuwa 40.0%, yaani kiwango cha D+. alama hii, kwa mujibu wa mfumo wa uainishaji wa matamshi inamaanisha kuwa wanafunzi hawa wana 'matamshi dhaifu' hasa ikizingatiwa kwamba wengi wao (65%) wana alama chini ya 50%.

(b) Shule B

Alama	f	x	fx
60 – 69	03	64.5	193.50
50 – 59	02	54.5	109.00
40 – 49	05	44.5	222.50
30 – 39	07	34.5	241.50
20 – 29	01	24.5	24.50
10 – 19	01	14.5	14.50
00 – 09	01	04.5	04.50
	∑f 20		∑fx 810

Msambao wa umaratokezi (b) unaonyesha kuwa wanafunzi katika shule B walipata alama ya wastani ya 40.5%, katika kiwango cha D+ yaani 'matamshi dhaifu'. Sehemu yao kubwa (75%) walipata chini ya alama 50%.

(c) Shule C

Alama	f	x	fx
80 – 89	02	84.50	169.00
70 – 79	04	74.50	298.00
60 – 69	08	64.50	516.00
50 – 59	03	54.50	163.50
40 – 49	02	44.50	89.00
30 – 39	00	34.50	00.00
20 – 29	01	24.50	24.50
	∑f 20		∑fx 1260

Katika msambao wa umaratokezi (c) hapo juu, ni bayana kuwa wanafunzi katika shule C walipata alama ya wastani ya 63.0%, katika kiwango cha B- yaani wana 'Matamshi Mazuri'. Wengi miongoni mwao (70%) walipata zaidi ya alama 50%.

(d) Shule D

Alama	f	x	fx
70 – 79	01	74.50	74.50
60 – 69	07	64.50	451.50
50 – 59	08	54.50	436.00
40 – 49	03	44.50	133.50
30 – 39	01	34.50	34.50
	∑f 20		∑fx 1130

Wanafunzi wa shule D walipata alama ya wastani ya 56.5%, katika kiwango cha C+. Matamshi yao, kwa hivyo, yaligezwa kuwa 'Matamshi Wastani'. Hili lilitokana na sababu kuwa idadi kubwa (80%) miongoni mwao walipata zaidi ya alama 50%.

(e) Shule E

Alama	f	x	fx
70 – 79	01	74.5	74.50
60 – 69	01	64.5	64.50
50 – 59	01	54.5	54.50
40 – 49	05	44.5	222.50
30 – 39	06	34.5	207.00
20 – 29	03	24.5	73.50
10 – 19	03	14.5	43.50
	∑f 20		∑fx 740

Hatimaye wanafunzi wa shule E waligezwa kuwa na alama ya wastani ya 37.0%, iliyojumuishwa katika kiwango cha D yaani wengi wao walipatikana kuwa na 'Matamshi Dhaifu'. Isitoshe, 85% walipatikana kuwa na alama chini ya 50%.

Kwa jumla shule A, B na E zilipatikana kuwa na 'matamshi dhaifu'. Shule C pekee ndiyo iliyokuwa na 'matamshi mazuri'. Shule D kwa upande wake ilipatikana kuwa na 'matamshi wastani'. Hakuna shule iliyogezwa kuwa na 'Matamshi mazuri sana' wala 'Matamshi finyu mno'. Ili kuthibitisha tathmini hii, mtafiti alitumia kifaa cha pili – Mijadala, kuona iwapo utofauti ungejitokeza.

4.4.3 Mijadala

Mjadala ni namna ya mazungumzo ambayo yanaegemea katika mashindano baina ya watu au makundi mbalimbali ya watu. Kwa njia ya mjadala kama huu, mtafiti alipima ufasaha wa wanafunzi wa kujieleza, ukakamavu wao kuzungumza na matumizi yao ya lugha sahihi kimatamshi. Hatimaye alitoa uamuzi.

Kwa ushirikiano na walimu wa Kiswahili, wanafunzi wa kidato cha tatu walitayarishwa kwa mijadala. Wanafunzi waligawanywa katika makundi mawili, moja la kuunga mkono na lingine la kupinga. Walipewa mada ya mjadala, yaani *'Athari za Dawa za Kulevya'* siku mbili kabla ya mjadala wenyewe. Kutokana na mijadala hii, wanafunzi walitoa hoja zao kwa mawazo yaliyofululiza kwa uhalisia wake na hivyo kumwezesha mtafiti kukadiria umilisi wa lugha wa wanafunzi katika Kiswahili zungumzi.

Kila mzungumzi alipewa fursa ya dakika tano kuchangia mjadala kwa kupinga au kuunga mkono. Kila upande uliwakilishwa na washiriki kumi. Mazungumzo yalinaswa kwa kinasa sauti. Kutokana na mazungumzo haya, kuwepo au ukosefu wa makosa ya kimatamshi miongoni mwa wanafunzi ishirini kuliainishwa. Kuwepo au kutokuwepo kwa makosa haya kulitumiwa kuthibitisha athari za ruwaza za matumizi ya lugha kwa umilisi wa lugha zungumzi ya Kiswahili kimatamshi.

Kati ya washiriki ishirini kila mmoja aliichangia shule yake alama tano. Kila kosa la kimatamshi lililofanywa lilipunguza alama hizi kwa nusu alama hadi makosa kumi. Hata hivyo, utafiti huu haukujishughulisha na kueleza aina ya kosa lenyewe la matamshi. Kwa mfano, mwanafunzi aliyefanya makosa nane alipoteza alama nne na kuchangia shule yake alama moja. Misambao ya umaratokezi (Jedwali 18 (a) - (e)) inaonyesha idadi ya makosa ya kimatamshi yaliyofanywa na wanafunzi katika kila shule. Kutokana na makosa haya, alama walizopata ziliweza kubainishwa.

Jedwali 18 (a) - (e) Makosa ya Kimatamshi Yaliyotokana na Mijadala

(a) Shule A

Makosa (x)	f	fx	fx/2
09	02	18	9.0
08	03	24	12.0
07	05	35	17.5
06	03	18	9.0
05	03	15	7.5
04	03	12	6.0
03	01	03	1.5
	∑f 20	∑fx 125	62.5

Katika michango yao iliyoainishwa katika msambao wa umaratokezi (a), wanafunzi wa shule A walifanya wastani wa makosa 6.25 ya kimatamshi kila mmoja. Hili liliwapelekea kupoteza jumla ya alama -62.5% na hivyo kuchangia shule yao alama 37.5% katika kiwango cha D yaani wana 'matamshi dhaifu'.

(b) Shule B

Makosa (x)	f	fx	fx/2
10	01	10	05
09	00	00	00
08	04	32	16
07	04	28	14
06	06	36	18
05	00	00	00
04	02	08	04
03	02	06	03
02	01	02	01
	∑f 20	∑fx 122	61

Michango ya wanafunzi wa shule B iliyoainishwa katika msambao wa umaratokezi (b) inaonyesha walifanya wastani wa makosa 6.1 ya kimatamshi kila mmoja. Hali hii iliwafanya kupoteza jumla ya alama -61.0% na hivyo kuchangia shule yao alama 39% katika kiwango cha D kwa maana kuwa wana 'matamshi dhaifu'.

(c) Shule C

Makosa (x)	**f**	**fx**	**fx/2**
06	01	06	3.0
05	03	15	7.5
04	00	00	00
03	09	27	13.5
02	05	10	5.0
01	01	01	0.5
00	01	00	00
	∑f 20	∑fx 59	29.5

Wanafunzi wa shule C, katika michango yao iliyoainishwa katika msambao wa umaratokezi (c), walifanya wastani wa makosa 2.95 ya kimatamshi kila mmoja. Hii ni idadi ndogo ya makosa ikilinganishwa na shule zingine. Hata hivyo, hali hii iliwafanya kupoteza jumla ya alama -29.5% na hivyo kuchangia shule yao alama 70.5% katika kiwango cha B+. alama hii ilimaanisha kuwa wana 'matamshi mazuri'.

(d) Shule D

Makosa (x)	**f**	**fx**	**fx/2**
06	03	18	9.0
05	06	30	15.0
04	04	16	8.0
03	05	15	7.5
02	02	04	2.0
	∑f 20	∑fx 83	41.5

Kwa upande wao, wanafunzi katika shule D wakitoa michango yao katika mjadala, walifanya wastani wa makosa 4.15 ya kimatamshi kila mmoja. Kwa kufanya hivyo, walipoteza jumla ya alama -41.5% na hivyo kuchangia shule yao alama 58.5% katika kiwango cha C+ kwa maana kuwa wana 'matamshi Wastani'.

(e) Shule E

Makosa (x)	**f**	**fx**	**fx/2**
10	01	10	5.0
09	02	18	9.0
08	03	24	12.0
07	05	35	17.5
06	04	24	12.0
05	02	10	5.0
04	02	08	4.0
03	00	00	00
02	00	00	00
01	01	01	0.5
	∑f 20	∑fx 130	65

Michango ya wanafunzi wa shule E, iliyoainishwa katika msambao wa umaratokezi (e), inaonyesha kuwa walifanya wastani wa makosa 6.5 ya kimatamshi kila mmoja. Makosa haya yaliwafanya kupoteza jumla ya alama -65.0% huku wakichangia shule yao alama 35% katika kiwango cha D. Hili lilipelekea matamshi yao kugezwa kuwa 'matamshi dhaifu'.

Ni dhahiri kuwa tathmini za vifaa hivi viwili – Mjarabu na Mijadala zinapima umilisi lugha zungumzi ya Kiswahili kimatamshi kwa njia inayoonyesha uhusiano wa moja kwa moja.

4.5 Majadiliano

Msingi wa majadiliano ya uchunguzi huu ni matokeo ambayo tumeyawasilisha katika sehemu iliyotangulia hapo juu. Majadiliano na ufafanuzi wenyewe umefanywa kwa kuzingatia mada zifuatazo: Jumla ya lugha za wanafunzi na walimu, lugha katika mawanda mbalimbali, matumizi ya lugha nyumbani, lugha ya usomaji wa magazeti na usikilizaji wa redio, lugha ya uandishi wa barua, matumizi ya lugha shuleni, uzungumzi wa wanafunzi, na athari za matumizi ya lugha zungumzi kwa matamshi fasaha ya Kiswahili. Mada hizi zimejadiliwa mintarafu maandiko na tafiti za awali tulizohakiki katika sura ya pili. Isitoshe, deta zilizopatikana kupitia kwa uchunguzi shiriki zimejadiliwa na kufafanuliwa kama ithibiti za ziada.

4.5.1 Jumla ya Lugha za Wanafunzi na Walimu

Lugha azijuazo mtu hutawala matumizi yake ya lugha. Mtu aliyejifunza lugha zaidi ya moja mara nyingi huchanganya ndimi au kuchupia ndimi anapozungumza. Halikadhalika, kuna wale wanaozungumza kwa lugha, labda Kiswahili, kisha hapa na pale, wakaingiza sentensi au msamiati wa lugha nyingine. Kwa hivyo, kutuwezesha kujadili ruwaza za matumizi ya lugha zungumzi, ilitulazimu kueleza jumla ya lugha wazijuazo wanafunzi pamoja na walimu wao.

Matokeo kuhusu jumla ya lugha ambazo wanafunzi na walimu wanazijua na kuzitumia yalionyesha kuwa wengi wao walitumia lugha tatu – Kiswahili, Kiingereza na Lugha yà uzawa. Hali hii inalandana mno na ya wakenya wengi ambao hutumia lugha tatu kama ilivyobainishwa katika tafiti za awali (Gorman, 1974; Chimerah, 2000; Beja, 2001). Wanafunzi waliodai kutumia lugha nne walitaja Sheng kuwa ya nne. Ni dhahiri kuwa Sheng imeanza kukita mizizi kimatumizi katika shule za shamba ambako sampuli yetu ilitekwa.

Wanafunzi wengi walioshiriki katika uchuguzi huu walizungumza Lugha ya Kwanza moja – Dholuo. Kama tulivyoeleza, hali hii ilitokana na uhalisia kwamba wanafunzi wengi

katika shule za kutwa ni wakazi na wazawa wa viunga vya shule husika. Hata hivyo, wachache miongoni mwao walitumia kati ya Lunyole, Luloogoli, Kikamba, Kikisii, Gikuyu na Kinandi kama Lugha ya Kwanza.

Matumizi ya lugha ya walimu kumi yalichunguzwa ili kuthibitisha iwapo yaliathiri na kuhusiana na yale ya wanafunzi wao. Takriban walimu wote waliokamilisha hojaji waliripoti kujua na kutumia lugha tatu; wengi wao wakiwa na Lugha ya Kwanza sawa na ya wanafunzi wao. Wote walizungumza Kiingereza na Kiswahili. Idadi kubwa ilitumia Dholuo kama Lugha ya Kwanza huku Lutsotso, Lumarachi, Lunyole na Lulogooli zikizungumzwa na mmoja au wawili tu.

Walimu wengi katika shule zote zilizochunguzwa walisikika na kuonekana kwingi wakitumia Lugha ya Kwanza – Dholuo - katika mazungumzo baina yao. Hali hii iliwanyima fursa muhimu kuwa viigwa bora vya matumizi ya Kiswahili na Kiingereza kwa wanafunzi wao. Mijadala mikali kuhusu mada mbalimbali pamoja na mazungumzo ya kawaida yaliweza kusikika kutoka ofisini na hata katika vyumba vya walimu. Jambo la ajabu ni kwamba ni walimu wawa hawa waliowataka wanafunzi wao watumie Kiswahili na Kiingereza pekee shuleni. Unafiki ulioje?

Kwa hivyo, ni bayana kwamba midahalo na shughuli nyingine za kimtagusano miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili wilayani Siaya zinatekelezwa katika mazingira ya wingi lugha. Kwa vile watu huzungumza lugha wanazozifahamu, ujuzi wa lugha tofauti tofauti kama huu husababisha hali ya kuchanganya ndimi au kuhamisha ndimi. Mbali na umaarufu wa Kiswahili na Kiingereza, Dholuo ni lugha muhimu katika mazungumzo ya walimu (70%) na ya wanafunzi (98%). Hata hivyo, Sheng imebainika kama lugha ya mazungumzo miongoni mwa wanafunzi (69%) wala sio walimu.

4.5.2 Lugha Katika Mawanda Mbalimbali

Matokeo kuhusu lugha zinazotumiwa na wanafunzi kwa urahisi na haraka katika mawanda mbalimbali yalibainisha Kiingereza kuwa ndiyo lugha ambayo wanafunzi wangeweza kuisoma (85%) na kuiandika (79%) kwa urahisi zaidi. Kiingereza ni somo la lazima na ndiyo lugha ya kufundishia masomo yote isipokuwa la Kiswahili. Kutokana na hali hii, marudio pamoja na kusoma kwao kwingi hutekelezwa katika Kiingereza kuliko lugha ingine.

Mazungumzo baina ya wanafunzi yalifanyika zaidi katika Sheng (31%), Dholuo (27%), Kiingereza (22%), Kiswahili (19%) na Kinandi (1%). Takwimu hizi ni ithibati kuwa wanafunzi wengi wamekuza ujuzi wao wa kuzungumza Lugha ya Mama na Sheng zaidi ya lugha ingine yoyote. Hili linaweza kuhusishwa na ukweli kwamba wanafunzi hawa wanatumia muda wao mwingi kuzungumza lugha hizi kuliko Kiswahili.

Usikilizaji ulitajwa kutekelezeka vyema zaidi katika Kiswahili (28%), Kiingereza (25%), Dholuo (25%) na Sheng (22%). Usikilizaji huu huenda unaathiriwa na lugha zitumikazo katika vyombo vya habari kama vile redio, runinga na teknolojia ya habari kwa jumla. Vyombo hivi aghalabu hutumia Kiswahili na Kiingereza. Isitoshe, walimu huzitumia lugha hizi kufundishia masomo mbalimbali shuleni mbali na kwamba ndizo *lingua franca* maarufu miongoni mwa Wakenya wengi.

Matokeo katika sehemu hii yanaweza kufafanuliwa mintarafu ya muda unaotumiwa na wanafunzi kukuza stadi mbalimbali za lugha. Kama lugha rasmi, somo la lazima na lugha ya kufundishia shuleni, wanafunzi wamekuwa wakisoma na kuandika katika Kiingereza tangu walipoanza masomo yao. Hii ndiyo sababu wanaweza kusoma na kuandika kwa urahisi zaidi katika Kiingereza kuliko lugha ingine yoyote.

Kwa upande mwingine, mazungumzo mengi hutendeka katika Lugha ya Kwanza na Sheng. Hali hii inawafanya wanafunzi waweze kuzungumza kwa urahisi na haraka sio tu Lugha

ya Kwanza pekee bali Sheng pia. Isitoshe, kutokana na mazungumzo katika lugha hizi, wanafunzi wanasikiliza wazungumzaji mahiri ambao ni viigwa bora kwao. Pakubwa, jambo hili ni zao la mazoezi yatokanayo na uteuzi na matumizi mengi ya lugha hizi katika miktadha, hali na mahali mbalimbali miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili wilayani Siaya.

4.5.3 Matumizi ya Lugha Nyumbani

Matokeo yalionyesha Dholuo (L1) na Sheng kuwa ndizo zilizokuwa lugha maarufu katika mazungumzo nyumbani. Umilisi wa wazazi wa wanafunzi hawa katika kuzungumza lugha mbalimbali ulionyesha kuathiri uteuzi na matumizi haya kwa kiwango fulani. Isitoshe, baadhi ya nyumba ziliripotiwa kuweka vikwazo kwa matumizi ya lugha nyumbani.

Maelezo kuhusu lugha katika mazungumzo nyumbani yalifanikishwa na wanafunzi kuulizwa kutaja lugha mbalimbali walizotumia mno katika mazungumzo na wazazi, ndugu na dada, marafiki jirani na wanapopiga gumzo na marafiki nje ya shule. Maelezo yao yalilinganishwa na ya sehemu ya lugha katika mawanda mbalimbali ili kuthibitisha na kuonyesha uhusiano uliokuwepo.

Kwa jumla, lugha zinazotawala midahalo ya watafitiwa nyumbani ni Dholuo (33.75%) na Sheng (34.5%). Hizi ndizo lugha ambazo walikuwa wamezitaja awali kuwa ndizo walizozizungumza kwa wepesi (yaani Sheng, 27% na Dholuo, 22%).

Kutuwezesha kufidia deta tuliyoipata kuhusu matumizi ya lugha nyumbani, wanafunzi waliulizwa kugeza umilisi wa wazazi wao katika kuzungumza Kiswahili, Kiingereza na Sheng. Kugeza huku kulidhamiriwa kuthibitisha iwapo umilisi wa wazazi katika lugha mbalimbali uliathiri uteuzi na matumizi ya lugha mbalimbali nyumbani.

Kwa jumla, matokeo yalionyesha kuwa wazazi wa watafitiwa hawakuwa na umilisi katika kuzungumza Sheng. Hali hii inatokana na uwezekano kwamba lugha hii, kimsingi,

hutumiwa na vijana katika mazungumzo kati yao ili kujitenga kimawasiliano na wazee wao (Aswani, B. na wenzake, 2006:61-62). Wazazi, kwa upande wao huiona Sheng, kama lugha ya 'kihuni' au ya vijana mitaani na ambayo haifai kutiliwa maanani. Mielekeo hasi kama hii inawapelekea kupiga vita matumizi ya Sheng nyumbani.

Wazazi wa wanafunzi hawa, hata hivyo, wana umilisi mzuri wa kuzungumza Kiswahili na Kiingereza, yaani 'vizuri sana' na 'vizuri'. Umilisi mzuri kama huu unaweza tu kuhusishwa na elimu, mielekeo yao chanya na mchango wa vyombo vya habari kama vile redio na magazeti mbali na kuingiliana kwao na watu wengine wanaozungumza Lugha za Kikabila tofauti hasa mijini na hivyo kulazimika kutumia lugha sambazi kama Kiswahili au Kiingereza. Ajabu ni kwamba lugha hizi hazikuelezwa kuteuliwa wala kutumika katika midahalo nyumbani. Jambo hili lilitusukuma kutafuta kujua iwapo kulikuwepo vikwazo katika matumizi ya lugha nyumbani.

Wanafunzi waliulizwa kueleza iwapo walikumbana na vikwazo vyovyote katika uteuzi na matumizi yao ya lugha nyumbani. Wanafunzi wengi (78%) hawakuzuiliwa wala kupingwa moja kwa moja na wazazi wao kutumia lugha fulani nyumbani. Hata hivyo, idadi ndogo ya wanafunzi (22%) walipingwa kutumia baadhi ya lugha ambazo wanazijua. Lugha ambazo hazikupendekezwa kwa matumizi nyumbani kwa wanafunzi hawa zilikuwa: Sheng (15%), Kiingereza (4%) Dholuo (L1, 2%) na lugha nyinginezo (1%). Kutopendelewa kwa Sheng nyumbani kuliripotiwa miongoni mwa watafitiwa 15 kati ya watafitiwa wote 22 waliokumbwa na vikwazo hivi. Hali hii huenda ilitokana na sababu kwamba watu wengi nyumbani na katika ujirani hawakuelewa wala kuitumia lugha ya Sheng na ndiposa haikupendekezwa.

Ingawaje wanafunzi wengi (78%) waliripoti kutotingwa katika uteuzi na matumizi yao ya lugha nyumbani, ni dhahiri kwamba kuwepo kwa washiriki katika mazungumzo wasioelewa wala kuzungumza lugha kama Kiswahili au Kiingereza kuliathiri uteuzi na matumizi yao ya lugha. Hali hii ilipelekea Lugha ya Mama kuteuliwa na kutumiwa mara nyingi nyumbani.

Matumizi ya lugha isiyoeleweka na baadhi ya watu nyumbani yalichukuliwa kama maringo, kiburi, ukaidi na ukosefu wa heshima kwao.

Kwa jumla, kuwepo kwa vikwazo kama hivi kunatinga uhuru wa uteuzi na matumizi ya lugha nyumbani. Kwa kiwango kikubwa, mazungumzo nyumbani hayatoi nafasi kwa wanafunzi kufanya mazoezi ya Kiswahili wanachojifundisha shuleni wala kuwapa viigwa bora vya matumizi fasaha katika mazingira asili na hivyo kuathiri vibaya matumizi na umilisi wa kutumia lugha zungumzi fasaha ya Kiswahili.

Hali hii inakinzana na matokeo na mapendezo ya tafiti nyingi za awali (Gakuru, 1979; Hughes, 1990 na Kathuri, 1984) ambazo zimeeleza umuhimu wa malezi na mazingira ya nyumbani kwa ujifunzaji wa lugha, hasa ya pili. Malezi ya mtu huwa muhimu sana katika matumizi yake ya lugha. Mtu aliyenyimwa nafasi ya kuongea lugha husika katika utoto wake, ataitumia lugha hiyo kwa namna tofauti na mtu aliyepewa nafasi. Aliyepewa nafasi huweza kuingiliana na lugha mapema na pana uwezekano wa mtu kama huyo kujifunza lugha na kubobea katika kuzitambua kanuni zinazotawala matumizi ya lugha.

4.5.4 Lugha ya Usomaji wa Magazeti na Usikilizaji wa Redio

Vyombo vya habari vimechukua wajibu mkubwa sana katika kueneza na kukuza lugha ya Kiswahili. Kupitia vipindi na makala mbalimbali hasa yanayolenga ustawishaji wa Kiswahili, magazeti pamoja na idhaa za redio zimekuwa mhimili wa Kiswahili nchini. Ni katika msingi huu ambapo tulitafuta kueleza nafasi ya usomaji wa magazeti na usikilizaji wa redio katika uteuzi na matumizi ya lugha miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili.

Uteuzi wa vipindi vya redio na usomaji wa magazeti ulitingwa na uhalisia kwamba vilitayarishwa katika lugha chache tu, yaani, Kiingereza na Kiswahili hasa. Aidha, uamuzi

kuhusu idhaa au gazeti litakalosomwa nyumbani au shuleni mara nyingi uliripotiwa kutekelezwa na watu wazima – walimu au wazazi wala sio wanafunzi au watoto.

Usomaji wa magazeti na majarida ulielezwa mintarafu ya lugha nne - Kiswahili, Kiingereza, Lugha ya Mama na Sheng. Matokeo haya yalilinganishwa na ripoti za wanafunzi kuhusu stadi ya kusoma katika sehemu ya 'Lugha Katika Mawanda Mbalimbali'. Wanafunzi wengi katika shule zote walieleza kusoma magazeti na mjarida ya Kiingereza mara kwa mara (85%). Usomaji katika Kiswahili uliripotiwa miongoni mwa 41% ya wanafunzi. Usomaji wa magazeti katika lugha ya Sheng uliripotiwa miongoni mwa 38% ya wanafunzi. Wengi, hata hivyo, waliripoti kusoma magazeti katika Lugha ya Mama kwa nadra sana. Ajabu ni kwamba magazeti haya, hasa ya kisiasa na kidini, yalisemekana kuwepo. Matokeo haya hayakuonyesha tofauti kubwa yalipolinganishwa na ripoti za wanafunzi kuhusu stadi ya kusoma. Wengi wao (85%) walikuwa wametaja Kiingereza kuwa lugha ambayo wangeweza kuisoma kwa urahisi na haraka zaidi.

Magazeti na majarida katika Kiingereza yalielezwa kusomwa mara kwa mara (85%). Hili linaweza kuelezwa na sababu kwamba kuna machapisho mengi katika Kiingereza yanayowafikia wanafunzi shuleni kuliko ya lugha nyingine. Isitoshe, wanafunzi wana mielekeo chanya kuhusu usomaji wa machapisho katika Kiingereza mbali na kwamba wazazi na walimu huyapendekeza pakubwa.

Uchachefu wa magazeti na majarida katika Kiswahili ni moja kati ya sababu zinazochangia usomaji mdogo (41%) wa machapisho katika Kiswahili. Magazeti maarufu ni *Taifa Leo* na *Taifa Jumapili* ambayo huchapisha habari, makala, mitihani ya majaribio, dondoo za hapa na pale na uchambuzi wa fasihi. Makala haya husisimua mbali na kukuza lugha ya mwanafunzi.

Ijapokuwa haujashika kani mno, usomaji wa magazeti yenye makala katika lugha ya Sheng kama vile, *Buzz*, *Straight Talk* na *Qz* upo. Usomaji kama huu uliripotiwa miongoni mwa 38% ya wanafunzi. Watafitiwa waliripoti kusoma magazeti katika Lugha ya Mama kwa nadra sana. Hata hivyo, magazeti kama haya yaliripotiwa kuwepo.

Hata hivyo, umuhimu wa magazeti katika kuikuza lugha husika hauwezi kupuuziliwa mbali. Lugha ya magazeti hubadilika kutegemea kinachogusiwa au kushughulikiwa na makala fulani. Makala mbalimbali, hususan ya kitaaluma, hushughulikia masuala ya kitaalam na hivyo msamiati wake hulenga mambo na dhana mbalimbali za taaluma husika. Kwa njia hiyo, lugha ya magazeti, hutalii takribani sajili zote na yaweza kuchangia na kukuza ujuzi sawa na umilisi wa lugha husika miongoni mwa wanafunzi wanaoisoma.

Watafitiwa walieleza usikilizaji wao wa vipindi vya redio katika Kiswahili, Kiingereza, Lugha ya Mama na Sheng. Maelezo yao hapa yalihusishwa na yale waliyoyatoa kuhusu stadi ya kusikiliza katika sehemu ya 'Lugha Katika Mawanda Mbalimbali'. Matokeo yalionyesha kuwa wanafunzi wengi walisikiliza vipindi vya redio katika Kiswahili kuliko Kiingereza, Sheng au Lugha ya Mama. Usikilizaji mwingi uliripotiwa kutekelezeka vyema zaidi katika Kiswahili (70%), Kiingereza (65%), Dholuo (13%) na hatimaye Sheng (37%). Kiswahili hupendelewa sio tu na idhaa nyingi bali wasikilizaji pia kwa sababu ni lugha isiyofungamanishwa wala kuhusishwa na tabaka wala kabila fulani. Lugha hii ni mwafaka sio tu kwa wazazi na wanafunzi bali kwa wasomi na wasiosoma pia.

Wanafunzi waliokiri kusikiliza vipindi vya redio katika Lugha ya Mama 'Mara kwa Mara' walikuwa wengi zaidi kuliko waliokiri kusoma magazeti na majarida kwayo. Hali hii ilitokana na umaarufu wa idhaa nyingi chipukizi ambazo zinatangaza katika lugha za Kikabila katika eneo ambamo uchunguzi wetu ulifanyika. Stesheni hizi ni kama vile: *Radio Lake Victoria, Radio Ramogi, Radio Star, West FM, Radio Simba, KBC Kisumu* na *Mulembe FM.*

Takriban stesheni zote za redio hazitilii maanani kuendeleza Kiswahili. Wanapenda tu Kiingereza. Watu wengi, wakiwemo watangazaji katika idhaa hizi – kongwe na chipukizi, hawazingatii kanuni za kisarufi na ufasaha wa Kiswahili. Hali hii inatatanisha hasa tukizingatia kuwa tafiti nyingi (Fishman, 1966; Onyango, 1990; Mukunya, 1994 na Kizito, 2002) zimeonyesha kwamba mtu akitaka kuijua lugha anafaa asome kazi mbalimbali na kusikiliza vipindi vingi vya / au katika lugha husika. Usikilizaji wa vipindi vya redio mara kwa mara katika Kiswahili fasaha unaweza kusaidia kukuza umilisi wa lugha zungumzi fasaha na hasa matamshi yake. Mbali na kukuza kiwango chake cha msamiati, mwanafunzi hujifunza matamshi na sajili mbalimbali kutokana na watangazaji au waalikwa katika vipindi mbalimbali.

4.5.5 Lugha ya Uandishi wa Barua

Kuimudu lugha ni kuiongea kwa ufasaha, kuiandika na kuitumia kwa njia mufti. Imedhihirika kwamba kujizoesha kuongea lugha fulani humwezesha mtu kuielewa pia. Isitoshe, kuisoma lugha hiyo ni kujitahidi kuifahamu zaidi. Kupitia kwa hojaji, wanafunzi walieleza lugha waliyoitumia kwa wepesi kuandika barua kwa marafiki, wazazi na 'watu wengine' wasio na uhusiano wa karibu nao. Majibu yao yalisheheni matokeo ambayo yameainishwa katika Jedwali 9 na ambayo yalihusishwa na stadi ya Kuandika katika sehemu ya 'Lugha Katika Mawanda Mbalimbali'.

Kwa jumla, ni wazi kwamba Kiingereza ndicho lugha maarufu zaidi katika mawasiliano kupitia uandishi wa barua, yaani 47% kwa marafiki, 51% kwa wazazi na 77% kwa wengine. Hali hii inaafikiana na ripoti za wanafunzi wengi ambao walikuwa wametaja Kiingereza kuwa lugha ambayo wangeweza kuiandika (79%) kwa urahisi na haraka zaidi. Sheng na Lugha ya Mama hazikujitokeza kama lugha muhimu katika fani hii.

Matumizi ya Kiingereza katika uandishi wa barua yanaelekea kuhakikisha alichosema Whiteley (1974) kwamba Kiingereza ndiyo lugha ya barua za kimapenzi miongoni mwa wanafunzi wa shule. Matumizi ya Kiingereza hapa yanaweza kuhusishwa na hadhi ya juu inayopewa lugha hii. Watu wenye uwezo wa kuandika Kiingereza kwa ufasaha hujiona bora na wenye hadhi ya juu kuliko wale wasioimudu.

Kwa mujibu wa Ongechi, N. (2003) ni watu wachache mno ambao huandika barua zao za kibinafsi katika Lugha ya Mama. Anashikilia kuwa uandishi wa barua kiasili ni mawasiliano miongoni mwa tabaka la 'wasomi' ambao hupendelea Kiingereza kuliko Kiswahili au Lugha ya Mama. Wachache wanaotumia Lugha ya Mama hufanya hivyo wanapowaandikia wazazi wao wakongwe wasiomudu Kiingereza. Kuna uwezekano mkubwa kuwa hizi pia ndizo sababu zinazowafanya wanafunzi wa shule za upili kupendelea Kiingereza katika uandishi wa nyaraka zao.

4.5.6 Matumizi ya Lugha Shuleni

Ruwaza za matumizi ya lugha shuleni zimeelezwa kwa kuzingatia habari ambazo wanafunzi walitoa kuhusu lugha ya mazungumzo na mwalimu, lugha katika miktadha mbalimbali ya maingiliano, lugha ya mazungumzo na wanafunzi kutoka shule nyingine, lugha katika majadiliano ya mada na masomo mbalimbali na sera ya lugha shuleni. Habari zilizopatikana kupitia uchunguzi shiriki pia zimetolewa kama ithibiti za ziada.

Lugha ya Kiingereza iliripotiwa kuwa nyenzo kuu ya maingiliano kati ya walimu na wanafunzi kama ilivyoainishwa katika Jedwali 10. Kimsingi, uteuzi na matumizi ya lugha ya wanafunzi yalishurutishwa na mamlaka ya mwalimu. Walimu waliathiri lugha iliyotumiwa na wanafunzi katika mzungumzo nao. Ni wazi kutokana na matumizi ya lugha ya wanafunzi katika mazingira asilia, pasipo na mwalimu, kwamba maingiliano kati yao na walimu katika Kiingereza

ni ya shida, ya kulazimisha na ya kujifanya kwingi. Mazungumzo kama haya yalipoonekana yakiendelea, pengi yalielekea kutekeleza jukumu fulani tu. Hata hivyo, ipo haja kwa walimu kuwahimiza wanafunzi kujieleza kwa ufasaha ama kwa Kiingereza au Kiswahili nyakati zote. Hali hii itasaidia kuzikuza lugha hizi zote kwa pamoja kimazungumzo.

Majibu ya wanafunzi kuhusu lugha waliyotarajia kutumia katika mazungumzo na wanafunzi kutoka shule ingine yalitofautiana kutoka shule moja hadi nyingine kama inavyobainishwa na Jedwali 11. Hata hivyo, watafitiwa wengi (46%) waliripoti kutumia Sheng katika mazungumzo na wenzao kutoka shule ingine. 23% walitaja Kiingereza, 17% Kiswahili na 12% wakataja mseto wa Kiswahili na Kiingereza.

Umaarufu wa Sheng miongoni mwa vijana wa shule za upili, kwa mujibu wa Aswani, B na wenzake (2006: 61-62), unatokana na sababu kwamba wanaitumia kama chombo cha kujitambulisha kama vijana wa kisasa. Wanashikilia kuwa Sheng inaonyesha namna vijana hawajaridhishwa na uhusiano walio nao na asasi za uongozi - asasi wanazohisi zimewaweka pembeni. Kwa hivyo, wanawasiliana kwa kuficha maana. Wanapoongea Sheng, vijana wanaonyesha umoja wao wa kimtazamo na kimwelekeo. Uwezo wa kuzungumza Sheng unakuwa dhihirisho kwamba msemaji ni mmoja wao. Sheng ni njia ya kujihami na kujitenga na watu wazima.

Kubadilika kwa mada au somo huathiri uteuzi na matumizi ya lugha katika miktadha isiyo rasmi. Maelezo kuhusu hali hii yalifanikishwa kwa watafitiwa kutaja ni lugha ipi waliyotarajia kutumia katika mazungumzo na majadiliano juu ya Hisbati, Kemia, Fasihi katika Kiingereza, Fasihi katika Kiswahili na Sherehe ya kitamaduni. Majibu yao yameanishwa katika Jedwali 12. Matokeo katika shule zote yakifasiriwa pamoja, masomo ya Hisbati, Kemia, na Fasihi katika Kiingereza yalielezwa kujadiliwa na wanafunzi katika Kiingereza, yaani 90%, 96% na 94% mtawalia. Somo la Fasihi katika Kiswahili nalo lilijadiliwa katika Kiswahili (99%).

Mada kuhusu sherehe ya kitamaduni zilijadiliwa pakubwa katika Lugha ya Mama (71%). Ni dhahiri kuwa, ijapokuwa matumizi ya lugha miongoni mwa wanafunzi shuleni yalifaa kuongozwa na sera ya lugha, mada au somo lililozungumziwa au kujadiliwa pia lilielekeza uteuzi na matumizi ya lugha mwafaka.

Wanafunzi walitaja lugha waliyoitumia hasa katika sehemu mbalimbali za maingiliano shuleni ili kueleza jinsi kubadilika kwa mahali kulivyoathiri uteuzi na matumizi wa lugha shuleni. Muhtasari wa matokeo haya umetolewa katika Jedwali 13. Wakieleza matumizi yao ya lugha mintarafu mahali mbalimbali shuleni, wanafunzi wa shule A (ya kutwa) walitaja kutumia Sheng zaidi ikifuatiwa na mseto wa Kiingereza na Kiswahili. Miktadha hii ikichukuliwa pamoja katika shule B (ya kutwa), Sheng ndiyo iliyotajwa kuwa lugha maarufu zaidi ikifuatiwa na Kiswahili. Majibu ya wanafunzi katika shule C na D yalionyesha umaarufu wa Sheng. Kwa jumla, Lugha ya Mama ndiyo iliyotumika zaidi katika shule E.

Katika mazingira kama haya, ni bayana kuwa uendelezaji wa lugha ya Kiswahili shuleni mwomwote unahitaji ushirikiano, kujitolea kwingi na umoja kati ya walimu na wanafunzi. Njia moja ya kutekeleza jukumu hili ni kuweka mikakati na kaida zitakazohimiza matumizi ya lugha husika. Ni kutokana na msingi huu ambapo tulitafuta kujua iwapo kulikuwa na sera yoyote ya lugha katika shule zilizochunguzwa. Hili lilifanywa kupitia kwa majibu ya wanafunzi na walimu ambao walieleza changamoto walizokabiliana nazo katika utekelezaji wa sera ya lugha husika katika shule zao. Kilichoibuka, hata hivyo, ni kwamba sera ya lugha katika shule nyingi (yaani A, D, na E) ilizingatiwa 'vizuri tu' au 'haizingatiwi vizuri sana'. Shule B pekee ndiyo iliyoonyesha ufanisi kwa kiwango fulani tu. Shule C haikuona haja ya kuwa na sera ya lugha. Huenda hii ndiyo sera yake, yaani wanafunzi watumie ama Kiingereza, Kifaranza au Kiswahili bila kujifunga katika mikatale ya wakati au siku.

Shuleni ambamo mlikuwa na sera ya lugha, ilinuiwa kuwahimiza wanafunzi kuzungumza Kiingereza na Kiswahili. Hili lilitekelezwa katika shule nyingi kwa mfumo wa kufuatilia matumizi ya lugha miongoni mwa wanafunzi. Wanafunzi waliadhibiwa kwa kupatikana wakizungumza lugha za kikabila na Sheng. Hata hivyo, ripoti za walimu wengi zilionyesha kuwa mifumo iliyotumiwa kwingi haikuwa na mafanikio makubwa. Walitaja ukosefu wa ushirikiano miongoni mwa walimu wenzao pamoja na mielekeo hasi ya wanafunzi kuwa vikwazo vikuu kwa utekelezaji wa sera ya lugha shuleni. Kutozingatiwa kwa sera ya lugha shuleni kama huku kulikuwa kumejitokeza katika tafiti za awali (Hemphill, 1974; Obura, 1991; Rukia, 1992; Kimemia, 2001; Kaniu, 2003) pia.

Kinachoibuka ni kwamba ipo haja ya walimu kujaribu kubadilisha mielekeo ya wanafunzi kuhusu lugha zungumzi ya Kiswahili kwa kuwahamasisha maradufu kuhusu umuhimu wake. Hii itakuwa nyenzo bora zaidi kuliko kutoa adhabu ili kuhimiza uzingatiaji kununi za matumizi ya lugha. Kama wakala wa mabadiliko ya kijamii, watawala wa shule pamoja na walimu wana jukumu la kufanya kila wawezalo kuyazatiti matumizi ya Kiswahili fasaha miongoni mwa wanafunzi.

4.5.7 Uzungumzi wa Wanafunzi

Uhusiano wa moja kwa moja umeelezwa kuwepo kati ya ruwaza za matumizi ya lugha na lugha zungumzi fasaha ya Kiswahili miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili wilayani Siaya. Hili ni kwa mujibu wa walimu wa Kiswahili wote katika shule tano zilizochunguzwa. Umilisi wa kutumia lugha zungumzi ya Kiswahili wa wanafunzi katika shule A, C na D ulielezwa kwa maneno: 'wanazungumza kwa ufasaha wastani' ilhali ule wa shule B na E uligezwa kuwa 'hawana ufasaha katika mazungumzo'.

Miongoni mwa sababu zilizotolewa kueleza hali hii zilikuwa: matumizi yao ya Kiswahili ni ya kiwango cha chini, ama wanafunzi ni waoga kuzungumza Kiswahili au wana mazoea ya kutumia lugha yenyewe vibaya na hivyo ni vigumu kwao kujifunza lugha zungumzi fasaha, wengi walielezwa kuiandika kwa kutegemea jinsi walivyozungumza lugha yenyewe, walitumia muda wao mwingi kuzungumza Kiingereza na Sheng na hivyo kudumaza ufasaha wao wa Kiswahili sanifu, walielekea kunasibisha sarufi ya Lugha ya Mama na ile ya Kiswahili kutokana na kuzoea kuzungumza Lugha ya Mama au kutumia sarufi iliyopotoshwa na athari za lugha nyingine wanazozitumia zaidi na hivyo kuathiri umilisi wao wa lugha zungumzi ya Kiswahili waliyoitumia kwa nadra mno.

Kuboresha matumizi ya Kiswahili kimatamshi, wanafunzi hawana budi kujihusisha zaidi katika shughuli za kimtagusano katika sehemu mbalimbali za maingiliano shuleni kwa kutumia Kiswahili fasaha. Juhudi kabambe kama hizi zitawawezesha kuimudu na kuithibiti zaidi lugha ya Kiswahili kimazungumzo. Baadhi ya sababu walizotoa walimu wa Kiswahili zimejitokeza pia katika kazi za awali (Mbaabu, 1985; 1995; Mangwa, 2004 na King'ei na Musau, 2002).

Kutokana na ukweli kwamba stadi ya 'Kuzungumza' haikuwa inatahiniwa katika mitihani ya kitaifa - jambo ambalo lingewafanya wanafunzi kutoitilia maanani. Tulitafuta kujua sababu au hali ambayo ingewapa motisha wa kutaka kuteua na kutumia Kiswahili katika mazungumzo yao. Wakichangia kuhusu manufaa ya kuwa na umilisi wa kutumia lugha zungumzi fasaha ya Kiswahili, wanafunzi wengi (84%) katika shule zote ambazo zilichunguzwa walikubali kuwa kulikuwa na natija ya kuwa na umilisi wa lugha zungumzi ya Kiswahili. Ni idadi ndogo tu (16%) ambao hawakuona faida ya kuwa nao.

Wanafunzi walieleza manufaa ya kuwa na umilisi wa kuzungumza Kiswahili fasaha kuwa: kuweza kuwasiliana kwa ufasaha na makabila mbalimbali, kwamba ni dhihirisho la uzalendo wa mhusika kwa sababu Kiswahili ni Lugha ya Taifa, ni njia ya kumpa mwanafunzi

uwezo wa kufanya vizuri katika sarufi pia, humwezesha mtu kupata fahari itokanayo na ugwiji/ulumbi, ni njia moja ya kuikuza na kuionea fahari lugha ya Kiswahili, kwamba ni njia ya kumwezesha mzungumzaji kupata ajira na ni sehemu ya kivutio cha watalii - upekee wa wakenya na taifa lao, miongoni mwa manufaa mengine mengi.

Hata hivyo, maelezo haya yalielekea kupotosha kwa sababu wanafunzi wengi hawakuchangamkia matumizi fasaha ya Kiswahili kimazungumzo. Hili lilitupelekea kudadisi juhudi za walimu katika kuwahamasisha wanafunzi wao kuhusu umuhimu na manufaa ya Kiswahili. Ajabu ni kwamba walimu wote walioshirikishwa katika uchunguzi huu walishikilia kuwa wanafunzi wao ama wanafahamu 'vizuri' au 'vizuri sana' umuhimu wa lugha ya Kiswahili. Hali ambayo walieleza kuwa ilitokana na juhudi zao za kuwahamasisha. Walieleza kuwafahamisha habari kuhusu umuhimu wa Kiswahili ama 'mara kwa mara' au 'mara moja moja'.

Ijapokuwa uhamasishaji kuhusu dhima ya Kiswahili upo, maneno na maelezo matupu bila vitendo halisi hayawezi kuboresha ufasaha wa lugha zungumzi. Kwingi, juhudi za walimu wa lugha katika kuwahusisha wanafunzi katika shughuli za kimtagusano kama vile mazungumzo, dayalojia, michezo ya lugha, hotuba, michezo ya kuigiza na mijadala kwenye miktadha na mazingira yanayoakisi hali halisi ziliripotiwa kuwa ndogo mno. Jambo liloelekea kukubaliana na maoni ya Crystal (1987) kwamba wanafunzi hupata nafasi ndogo mno kujihusisha katika mazungumzo darasani. Hali hii iliwapunguzia wanafunzi nafasi za kujieleza katika lugha zungumzi fasaha ya Kiswahili.

Pingamizi ingine kwa ufanisi wa Kiswahili kimazungumzo imekuwa kutotilia maanani stadi ambazo hazitahiniwi katika mitihani ya kitaifa. Kwa muda mrefu sasa, stadi ya kuzungumza, ingawa inafundishwa kuanzia kidato cha kwanza hadi cha nne, haitahiniwi katika mtihani wa kitaifa (KCSE). Hali hii ilithibitishwa na walimu wote walioshiriki katika uchunguzi

huu. Ni jambo lisilopingika kuwa hali hii inadumaza juhudi za washika dau wote kuyaafikia malengo ya mada za 'Kusikiliza' na 'Kuzungumza' katika mtalaa wa Kiswahili.

Hata hivyo, ni jambo la kushusha moyo kutambua kwamba walimu na wanafunzi hupuuzilia mbali stadi na mada ambazo hazitahiniwi katika mitihani ya kitaifa japo zipo katika mtalaa. Walimu wote walioshiriki walieleza kuwa kutotahiniwa kwa lugha zungumzi katika mitihani ya kitaifa kulifanya stadi hii isitiliwe maanani sio tu na walimu pekee yao bali na wanafunzi pia.

Uhalisia kwamba ipo haja ya kushughulikia tatizo sugu la ukosefu wa umilisi wa lugha zungumzi miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili, ni jambo ambalo haliwezi kupuuziliwa mbali. Njia mojawapo ya kufikia lengo hili, yaelekea, ni kutahini stadi za 'Kusikiliza' na 'Kuzungumza' moja kwa moja katika mitihani ya kitaifa.

4.5.8 Athari za Matumizi ya Lugha Zungumzi kwa Matamshi Fasaha ya Kiswahili

Ruwaza mahususi za matumizi ya lugha zungumzi miongoni mwa wanafunzi katika kila shule zimebainishwa hapa kama njia moja ya kufafanua athari za matumizi ya lugha zungumzi kwa matamshi fasaha ya Kiswahili. Hili tumelifanya kwa kuhusisha ruwaza zenyewe na matokeo katika Mjarabu na Mijadala kwa mujibu wa kila shule.

Wanafunzi wengi katika shule A, ya Kutwa ya Mseto, waliteua na kutumia kati ya Kiswahili, Kiingereza, Dholuo na Sheng – lugha zilizojumuisha hazina ya lugha walizozijua. Matumizi ya lugha hizi yalisheheni ruwaza mahsusi. Dholuo ilitawala mazungumzo, usikilizaji mwingi ukafanyika katika Kiswahili ilhali kusoma na kuandika kwao kukafanyika zaidi katika Kiingereza.

Nyumbani, wanafunzi katika shule A walitumia Dholuo katika mazungumzo yao. Walisoma magazeti na majarida katika Kiingereza na kusikiliza vipindi vya redio katika Kiswahili. Uandishi wao wa barua ulifanywa katika Kiingereza.

Shuleni, walizungumza na walimu pakubwa kwa kutumia Kiingereza. Mazungumzo na wanafunzi kutoka shule zingine yalifanywa katika Sheng. Mazungumzo au majadiliano kuhusu masomo yote isipokuwa somo la Kiswahili yalifanywa katika Kiingereza. Majadiliano kuhusu mada zingine za kawaida yalifanywa katika Dholuo. Ingawa walidai kutumia Kiswahili na Kiingereza katika mahali na miktadha mbalimbali shuleni, walikiri kutozingatia sera ya lugha japo ilikuwepo. Walielezwa na walimu wao kuwa walizungumza kwa ufasaha wastani kwa sababu matumizi yao ya Kiswahili yalikuwa hafifu na ya kiwango cha chini.

Kutokana na ruwaza zilizoibuka, ni dhahiri kuwa lugha zungumzi fasaha ya Kiswahili haikuchukua nafasi kubwa katika shughuli za kimtagusano za wanafunzi katika shule A. Kwa hivyo, hali hii inaweza kulaumiwa kuathiri vibaya matamshi katika Kiswahili sanifu. Hili limebainika katika tathmini za matamshi yao. Katika Mjarabu walipata alama ya wastani ya 40% ambayo ni ya kiwango sawa na ile waliyoipata katika katika kuchangia kwao katika Mjadala, walipata 37.5% katika kiwango cha D kumaanisha kuwa walikuwa na 'matamshi dhaifu'. Kwa jumla matamshi ya wanafunzi katika shule A yalipatikana kuwa dhaifu.

Shule B, ambayo ni ya Kutwa ya Mseto, kwa upande wake ilikuwa na wanafunzi walioweza kuzungumza Dholuo (L1), Kiswahili, Kiingereza na Sheng. Walieleza kuzungumza na kusikiliza vizuri zaidi Dholuo ilhali walisoma na kuandika kwa urahisi zaidi katika Kiingereza.

Nyumbani, Dholuo ilipewa nafasi kubwa zaidi katika mazungumzo yote yaliyofanyika. Walisoma magazeti na majarida mara kwa mara katika kiingereza huku usikilizaji wao wa

vipindi vya redio ukifanyika mara kwa mara katika Kiswahili. Hata hivyo, barua zao nyingi ziliandikwa katika Kiingereza.

Shuleni, mazungumzo mengi kati yao na walimu yalifanyika katika Kiingereza, hali ambayo ilitofautiana na mazungumzo kati yao na wanafunzi kutoka shule zingine ambao walizungumziwa Sheng. Walijadiliana mada zilizohusu masomo yote katika Kiingereza isipokuwa somo la Kiswahili ambalo lililazimu matumizi ya Kiswahili. Mada za kiutamaduni au zisizohusiana na shughuli za kiusomi zilijadiliwa pakubwa katika Dholuo. Ijapokuwa ni kosa la kujumlisha kueleza kuwa ni lugha moja inayotumiwa mahali mbalimbali shuleni, ni dhahiri kuwa Sheng ni maarufu mahali pengi shuleni B.

Umaarufu wa Sheng kwingi shuleni una maana kuwa kueleza kwa wanafunzi eti walizingatia sera ya lugha 'vizuri' hakuna mashiko. Hili lilithibitishwa na walimu wao waliowataja kuwa hawakuwa na ufasaha katika mazungumzo katika Kiswahili sanifu. Isitoshe, tathmini za matamshi yao katika Kiswahili sanifu zinaonyesha udhaifu wao. Walipata alama ya wastani ya 40.5% katika kiwango cha D+ yaani 'matamshi dhaifu'. Nayo michango yao katika Mjadala iliwawezesha kupata alama 39% katika kiwango cha D kwa maana kuwa wana 'matamshi dhaifu'. Kwa hivyo, matamshi yao ni dhaifu.

Watafitiwa katika shule C, ya bweni ya wasichana, waliripoti kuwa na ujuzi wa kuzungumza Kiswahili, Kiingereza, Dholuo, Kifaransa, Lulogooli, Kikisii, na Sheng. Mazungumzo mengi shuleni yalitekelezwa katika Sheng. Waliripoti kusikiza na kuelewa Sheng kwa wepesi zaidi. Walieleza kuandika na kusoma kwa wingi wakitumia Kiingereza.

Nyumbani, mazungumzo mengi yalitekelezwa kwa Sheng (58.75%). Waliripoti kusoma magazeti na majarida ya Kiingereza mara kwa mara. Vile vile walisikiza vipindi vya redio katika Kiingereza mara kwa mara. Uandishi wao wa barua kwa marafiki, wazazi na watu wengine ulitekelezwa katika Kiingereza.

Shuleni, Kiingereza kilikuwa maarufu zaidi katika mazungumzo mengi na walimu. Idadi ndogo tu (5%) iliripoti kuchanganya Kiingereza na Kiswahili huku 20% wakitumia Kiswahili hasa. Sheng na Lugha ya Mama hazikutumika katika mazungumzo na mwalimu. Katika mazungumzo na wanafunzi wenzao kutoka shule zingine, Shule C ilitaja kutumia Sheng. Majadiliano yao yasiyo rasmi kuhusu masomo yote isipokuwa Kiswahili yalifanyika hasa katika Kiingereza. Walieleza kutumia Lugha ya Mama kujadili mada kuhusu sherehe ya kitamaduni na Sheng kujadili mada nyinginezo zisizohusiana na shughuli za kiusomi. Kwa ujumla, umaarufu wa Sheng ulikuwa dhahiri katika sehemu nyingi za maingiliano shuleni. Hili huenda lilitokana na ukweli kuwa shule hii haikuwa na sera yoyote iliyoongoza matumizi ya shuleni. Hata hivyo, matumizi ya Lugha ya Kwanza hayakuwa dhahiri. Wanafunzi walielekea kuteua na kutumia kati ya Kiingereza, Kifaransa na Kiswahili, na kwa kiwango fulani Sheng.

Umilisi wao wa kutumia lugha zungumzi ya Kiswahili ulielezwa kuwa 'wanazungumza kwa ufasaha wastani'. Kwa hivyo, ruwaza za uzungumzaji wao ziliathiri umilisi wao wa lugha zungumzi ya Kiswahili kwa sababu walitumia muda wao mwingi kuzungumza Kiingereza na Sheng na hivyo kudumaza ufasaha wao wa Kiswahili sanifu. Hata hivyo, matumizi yao ya sheng kuliko Lugha ya Mama yalielekea kuboresha ufasaha wao katika Kiswahili kimatamshi. Hili limeonyeshwa na matokeo ya tathmini za matamshi yao. Walipata alama ya wastani ya 63.0% katika kiwango cha B- yaani wana 'matamshi mazuri'. Michango yao katika Mjadala ilitunukia shule yao alama 70.5% katika kiwango cha B+. Alama hii ilimaanisha kuwa wana 'matamshi mazuri'.

Shule ya bweni ya wavulana, D, ilikuwa na watafitiwa waliozungumza Kiingereza, Kiswahili, Dholuo, Sheng na Lunyole. Wanafunzi walipendelea kuzungumza Sheng. Kusikiliza kwao kwingi kulifanyika katika Kiingereza. Lugha ya kusoma na kuandika ilijitokeza kuwa Kiingereza.

Kwa jumla, lugha iliyotawala mazungumzo nyumbani ilikuwa Sheng. Walisoma magazeti na majarida katika Kiingereza mara kwa mara. Vile vile walichangamkia vipindi vya Kiingereza zaidi kuliko lugha ingine. Waliandika nyaraka zao kwa Kiingereza.

Shuleni, lugha mbili tu – Kiswahili na Kiingereza ndizo zilizotumika katika mazungumzo na mwalimu katika shule D. Waliripoti kutumia Sheng katika mazungumzo yao na wenzao kutoka shule zingine. Walieleza kutumia Kiingereza katika majadiliano yao kuhusu masomo yote isipokuwa Kiswahili. Kiswahili kilitajwa kuwa lugha ya mazungumzo kuhusu Fasihi katika Kiswahili. Hata hivyo, mazungumzo kuhusu sherehe ya kitamaduni yalielezwa kufanyika katika Lugha ya Mama. Sheng ilitawala midahalo ingine yoyote isiyohusu masomo. Sheng ndiyo lugha ambayo ilikuwa maarufu zaidi shuleni humu.

Kulikuwepo sera ya lugha katika shule D iliyolenga kuimarisha Kiingereza na Kiswahili miongoni mwa wanafunzi. Wanafunzi wengi walikiri 'kutoizingatia sera ya lugha vizuri sana'. Walieleza kuwa wakati mwingine wao hujikuta wakitumia Sheng na hata Lugha ya Mama katika mazungumzo na marafiki. Hali hii iliwafanya kugezwa kuwa 'wanazungumza kwa ufasaha wa wastani' na walimu wao. Matumizi yao ya lugha yalielezwa kuathiri umilisi wao katika Kiswahili. Walielekea kuzungumza Sheng na kutozoea kutumia Kiswahili katika mazungumzo yao.

Hata hivyo, kuzungumza Sheng kwao kulielekea kuwafaidi kwa kiwango fulani kwa sababu matokeo ya tathmini za matamshi yao ziliwaonyesha kuwa na matamshi wastani. Walipata alama ya wastani ya 56.5% katika kiwango cha C+. Wakitoa michango yao katika Mjadala, walichangia shule yao alama 58.5% katika kiwango cha C+ kwa maana kuwa wana 'Matamshi Wastani'.

Hatimaye shule E, ya Mseto iliyo na waafunzi wa kutwa na wa Bweni ilishirikisha wanafunzi waliozungumza Kiswahili, Kiingereza Sheng Kinandi, Kikisii, Gikuyu, Kikamba na

Dholuo. Wanafunzi wengi walieleza kuzungumza kwa urahisi zaidi katika Dholuo. Kusikiliza kwao kwingi vile vile kulifanyika katika Dholuo. Lugha iliyopendelewa katika shughuli zao za usomaji na uandishi ni Kiingereza.

Lugha iliyotawala mazungumzo yote ya wanafunzi hawa nyumbani ilikuwa Dholuo. Walisoma magazeti na majarida ya Kiingereza mara kwa mara na kusikiliza vipindi vya redio mara kwa mara katika Kiswahili.Waliandika barua kwa marafiki, wazazi na watu wengine wakitumia Kiingereza.

Shuleni, wanafunzi wa shule E waliripoti kutumia Kiingereza hasa katika mazungumzo na mwalimu. Walieleza kutumia Sheng katika mazungumzo yao na wenzao kutoka shule zingine. Majadiliano kuhusu masomo yote isipokuwa Kiswahili yalifanyika katika Kiingereza. Mada zilizohusu sherehe ya kitamaduni au mada nyinginezo zilizungumziwa kwa Lugha ya Mama. Kwa kiasi kikubwa, Lugha ya Mama ilitumika zaidi katika sehemu na mahali mbalimbali shuleni.

Kuwepo kwa sera ya lugha shuleni kulihakikishwa na walimu na wanafunzi. Lugha zilizopendekezwa kwa matumizi shuleni zilikuwa Kiswahili na Kiingereza. Hata hivyo, wanafunzi wengi walikiri 'kutoizingatia vizuri sana' - yaani baadhi yao walishindwa kuwasilisha ujumbe wao vyema kwa Kiswahili na Kiingereza na hivyo kutumia Lugha ya Kwanza, wengine walijikuta wamezungumza Sheng, Lugha ya Mama au hata Kiingereza siku ya Kiswahili, na kwamba wengi wao huzungumza Lugha ya Mama iwapo mwalimu hayupo.

Si ajabu kwamba wanafunzi hawa walielezwa kuwa 'hawana ufasaha katika mazungumzo' na walimu wao wa lugha. Hali hii ilielezwa kutokana na wanafunzi ama kujizoesha kuzungumza Lugha ya Mama au kutumia sarufi iliyopotoshwa na athari za lugha nyinginezo wanazozitumia zaidi na hivyo kuathiri umilisi wao wa lugha zungumzi ya Kiswahili ambayo waliitumia kwa nadra sana.

Matumizi ya lugha kama haya yaliwafanya kugezwa kuwa na alama ya wastani ya 37.0% iliyojumuishwa katika kiwango cha D yaani wengi wao walipatikana kuwa na 'matamshi dhaifu'. Katika mjadala walichangia shule yao alama 35% katika kiwango cha D. Hili lilipelekea matamshi yao kugezwa kuwa 'matamshi dhaifu'.

Kwa jumla, ruwaza za matumizi ya lugha zilizojitokeza zilionyesha ukuruba mkubwa na zile zilizobainika katika uchunguzi wa Kaniu, G. (2003). Matumizi ya Lugha ya Mama yalikuwa yamekithiri katika mawasiliano miongoni mwa wanafunzi waliotumia Lugha ya Mama moja – yaani shule A, B na E. Hata hivyo, watafitiwa katika shule C na D ambao walizungumza lugha za uzawa tofauti waliteua na kutumia Sheng mno.

Ulinganisho wa ruwaza za matumizi ya lugha na umilisi wa lugha zungumzi kimatamshi kwa kila shule ulituwezesha kufikia hitimisho kuwa wanafunzi waliogezwa kuwa na ama wana 'matamshi mazuri' au 'matamshi wastani' katika Mjarabu pamoja na Mjadala, yaani shule C na D, ni wale waliotumia ama Sheng au Kiswahili zaidi katika mazungumzo yao. Kwa upande mwingine, wale waliopatikana kuwa na matamshi dhaifu, yaani shule A, B na E, ni wale waliotumia lugha zingine- hasa ya kwanza - mbali na Kiswahili.

4.6 Hitimisho

Katika sura hii tumeeleza ruwaza za matumizi ya lugha miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili wilayani Siaya. Tumeonyesha hali ya uzungumzi wao na kubainisha athari za matumizi ya lugha zungumzi kwa matamshi fasaha ya Kiswahili sanifu. Isitoshe, tumetoa ufafanuzi wa matokeo haya kwa njia ya majadiliano huku tukiyahusisha matokeo hayo na ithibati, kazi na tafiti za awali ambazo zilikuwa zimehakikiwa katika sura ya pili. Muhtasari wa matokeo muhimu ya utafiti huu pamoja na mapendekezo ya utafiti zaidi yamewasilishwa katika sura ya tano.

SURA YA TANO

MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

5.1 Utangulizi

Sura ya tano imehitimisha uchunguzi huu kwa kuwasilisha muhtasari wa matokeo ya utafiti huku ikitoa mapendekezo ya utafiti zaidi. Utafiti huu ulinuiwa kuchunguza ruwaza za matumizi ya lugha zungumzi na kubainisha athari za ruwaza hizi kwa matamshi fasaha ya Kiswahili miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili wilayani Siaya.

Matokeo ya uchunguzi huu yalithibitisha kuwepo kwa ruwaza mahsusi za matumizi ya lugha zungumzi na kwamba ruwaza hizi ziliathiri usahihi wa matamshi katika uzungumzi wa wanafunzi wa shule za upili wilayani Siaya kama tulivyokuwa tumekisia awali katika nadharia tete zetu.

5.2 Muhtasari wa Matokeo Muhimu

Uchunguzi wa ruwaza za matumizi ya lugha zungumzi ulidhihirisha kuwa mazungumzo miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili wilayani Siaya yalitekelezwa katika mazingira ya wingilugha. Hata hivyo, mbali na Kiswahili na Kiingereza, Dholuo ilikuwa lugha muhimu na maarufu katika mazungumzo ya walimu (70%) na ya wanafunzi wao (98%) vilevile. Sheng kwa upande mwingine ilibainika kama lugha ya wanafunzi (69%) lakini haikuwa maarufu miongoni mwa walimu wao.

Shule zote tano zikichukuliwa pamoja, hazina ya lugha wazijuazo wanafunzi wengi ni Kiingereza, Lugha ya Kwanza, Kiswahili na Sheng. Kati ya wanafunzi wote walioshiriki katika uchuguzi huu, 89% walizungumza Lugha ya Kwanza moja, yaani Dholuo. 11% walitumia kati ya Lunyole, Luloogoli, Kikamba, Kikisii, Gikuyu na Kinandi kama lugha zao za kwanza. Baadhi ya wanafunzi wanatumia zaidi ya lugha mbili za kigeni na za kikabila.

Kuhusu matumizi ya lugha katika mawanda mbalimbali wanafunzi wengi walitaja Kiingereza kuwa lugha ambayo wangeweza kuisoma na kuandika kwa urahisi na haraka zaidi. Mazungumzo mengi kati yao ama yalifanyika kwa Sheng au Lugha ya Mama. Usikilizaji nao uliripotiwa kutekelezeka vyema zaidi kupitia kwa Kiswahili.

Lugha ya Mama ilishamiri zaidi kimatumizi katika shule za kutwa kwa sababu wanafunzi wengi walizungumza Lugha ya Mama moja. Isitoshe Lugha ya Mama ilitawala takriban mazungumzo yote nyumbani na katika majadiliano yote ya mada zisizo za kiusomi katika shule hizi. Kwa upande mwingine, Sheng ilikuwa maarufu zaidi katika shule za bweni ambazo zilikuwa na wanafunzi waliozungumza Lugha ya Mama tofauti.

Sheng na Lugha ya Mama ndizo lugha zilizotawala midahalo mingi ya watafitiwa nyumbani. Sheng ndiyo lugha iliyotumiwa katika mazungumzo na marafiki ilhali mazungumzo na wazazi yalifanyika katika Lugha ya Mama. Wanafunzi wengi walieleza kusoma magazeti na mjarida ya Kiingereza mara kwa mara. Walisikiliza vipindi vya redio katika Kiswahili kuliko Kiingereza, Sheng au Lugha ya Mama. Kiingereza kilibainika kuwa lugha maarufu zaidi katika mawasiliano kupitia uandishi wa barua.

Shuleni, Kiingereza ndiyo lugha iliyokuwa maarufu katika mazungumzo na walimu katika takribani shule zote. Walimu waliathiri uteuzi wa lugha iliyotumiwa na wanafunzi katika mazungumzo nao. Wanafunzi wengi waliripoti kutumia Sheng katika mazungumzo na wenzao kutoka shule zingine. Walijadiliana mada zilizohusu masomo yote katika Kiingereza isipokuwa somo la Kiswahili ambalo lililazimu matumizi ya Kiswahili. Mada za kiutamaduni au mada nyinginezo zisizohusiana na shughuli za kiusomi zilijadiliwa pakubwa katika Lugha ya Mama na kwa kiwango kidogo Sheng katika miktadha ambapo wanafunzi walizungumza Lugha ya Mama tofauti.

Sheng ndiyo lugha iliyotumika mahali mbalimbali mwa maingiliano katika shule zote isipokuwa katika shule moja ambamo Lugha ya Mama ilitamalaki kwingi. Kilichoibuka ni kwamba sera ya lugha katika shule nyingi haizingatiwi vizuri sana. Shule moja pekee ndiyo iliyoonyesha ufanisi kwa kiwango fulani.

Umilisi wa kutumia lugha zungumzi ya Kiswahili miongoni mwa wanafunzi katika shule nyingi ulielezwa na walimu kuwa 'wastani', wachache walielezwa kuwa 'hawana ufasaha'. Karibu shule zote zilipatikana kuwa na 'matamshi dhaifu'. Shule moja pekee ndiyo iliyokuwa na 'matamshi mazuri' na ingine ikapatikana kuwa na 'matamshi wastani'. Hakuna shule iliyogezwa kuwa na 'Matamshi mazuri sana' wala 'Matamshi finyu mno' katika Mjarabu na Mjadala.

Kwa kulinganisha ruwaza za matumizi ya lugha na umilisi wa lugha zungumzi kimatamshi kwa kila shule tulifikia hitimisho kuwa wanafunzi waliofanya vyema katika Mtihani wa Majaribio na Mjadala, yaani wenye 'matamshi mazuri' au 'matamshi wastani'ni wale waliotumia ama Sheng au Kiswahili katika miktadha mingi ya mazungumzo yao. Kwa upande mwingine, wale waliopatikana kuwa na matamshi dhaifu ni wale waliotumia lugha zingine katika mazungumzo yao - hasa ya kwanza - mbali na Kiswahili.

5.3 Hitimisho

Uchunguzi huu ulinuiwa kuchunguza ruwaza za matumizi ya lugha zungumzi na kubainisha athari za ruwaza hizi kwa matamshi fasaha ya Kiswahili miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili wilayani Siaya. Deta iliyopatikana ilibainisha kuwa wanafunzi wengi waliteua na kutumia ama Lugha ya Mama au Sheng katika mazungumzo yao. Matumizi ya Lugha ya Mama na Sheng kwa upande mmoja ni dhihirisho la umilisi au ujuzi wao katika lugha hizi. Kwa upande mwingine, kutotumia Kiswahili vilevile ni dhihirisho la udhaifu wao katika kuizungumza lugha hii kwa ufasaha. Hali hii iliwanyima fursa adimu ya kujizoesha na kujifundisha Kiswahili

fasaha kwa kuvumbua maana, sheria za kisarufi na matamshi sahihi mbalimbali yanayoweza kupatikana katika lugha yenyewe kwa kushiriki katika mazungumzo mara kwa mara kupitia kwayo.

5.4 Mapendekezo

Uhalisia kwamba kuna haja ya kushughulikia tatizo sugu la ukosefu wa umilisi wa lugha zungumzi miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili ni jambo ambalo haliwezi kuepukika wala kupuuziliwa mbali. Kutuwezesha kushughulikia jambo hili, sehemu ifuatayo imetumiwa kutoa mapendekezo kuhusu jinsi ya kulitatua suala hili.

Vijana wengi huathiriwa pakubwa na utamaduni pendwa na lugha ya vyombo vya habari kama vile filamu, runinga, muziki, magazeti, majarida,magazini pamoja na ngoma. Ujumbe wa vyombo hivi uwasilishwe kwa Kiswahili sanifu na fasaha kwa manufaa ya umma kwa jumla na vijana hasa.

Waaidha, inawezekana kuwashajiisha wanafunzi wa shule za upili kutumia lugha zungumzi ya Kiswahili kwa namna mbalimbali kama vile:

a) Walimu wapende Kiswahili ili wawe viigwa bora kwa wanafunzi wao. Wazungumze Kiswahili kila wakati na kwa ufasaha. Hali hii itawavutia na kuwahimiza wanafunzi kuionea fahari.

b) Waalikwa waje mara kwa mara kuwahamasisha na kuwazungumzia wanafunzi kuhusu dhima ya Kiswahili.

c) Wanafunzi washughulishwe katika mambo ya sanaa, vyama vya Kiswahili na uandishi wa makala magazetini, majaridani na hata ya vitabu vya Kiswahili. Wahimizwe kutumia lugha fasaha ya Kiswahili kila wakati, kusikiliza vipindi vyenye Kiswahili fasaha na kusoma makala yenye lugha fasaha.

d) Wanafunzi wahimizwe kuwasiliana na kuingiliana katika shughuli kama vile kuigiza, tajiriba, vikundi, utatuzi wa mambo na mijadala huku wakizungumza Kiswahili sanifu.

5.5 Mapendekezo ya Utafiti Zaidi

Kutokana na matokeo ya uchunguzi huu, yafuatayo ni mapendekezo ya utafiti zaidi katika fani hii ya lugha:

1. Uchunguzi huu ulishughulikia matamshi fasaha kama kipengele kimoja cha kiisimu kinachoathiriwa na ruwaza za matumizi ya lugha zungumzi miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili. Hata hivyo, ipo haja ya tafiti zingine kushughulikia athari za ruwaza za matumizi ya lugha zungumzi kwa vipengele kama sarufi, maana na mawasiliano.
2. Uchunguzi huu uliwahusu wanafunzi wilayani Siaya. Tafiti zingine zinafaa kufanywa katika sehemu zingine nchini Kenya ili kuthibitisha ufaafu wa vifaa, mbinu na nadharia iliyotumiwa kwa matumizi mapana zaidi.
3. Uchunguzi wetu umeonyesha kuwa wanafunzi wanaozungumza Sheng na wala sio Lugha ya Mama ndio waliosheheni matamshi mazuri mazuri katika Kiswahili. Kutokana na utambuzi huu, kuna uhitaji wa utafiti kueleza athari za Sheng kwa uzungumzi wa Kiswahili sanifu miongoni mwa vijana.

MAREJELEO

Abdul Aziz na Osinde, K. N. (1997) "Sheng and English: Development of mixed codes amoung urban youth in Kenya" katika *International Journal of the Sociology of Language 125: 42- 63*

Aswani, B. et al. (2006) *Isimujamii kwa Wanafunzi wa Kiswahili.* Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.

Atsenga, M. P. (2002) *Factors Affecting the Teaching of Oral Communication Skills in Vihiga and Kakamega Districts*. (Unpublished M. ED. Thesis, Egerton University.).

Beja, K. S. (2001) "Language and Entrepreneurship: A case of small-scale Business in Kenya".Katika Labdo, U.M. (ed) (2001): *Islamic University Journal Vol.2 No 2. December, 2001*, Mbale- Uganda: Islamic University.

Brown, G. na Yule, G. (1983) *Teaching the spoken Language: An Approached Based on the Analysis of Conversational English*. Cambridge: Cambridge University Press.

Brumfit, C. L. (1976) "Communication and Learning to Use English" Katika *English Language Teaching Journal.*

Byne, (1976) *Teaching Oral English*. New York: Longman.

Chimerah, R. (2000) *Kiswahili: Past, Present and Future Horizons.* Nairobi: Nairobi University Press.

Chomsky, N. (1957) *Syntactic structures*. The Hague: Mouton Press.

Crystal, D. (1987) *Cambridge Encyclopedia of Language*. Cambridge: Cambridge University Press.

Dahl, S. na Johnson, D. (1978): *The Relationship Between Oral Language and Teaching Achievement*. London: Longman.

Dorian, N. C. (1981) *Language Death*: *The Life Cycle of a Scottish Gaelic Dialect.* Pennsylvania: Pennsylvania University Press.

D'souza, H. (1987) *Kenyan Education in its African Context Volume 2*. New York; Vintage Press.

Fasold, R. (1984) *The Sociolinguistics of Society.* New York: Blackwell Publishers Inc.

Fishman, J. A. (1965) "Who Speaks What Language to Whom and When" Katika Hoffmann, C. (1994): *An Introduction to Bilingualism*. London: Longman.

Fishman, J. A. (1972 a) *The Sociology of Language.* Massachusets: Newbury House-Rowley.

Gakuru, O. N. (1979) *Pre-School Education Access to Educational Opportunities in Nairobi.* (Unpublished MA. Thesis, University of Nairobi, Nairobi.).

Gorman, T. P. (1974) "Patterns of Language Use Among Schools Children and their Parents" Katika Whiteley, W. H. (1974). *Language in Kenya.* Nairobi: Oxford University Press.

Gorman, T. P. (1974) "The Development of Language Policy in Kenya with Particular Reference to the Education System." Katika Whitely, W. H (1974). *Language in Kenya.* Nairobi: Oxford University Press.

Gorman, T. P. (1974) "The Teaching of Languages at Secondary Level: Some Significant Problems." Katika Whiteley, W. H (1974). *Language in Kenya.* Nairobi: Oxford University Press.

Gorman, T. P. (1971) "Sociolinguistic Implications of a choice of Media of Instructions." Katika Whitely, W. H. (1971). *Language use Social Change: Problems of Multilingualism with Special Reference to Eastern Africa.* London: Oxford University Press.

Hammerly, H. (1991) *Fluency and Accuracy: Towards Balance in Language Teaching and Learning.* Clevedon: Multilingual Matters Limited.

Hatch, E. (1978) "Discourse Analysis and Second Language Acquisition" katika Hatch, E. (mhariri) *Second Language Acquisition: A Book of Readings.* Rowley, Massachusetts: Newbury House (Uk.401-435).

Hemphill, R. J. (1974) "Language Use and Language Teaching in Primary Schools of Kenya" Katika Whitely (Mhariri) (1974). *Language in Kenya.* Nairobi: Oxford University Press.

Hopkins, T. (1977) "The Development and Implementation of the National Language Policy in Kenya" Katika Kotey, P.F. na Der-Houssikian, H.(Wahariri) (1977) *Language and* Linguistics Problems in Africa. London Hornbeam Press.

Hudson, R. A. (1980) *Sociolinguistics.* Cambridge: Cambridge University Press.

Hughes, A.(1989) *Testing for Language Teachers.* Cambridge: Cambridge University Press.

Hughes, R. (1990) "The Family as an Educator in Kenya" in *Kenya Journal of Education 4 (2)* Nairobi.

Hymes, D. (1971): *Communication Competence in Language Learning.* London: Oxford University Press.

Jumba, P. (1997) *Language Use in Schools.* Nairobi: Nairobi University Press.

Kaniu, M. G. (2003) *Patterns of Language Use and their Effects on the Acquisition of English Oral Communication Skills: A case Study of Secondary Schools Students in Kandara Division of Maragwa District.* (Unpublished M.A Thesis, Egerton University).

Kathuri, N. J. (1984) "Some Factors which Influence the Performance of Pupils in the Certificate of Primary Education". *Institute of Development Studies (IDS) Working Paper 401.* Nairobi: University of Nairobi.

Kenya Institute of Education (KIE) (2002) *Secondary School Syllabuses (Volume Five).* Nairobi:Kenya Literature Bureau.

Kiessling, Roland & Mous, Maarten (2001) "Urban Youth Languages in Africa". Paper presented at the conference on Language, Migration and the City, 22 – 24, November 2001. Bayreuth: University of Bayreuth.

Kimemia, J. N. (2001) *Kiswahili: The Dilemma of Developing the National Language.*Njoro: Egerton University Press.

King'ei, G. K. na Musau, P. M. (2002) *Utata Wa Kiswahili Sanifu.* Nairobi: Didaxis Resources and Services.

Kizito, N. D. (2002) *Mielekeo Kuhusu Taarifa ya Habari: Uchunguzi Katika Mtaa wa Komarock Jijini Nairobi.* (Unpublished M. A. Thesis, Kenyatta University, Nairobi.).

Labdo, U. M. (Mhariri) (2001) Islamic *University Journal Volume 2 Number 2, December 2001.*Mbale Uganda: Islamic University.

Lumbasio, P.A (1990) *:A Historical Study Of Kiswahili in Kenya: A Project Submitted to Kenyatta University in Partial fulfillment of post graduate diploma in education.* (Unpublished).

Marylyn (1978) *Investigations in Language use in Kenya.* Nairobi: Nairobi University Press.

Mazrui, A. A. na Mazrui, A. M. (1995) Swahili *State and Society: the Political Economy of An African Language.* Nairobi: East African Educational Publishers.

Mbaabu, I. (1995) *Usahihishaji Wa Makosa Katika Kiswahili.* Nairobi: Longhorn Kenya Limited.

Mbaabu, I. (1985) *New Horizons in Kiswahili: A Synthesis in Developments, Research and Literature.* Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Mbaabu, I. (1978) *Kiswahili: Lugha ya Taifa.* Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Miguda-Attyang, J. (2002) *The Emergence Of Sheng in Nairobi: A Socio-Psychological Perspective.* Unpublished Ph.D Dissertation. Delhi: University of Delhi.

Milroy, L. (1987) *Observing and Analyzing Natural Language.* New York: Basil Blackwell.

Mkilifi, A. (1987) *Language Use Dynamics.* Nairobi: Nairobi University Press.

Mukunya, E. W. (1994) *An Investigation of The Factors Influencing The Acquisition of The Reading Skills in Kiswahili at Form Three Level in Secondary Schools Selected From Nairobi Province.* (Unpublished PGDE. Thesis, Kenyatta University, Nairobi.).

Mukuria (1995) "Kenya's Language Policy Developments with Special Emphasis on Kiswahili" Katika Senana, K. na Williams, D. (Wahariri) (1995) *Creative Use of Language in Kenya.* Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.

Mukuthuria, M. (2001) "Matatizo yanayokabili Kiswahili Karne ya ishirini na moja" Katika Labdo, U. M. (Mhariri) (2001) *Islamic University Journal Vol 2 No 2 December 2001.* Mbale –Uganda: Islamic University.

Musau, P. M. na Chacha, L. M. (2001) *Mbinu za Kisasa za kufundishia Kiswahili Kwa`Walimu wa shule za Msingi upili na vyuo.* Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Ngesa, Mildred (2002) *Trilingual Code-Switching in Kenya: Evidence from Ekegusii, Kiswahili, English and Sheng.* Unpublished PhD Dissertation. Hamburg: University of Hamburg.

Nyang'anya, J. A. (1997) *Sheng: Emerging Language in Kenya.* Unpublished MA Dissertation. Institute ofEducation, University of London.

Obura, A. P. (1991) "Language in Conflict in Education in Anglophone Africa: The Role of Languages in Primary Education in Eastern Africa with Special Reference to Kiswahili"- A Paper Prepared for International Kiswahili Workshop, Dar es Salaam, 1991.

Onyango, J. O. (1990) *Mielekeo ya Wasomi Kuhusu Matumizi ya Lugha Kiswahili nchini Kenya.* (Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Kenyatta, Nairobi. Haijachapishwa).

Ongechi, N. O. (2003) "On Language Rights in Kenya." Katika *Nordic Journal of African Studies 12(3)*: 277 – 295.

Osinde, K. N. (1986) Sheng: *An Investigation into the Social and structural Aspects of an Evolving Language* (Unpublished BA. Dissertation, University of Nairobi).

Rukia, N. B.(1992) *An investigation in the Causes of Pupils Errors in Kiswahili Composition Writing in Upper Primary Classes in Bungoma Municipality.* (Unpublished M.ED. Thesis, Kenyatta University, Nairobi.).

Saussure, F. (1916) *Course in General Linguistics*. New York: McGraw-Hill

Seliger, G. (1971) *Communicating in Second Language*. London: London University Press

Seliger, H. W. na Shohamy, E. (1990) *Second Language Research Methods*. London: Oxford University Press.

Senana, K. na Williams, D. (1995) *Creative Use of Language in Kenya.* Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.

Simon, J. (1980) *Paradigms Lost: Reflections on Literacy and its Decline*. New York: C. Potter Inc.

Wardhaugh, R. (1986) *An Introduction to Sociolinguistics.* New York: Blackwell Publishers.

Webb, V. & Kembo-Sure (2000) *African Voices: An Introduction to the Languages and Linguistics of Africa.* Cape Town: Oxford Press Southern Africa.

Whiteley, W. H. (Mhariri) (1971) *Language use Social Change: Problems of Multilingualism with Special Reference to Eastern Africa.* London: Oxford University Press.

Whiteley, W. H. (Mhariri) (1974) *Language in Kenya.* Nairobi: Oxford University Press.

KIAMBATISHO A

HOJAJI KWA WANAFUNZI

Maagizo:

(a) Kupitia kwa hojaji hii, tungependa kupata habari kuhusu matumizi yako ya lugha mbalimbali na umilisi wako wa lugha zungumzi ya Kiswahili.

(b) Huu si mtihani kwa hivyo hakuna majibu yaliyo sawa wala yasiyo sawa.

(c) Soma kila swali kwa makini kabla ya kulijibu.

Sehemu A

Habari za kibinafsi:

Tafadhali onyesha habari zinazokuhusu kibinafsi kwa kuweka alama (√) pafaapo.

(a) Jinsia: Mvulana ( ) Msichana ( )

(b) Shule:

Shule ya Bweni ya Wasichana	( )
Shule ya Bweni ya Wavulana	( )
Shule ya Kutwa ya Mseto	( )
Shule ya Mseto ya Kutwa na ya Bweni	( )

Sehemu ya B

Katika sehemu ifuatayo ama onyesha msimamo wako kuhusu kauli zilizotolewa kwa kuweka alama (√) kwa jibu lako au jaliza nafasi zilizoachwa wazi baada ya kila swali.

1.

a.) Je, unazungumza lugha ngapi? _____

b.) Tafadhali zitaje lugha hizo:

i _____

ii _____

iii _____

iv _____

v _____

c.) Kati ya lugha ulizozitaja hapo juu, ni ipi unayoitumia zaidi katika Mawanda yafuatayo?

(Stadi zifuatazo)

Kuzungumza _____

Kusikiliza _____

Kuandika _____

Kusoma _____

Ni lugha ipi unayoitumia sana katika miktadha ifuatayo:-

a.) Unapozungumza na wazazi nyumbani? _____

b.) Unapozungumza na ndugu na dada zako? _____

c.) Unapozungumza na marafiki ambao ni jirani zako? _____

d.) Unapoandika barua kwa marafiki? _____

e.) Unapoandika barua kwa wazazi? _____

f.) Unapoandika barua kwa wengine? _____

g.) Unapopiga gumzo na marafiki nje ya shule: _____

2.

a.) Kwa maoni yako, babako anazungumza vipi lugha zifuatazo?

Kiswahili _____

Kiingereza _____

Sheng _____

i) Vizuri sana

ii) Vizuri

iii) Sio vizuri sana

iv) Haijui hata kidogo

Kwa maoni yako, mama yako anazungumza vipi lugha zifuatazo

Kiswahili_____

Kiingereza_____

Sheng _____

- Vizuri sana
- Vizuri
- Sio vizuri sana
- Haijui hata kidogo

b.)

i) Je, wazazi wako wameweka vikwazo vyovyote kuhusu matumizi ya lugha fulani nyumbani?

Ndio ( ) La hasha ( )

ii) Ikiwa jibu lako ni ndio, je, ni lugha ipi/zipi isiyopendekezwa /zisizopendekezwa? Kwa nini? (Toa sababu ya jibu lako)

_____

_____

_____

_____

3. Ukiwa shuleni, ni lugha ipi unayotumia zaidi katika miktadha ifuatayo:

a.)Unapozungumza na mwalimu. _____

b.)Unazungumza na wanafunzi kutoka shule nyingine _____

c.)Unapozungumza na wanafunzi wenzako:

i Darasani_____

ii Bwenini _____

iii Uwanjani wakati wa michezo _____

iv Katika Ukumbi wa Maakuli _____

v Mkiwa njiani kuelekea Nyumbani _____

- Lugha ya mama pekee
- Lugha ya mama hasa
- Kiswahili hasa
- Kiswahili pekee
- Kiingereza hasa
- Kiswahili na Kiingereza
- Kiswahili na Lugha ya mama
- Kiingereza na Lugha ya mama
- Sheng

4. Ni lugha ipi/zipi unazozitumia sana katika majadiliano na wanafunzi wenzako kuhusu mada zifuatazo:-

(a) Hisabati (Hesabu) _____

(b) Kemia _____

(c) Fasihi Katika Kiingereza _____

(d) Fasihi katika Kiswahili _____

(e) Sherehe ya kitamaduni _____

5.

i) Je, waweza kuelezaje usikilizaji wako wa vipindi vya redio katika lugha zifuatazo:

(a) Kiswahili _____

(b) Kiingereza _____

(c) Lugha ya mama _____

(d) Sheng _____

- Mara kwa mara
- Mara moja moja
- Kwa nadra sana
- Hata!/Hata kidogo

ii) Eleza kwa kifupi usomaji wako wa magazeti na majarida katika lugha zifuatazo:

(a) Kiswahili _____

(b) Kiingereza _____

(c) Lugha ya Mama _____

(d) Sheng _____

- Mara kwa mara
- Mara moja moja
- Kwa nadra sana
- Hata!/Hata kidogo

6.Sera ya lugha shuleni.

a.) Je kuna sera inayoongoza matumizi ya lugha shuleni mwako?

Ndio ( ) La ( )

Iwapo ndio, fafanua _____

_____

_____

_____

b.) Unaizingatiaje sera ya lugha katika matumizi yako ya lugha shuleni? Eleza.

_____

_____

_____

_____

Vizuri sana Siizingatii vizuri sana

Vizuri Siizingatii hata kidogo

c.) Kwa maoni yako unapendekeza lugha ipi itumike kama njia ya mawasiliano shuleni?

_____

d.) Toa sababu ya jibu lako katika (c) hapo juu _____

_____

_____

_____

7. Mbali na kwamba stadi ya kuzungumza haitahiniwi je, unafikiri kuna manufaa ya kuwa na umilisi wa kutumia lugha zungumzi fasaha ya Kiswahili?

Ndio ( ) La ( )

Iwapo ndio, manufaa hayo ni yapi?

_____

_____

NASHUKURU

KIAMBATISHO B

HOJAJI KWA WALIMU WA LUGHA

Maagizo ya kijumla:

(a) Tungependa kujua maoni yako kuhusu ruwaza za matumizi ya lugha miongoni mwa wanafunzi shuleni mwako na athari zake kwa umilisi wa lugha zungumzwa fasaha ya Kiswahili.

(b) Huu si mtihani, kwa hivyo hakuna majibu yaliyo sawa wala yasiyo sawa.

(c) Isome Hojaji nzima kwa makini kabla ya kujibu kila swali kwa ukamilifu.

Sehemu A

Habari za Kibinafsi

Tafadhali onyesha habari zinazokuhusu kibinafsi kwa kuweka alama (√) pafaapo.

(a) Jinsia: Mume ( ) Mke ( )

(b) Shule: Shule ya Bweni ya Wasichana ( )
Shule ya Bweni ya Wavulana ( )
Shule ya Kutwa ya Mseto ( )
Shule ya Mseto ya Kutwa na ya Bweni ( )

(c) Kiwango cha Elimu:

M.E.D	( )	MA	( )
B.E.D	( )	B.A	( )
P.G.D.E	( )	K.C.S.E	( )
D IP	( )	K.A.C.E.	( )

NYINGINE _____

(d) Tajiriba ya kufundisha:

Miaka _____

Sehemu B:

Jibu maswali katika sehemu hii kwa kuweka alama (√) na kujaliza nafasi zilizoachwa wazi baada ya kila swali.

1. (a) Je, unazungumza lugha ngapi?_____

   (b) Tafadhali zitaje lugha hizo:

   (i) _____

   (ii) _____

   (iii) _____

   (iv) _____

2. (a) Je wanafunzi hutumia lugha ngapi katika mazungumzo yao shuleni?

   _____

   (b) Tafadhali zitaje lugha hizo:

   (i) _____

   (ii) _____

   (iii) _____

   (iv) _____

   (c) Kati ya lugha zinazozungumzwa na wanafunzi, ni ipi wanayoitumia sana?

   _____

   (d) Kwa maoni yako, unafikiri ni kwa nini wanafunzi wanaipendelea lugha uliyoitaja katika 2 (c) hapo juu?_____

   _____

   _____

   _____

3. (a) Je, kuna sera yoyote ya lugha shuleni?

   Ndio ( ) La ( )

   Iwapo ndio, eleza kwa kifupi.

   _____

   _____

   _____

(b) Je, lengo kuu la sera hii ya lugha shuleni ni lipi?_____

_____

_____

_____

(c) Unaweza kuelezaje utekelezaji wa sera ya lugha shuleni?

( ) Umefanikishwa vizuri sana

( ) Umefanikishwa kwa kiwango fulani

( ) Hauna mafanikio makubwa

( ) Utekelezaji haupo hata kidogo

(d) Ni matatizo yapi mnayokumbana nayo katika utekelezaji wa sera ya lugha shuleni?_____

_____

_____

_____

4. a) Kati ya viwango vifuatavyo, ni kipi kinachoeleza kwa usahihi umilisi wa wanafunzi wako katika kutumia lugha zungumzi ya Kiswahili.

( ) Wanazungumza kwa ufasaha mkubwa

( ) Wanazungumza kwa ufasaha wastani

( ) Hawana ufasaha katika mazungumzo

( ) Ni wadhaifu mno

b)Kwa maoni yako, unadhani matumizi ya lugha ya wanafunzi yaathiri ujifunzaji wao wa lugha zungumzi fasaha ya Kiswahili?

Ndio ( ) La ( ) Sina uhakika ( )

Iwapo ndio vipi? _____

_____

_____

_____

5(a) "Mbali na kuwa lugha ya taifa letu, imekadiriwa kuwa lugha ya Kiswahili inazungumzwa na mamilioni ya wakazi wa mataifa mbalimbali yanayoungana pamoja ili kurahisisha maingiliano kibiashara, kijamii, kitamaduni, n.k" (K.I.E. 2002:23). Je, wanafunzi wako wanajuaje ukweli huu?

( ) Vizuri sana ( ) Vizuri

( ) Sio vizuri sana ( ) Hawajui katu

(b) Unaweza kueleza vipi juhudi zako kuwahamasisha wanafunzi wako kuhusu ukweli huu wa (5a) na manufaa ya lugha ya Kiswahili kwao sasa na siku za usoni.

( ) Mara kwa mara ( ) Mara mojamoja

( ) Kwa nadra sana ( ) La hasha

(c) Je, unawahusisha vipi wanafunzi wako katika shughuli za kimtagusano (Kimaingiliano) kama vile mazungumzo, dayolojia, michezo ya lugha, hotuba, tamthilia na mijadala kwenye miktadha na mazingira yanayoakisi hali halisi ?

( ) Mara kwa mara

( ) Mara moja moja

( ) Kwa nadra sana

( ) La hasha

6 (a) Kwa maoni yako, unadhani kutotahiniwa kwa stadi ya Kuzungumza katika mitihani ya kitaifa (KCSE) ni kikwazo kwa ujifunzaji, ufundishaji,na umilisi wa lugha zungumzi fasaha ya Kiswahili?

( ) Ndio ( ) La ( ) Sina uhakika

(b) Kwa maoni yako, kuna uhusiano gani kati ya mawasiliano andishi na zungumzi?

( ) Mawasiliano zungumzi ni kibadala cha mawasiliano andishi.

( ) Mawasiliano andishi ni kibadala cha mawasiliano zungumzi

( ) Mawasiliano zungumzi na andishi huchangiana na kukamilishana

( ) Hakuna uhusiano wowote

(C) Kwa maoni yako, je, lugha zungumzi ya Kiswahili miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili inaweza kuboreshwa? Toa mapendekezo yako. _____

_____

_____

_____

KIAMBATISHO C

MJARABU

Muda: Saa $1^1/_2$

Maagizo

Jibu maswali yote.

Maswali haya yameandaliwa kugeza umilisi wako wa lugha zungumzi ya Kiswahili kimatamshi.

Majibu yako uyaandike katika kijitabu hiki cha maswali.

SEHEMU A (ALAMA 45)

1. Chagua neno linalowakilisha matamshi mwafaka kujazia pengo lililopo katika kila sentensi. (alama 20).

a. Wacheza muziki watakuwa ni_____ya polisi. (pendi, bendi) (alama 1)

b. Baada ya mvua kukosa kwa miaka mingi, kulitokea___la njaa. (janga, changa) (alama 1)

c. Mtoto anayekunywa maziwa kwa wingi huwa na_____nzuri. (afya, afia, avya).(alama 1).

d. Wakati wa jioni wasafiri_____ugali. (walipiga, walipika) (alama 1).

e. Ukitaka kuoa ni sharti uwe na pesa za kutosha za kulipa____(mahari, mahali) (alama 1).

f. Dereva alishtakiwa kwa kuendesha gari lake lenye_____kuukuu. (tairi, tahiri) (alama 1).

g. Inasemekana kwamba kijana huyo _____ugonjwa wa ukimwi. (anaugua, anaungua, anauguwa) (alama 1).

h. Anyango alimwambia mwanawe, "_____hadithi zote upendazo, lakini utakiona cha mtema kuni".(Mbuni, Buni).

i. Sisi _____ni wananchi wa taifa hili. (sote, zote). (alama 1).

j. Mimea yetu_____na mvua. (iliadhiriwa, iliathiriwa, iliasiriwa) (alama 1).

k. Maduka mengi mjini Mombasa huuza _____pamoja na vitu vingine vinavyopendwa na watalii. (changa, shanga, sanga) (alama 1).

l. Haya ni _____ya nyumba zilizobomoka. (magofu, maghofu, makofu). (alama 1)

m. Baba amejenga_____kubwa la mahindi. (kala, ghala, gala). (alama 1)

n. Mwewe alishindwa kumkamata_____(kanga, kaanga, ganga). (alama 1)

o. Baada ya kuacha ulevi, Mzee Karani hafuatani tena na walevi, ama kwa kweli ametupa_____na mti wake. (jongo, jongoo, jogoo) (alama 1)

p. Mama _____chakula.(nililiye, nitilie) (alama 1)

q. Jirani yetu alipanda_____aina ya waridi. (mauwa, maua) (alama 1)

r. Mtoto wake aliendelea_____vizuri. (kukuwa, kukua) (alama 1).

s. Tuli_____(goma, koma) ku_____(koma, goma) kwa vile tuligundua kuwa tusipo_____ (koma, goma) ku_____ (koma, goma) tutafutwa kazi mara moja. (alama 4)

t. Mariamu alivaa blauzi inayom_____(bana, pana) bali ni vizuri kuvaa blauzi_____(pana, bana) isiyo_____(bana, pana) hata kidogo.(alama 4)

u. Baada ya ku_____(jenga, chenga) lile jengo nilitahayari nilipoona vile nilivyoli_____(chenga. Jenga) na kwa hivyo nikaanza kum_____(jenga, chenga) mwenyewe kwa vile hilo_____(jengo, chengo) halikuvutia kamwe. (alama 4).

2. a. Kati ya jozi hizi, andika neno linalowakilisha matamshi sahihi. (alama 5)

   i. Inje na Nje
   ii. Njadi na Jadi
   iii. Sayiri na Shayiri
   iv. Nzi na Inzi
   v. Haki na Aki

b. Kati ya maneno mawili yaliyotolewa ni lipi lililo na maana iliyoonyeshwa (a) na (b) ? (alama 10).

   i. (Ndoa, Doa)
      a. Muungano wa mwanamke na mwanamume
      b. Dosari, ila au kasoro.
   ii. (Suka, Shuka)
      a. Teremka
      b. Tikisa kichwa
   iii. (Apa, Hapa)
      a. Kitendo cha kula kiapo
      b. Mahali
   iv. (Dhana, Zana)
      a. Vyombo vya kufanyia kazi fulani
      b. Fikra au wazo
   v. (Gharama, Karama)

a. Kipawa au uwezo wa kipekee.

b. Matumizi ya pesa

SEHEMU B (ALAMA 55)

3 (a) Tofautisha sentensi zifuatazo:

vi. Nitafua nguo zangu kesho.

Nitavua nguo zangu kesho. (alama 2)

vii. Pilipili hizi ni kali

Pilipili hizi ni ghali (alama 2)

viii. Alilipa mali nyingi

Alilipa mahari nyingi (alama 2)

ix. John alifutwa kazi

John alivuta kasi (alama 2)

x. Makazi haya ni ya nani?

Makasi haya ni ya nani? (alama 2)

(b) Eleza tofauti za kimaana zinazotokana na matamshi ya maneno haya

I. Mwaja, Mwanga (alama 2)

II. Ada, Hadaa, Andaa. (alama 3

4 Sentensi zifuatazo ni zao la matamshi mabaya. Ziandike upya ili zionyeshe matamshi sahihi na fasaha.

a. Kingeresa ni luga ya kingeni inchini Kenya. (alama 2)

b. Zainabu anambabaika bure kuusa uamusi ya kamiti ya sule. (alama 2)

c. Baadhi ya watu wamefika mapema. (alama 2)

d. Umarufu wa bondia Achieng'umenea kwote.

e. Juma amenda kusalamia ndugu na marafiki. (alama 2)

f. Inchi wa Kenya huenda itakuwa na katiba mapya mwakani.(alama 2)

g. Ukishoma bibilia utaelewa nema ya Mungu. (alama 2)

h. Urefu wa musumari huu ni nchi sita. (alama 2).

i. Himza watu wajunge na chama ya giografia. (alama 2).

j. Africa mashariki nzima ina mualimu mumoja wa soshiologia. (alama 2)

5 Tunga sentensi mbili mbili kwa kila jozi ya maneno yafuatayo ili kuonyesha kwamba unayatofautisha kimatamshi.

a. Chora, jora. (alama 2)

b. Mbari, bali (alama 2)

c. Fuga, funga (alama 2)

d. Bundi, budi (alama 2

e. Bao, mbao (alama 2)

f. Jana, njana (alama 2)

g. Thibiti,dhibiti (alama 2)

h. Samani, thamani (alama 2)

i. Ghaya, gaya (alama 2)

j. Koma, komaa (alama 2)

KIAMBATISHO D

MWONGOZO WA MAHOJIANO NA MWALIMU

1. Je, ni lugha zipi zinazotumiwa na walimu na wanafunzi hapa shuleni?

2. Lugha hizi ulizozitaja huzungumzwa na wanafunzi lini na katika miktadha ipi? Tafadhali fafanua.

3. Kati ya lugha hizi, ni ipi inayopendelewa zaidi na wanafunzi katika mazungumzo yao? Kwa nini ?

4. Je, kuna sera yoyote ya lugha hapa shuleni? Eleza kwa kifupi.

5. Eleza kwa kifupi hali ya Kiswahili hapa shuleni.

6. Unaweza kusema nini kuhusu Kiswahili kinachozungumzwa na wanafunzi hapa shuleni?

7. Kama lugha sambazi na ya taifa, Kiswahili kinapasa kupewa nafasi muhimu sana katika nyanja mbalimbali za maisha. Je, unadhani Kiswahili kimepewa hadhi kinayoistahiki katika matumizi hapa shuleni?

8. Iwapo la, unafikiri ni kwa nini?

9. Unapendekeza hatua gani zichukuliwe ili kuboresha lugha zungumzi ya Kiswahili miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili?

KIAMBATISHO E

MFUMO WA UAINISHAJI WA MATAMSHI

A	80 – 100	**MATAMSHI MAZURI SANA**
A-	75 -79	
B+	70 -74	**MATAMSHI MAZURI**
B	65 – 69	
B-	60 -64	
C+	55 -59	**MATAMSHI WASTANI**
C	50 -54	
C-	45 – 49	
D+	40 -44	**MATAMSHI DHAIFU**
D	35 – 39	
D-	30 – 34	
E	00 – 29	**MATAMSHI FINYU MNO**

KIAMBATISHO F

SHULE ZA UPILI WILAYANI SIAYA

1.0 Shule za Bweni za Wasichana (11)

1. Aluor Girls'
2. Bishop Okoth Mbaga
3. Got Osimbo Girls'
4. Hawinga Girls'
5. Mutumbu Girls'
6. Ng'iya Girls'
7. Rang'ala Girls'
8. Sega Girls'
9. Sinaga Girls'
10. St.Julian's Academy
11. Nyawara Girls'

2.0 Shule za Bweni za Wavulana (08)

1. Ambira Boys'
2. Barding Boys'
3. Maliera Boys'
4. Mwer Boys'
5. Rang'ala Boys'
6. Sawagongo Boys'
7. St. Mary's Yala Boys'
8. Ukwala Boys'

3.0 Shule za Kutwa (Mseto) (49)

1. Agoro Oyombe Mixed
2. Alambo Lake Side
3. Anyiko Mixed
4. Apuoyo Mixed
5. Argwings Kodhek
6. Boro Mixed
7. Siaya Academy
8. Siaya Township
9. Sidindi Mixed
10. Simenya Mixed
11. Sirembe Mixed
12. Tingare Mixed
13. Ulumbi Mixed
14. Umina Mixed
15. Uranga Mixed
16. Yenga Mixed
17. Sigomre Mixed
18. Obambo Mixed
19. Dienya Mixed
20. Holy Cross Mixed
21. Hono Mixed
22. Inungo Mixed
23. Humweno Mixed
24. Jera Mixed
25. Kogelo Mixed
26. Kaudha Mixed
27. Kagonya Mixed
28. Kambare Mixed
29. Madungu Mixed
30. Miyare Mixed
31. Mbaga Mixed
32. Moi Uloma Mixed
33. Mudhiero Mixed
34. Ndenga Mixed
35. Ndere Mixed
36. Ndori Mixed
37. Nyalunya Mixed
38. Nyabeda Mixed
39. Nyagondo Mixed
40. Nyambare Mixed
41. Nyamninia Mixed
42. Nyang'ang'a Mixed
43. Nyang'ulu Mixed
44. Nyasanda Mixed
45. Rambula Mixed
46. Sagam Mixed
47. Sega Township Mixed
48. Sihay Mixed
49. Siginga Mixed

4.0 Shule za Mseto za Kutwa na Bweni (03)

1. Christian (Ya Kibinafsi)
2. Jubilee (Ya Kibinafsi)
3. Horace Ongili

JUMLA = SHULE 71

EGERTON UNIVERSITY LIBRARY